# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

## KCSE NATIONAL SCHOOLS TRIALS AND JOINT SERIES 2025

# KISWAHILI PAPER 2

KABARAK HIGH
ALLIANCE BOYS
ALLIANCE GIRLS
ASUMBI GIRLS
CRESCENDO JOINT
EAGLES JOINT
KISII SCHOOL
KENYA HIGH
LANJET JOINT
MANGU SCHOOL
MARANDA SCHOOL
MASENO SCHOOL
MERU SCHOOL
MIRROR JOINT
MOKASA JOINT 1
MOMALICHE
STAREHE GIRLS

**Compiled and distributed by Goldlite Online Supplies. For these and more inbox/text / WhatsApp 0724351706/0726960003. Marking schemes are available. Inbox now**

***These exams have been compiled from recently done national schools' trials and joint series***

***KNEC COMPLIANT***

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: ……………………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ………………DARASA: …............**

# SHULE YA UPILI YA KABARAK

**102/2**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA PILI**

**Maagizo**

***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

***b)*** *Jibu maswali yote.*

***c)*** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*

***d)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE**

| **SWALI** | **UPEO** | **ALAMA** |
|---|---|---|
| 1. UFAHAMU | 15 | |
| 2. UFUPISHO | 15 | |
| 3. SARUFI | 40 | |
| 4. ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**UFAHAMU (ALAMA 15)**

Katiba ni utaratibu wa sheria unaoweka mpango wa jamii kuendesha mambo. Ni muhimu kila raia ajue ya nchi yake.

Katiba yaweza kuwa imeandikwa au haikuandikwa. Katika hamii za jadi,katiba ilihifadhiwa na kupokezwa kwa mdomo. Mtindo wa kuandika katiba ulianza nchini Marekani mwaka 1787. Ingawa katiba hii imefanyiwa mabadiliko hap na pale, bado ni ileile. Kenya ilipowekwa china ya himaya ya Uingereza mwaka 1895, ilianza kutumia katiba ya Uingereza. Baada ya masetla wa kikoloni kujikita, Kenya kuwa koloni. Hii ililazimu pawe na katiba nyingine mwaka 1920. Waafrika waliupinga mfumo huu kwa sababu haukuwahusisha kikamilifu kwenye masuala ya uongozi. Utetezi wa wanasiasa ulilazimisha serikali ya Uingereza kuitisha makongamano mbalimbali kama vile ile la Devonshire na mengine ili kurekebisha katiba. Waafrika hawakuridhika. Wakaenda kudai katiba mwafaka. Harakati hizi zilileta kuitishwa kwa kongamano la katiba la Lancaster. Lengo lilikuwa kuandika katiba itakayotumiwa nchini hadi leo. Kati ya wajumbe walioenda Uingereza kuandika katiba mwaka 1962 ni pamoja na Tom Mboya, Jean Marie Seroney, Julius Kiano, Jomo Kenyatta, Masinde Mulilo, Oginga Odinga, Ronald Ngala, Daniel Arap Moi na James Gichuru. Wengine ni Martin Shikuku, Denis Akumu, Taita Towett, Abdilahi Nassir, Jeremiah Nyaga na John Keen.

Katiba ni kitovu cha taifa. Baina ya mambo inayotekeleza ni kuweka utaratibu na kanuni za utawala, kwa mfano, utawala wa kimikoa na serikali za wilaya. Pamoja na haya, katiba hufafanua vyombo vikuu vya serikali, mamlaka yavyo na mipaka yavyo ya kutenda. Vyombo hivi ni mbunge, mahakama, urais, jeshi n.k. Hali kadhalika, katiba hupambanua haki za raia.

Hii hudumisha demokrasia na huwawezesha wananchi kupata uhuru na haki za kimsingi. Katiba hukinga haki za kila raia, hasa kutoka na udhalimu wa wengi au wenye uwezo mkubwa. Zaidi ya yote, Katiba huimarisha asasi za umma ili kudumisha uwajibikaji.

Katiba huhalamishwa na watawaliwa. Hii hutokea wanaposhirikishwa katika uandishi wake. Kuanzia miaka ya themanini, raia walianza kudai katiba igeuzwe. Mwamko wa kutaka mageuzi ulianza kwa harakati za kubadilisha mfumo wa kisiasa ulilenga kuwashirikisha wananchi katika utawala na kuondoa uimla.

Harakati zilitia for a miaka ya tisini. Mambo yaliyochochea hali hii ni mengi. Kwanza, katiba iliyokuwa imeandikwa na watu wachaceh ilikuwa imefanyiwa marekebisho mengi. Marekebisho haya yalimpa rais mamlaka mengi juu ya serikali kuu na vyombo tofauti vya serikali. Pili, viongozi na watu wenye uwezo na utajiri walipuuza katiba. Raia walihisi wanadhulimiwa. Walilpinga hali ya wachache waliomzunguka rais kunufaika huku umma ukitengwa. Tatu, kutokana na uongozi uliokuweko wakati huo, wanawake, watoto na walemavu walidhulimiwa na kukosa uwakilishi ufaao.

Hatimaye, pakawa na ongezeko la uharibifu wa mazingira, ufisadi na unyakuzi wa mali ya umma kama vile ardhi. Waliopigania katiba mpya walikuwa na haja ya katiba ambayo uandikaji wake ungehusisha wakenya wote. Mwanzoni, serikali ilipinga wito wa mabadiliko. Lakini mnamo mwaka 2001 iliunda Tume ya Marekebisho ya

Katiba ili kutekeleza mahitaji ya wananchi. Tume hii iliwahamasisha na kuwashawishi raia kutoa maoni. Tume iliandaa vikao katika maenoe ya ubunge 210 ambapo wananchi walitoa mapendekezo kuhusu marekebisho ya katiba waliyotaka.

Katika mapendekezo hayo raia walisisitiza mambo kadhaa. Jambo la kwanza ni utawala mwema na uwajibikaji wa viongozi na maafisa wa umma. Jambo linguine ni kulinda haki za binadamu zikiwemo za wanawake, watoto na walemavu. Raia walidai kanuni za usawa na ulinganifu. Aidha waliitilia mkazo mahitaji ya msingi kiama chakula, afya nzuri, makao, elimu, usalama, uchumi na kadhalika.

Msingi wa mapendekezo hayo yote ni kuwepo na amani ya kitaifa, umoja na uadilifu ili kulinda maslahi ya wananchi wote na taifa.

**Maswali**

a) Eleza kilicho sababisha kongamano la katiba la Lancaster. (alama 3)

b) Taja mambo matatu yaliyotiliwa mkazo na raia katika maoni yao kuhusu katiba. (alama 3)

c) Eleza umuhimu wa katiba kwa mujibu wa taarifa. (alama 3)

(d)Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa. (alama 3)

i) Kitovu –

ii) Harakati –

iii) Hamasisha –

(e) Taja na ueleze mwafaka wa makala haya. (alama 3)

**MUHTASARI**

**Soma taarifa ifuatayo kwa makini kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Nchi nyingi duniani zimetia mkataba wa umoja wa mataifa kuhusu haki za watoto. Haki ni mambo mema ambayo watoto wanastahili kutendewa. Kwa kutia saini, nchi hizi zimetangaza kujitolea kwao kuzilinda na kuhakikisha kuwa hakuna ukiukaji wake na kuwa watoto wote katika himaya zao wananufaika kutikana na haki hizi.

Miongoni mwa haki hizi ni kuwa kila motto ana haki ya kuishi na kupata chakula cha kutosha na chenye viinilishe bora. Pili, kila mtoto ana haki ya kupata elimu. Elimu hii inafaa kutolewa bila ada na iwe inayofaa na inayopatikana kwa urahisi. Kisha kila motto ana haki ya kutopigwa na kutodumishwa kwa maana yoyote, iwe kitabaka, kirangi, kijinsia na vinginevyo. Mtoto ana haki pia kutolazimishwa kufanya kazi za kiutumwa, nzito na za kushurutishwa. Hali kadhalika, ana haki ya kuishi katika nyumba au makazi bora na salama, kutunzwa na kulindwa dhidi ya hali yoyote inayoweza kumtayarisha. Anatakiwa ashirikishwe katika kufanya maamuzi. Fauka ya haya, ana haki ya kupata huduma za afya, mahitaji maalum, michezo, upendo na habari. Isitoshe, anastahili kuheshimiwa kimawazo na

kihisia.  Haki hizi zinatakiwa kulindwa na kila mwanajamii, hivyo serikali za mataifa mengi zimeshirikisha haki hizi katika katiba za nchi zao na sheria zao.

Walakini haki hizi bado zinakiukwa. Watoto wengi kote duniani bado wananyimwa haki zao.  La kusikitisha na kukera ni kwa wanaotarajiwa kuwa vigogo vya kuzilikda haki hizi, ndio wanaoongoza kuzikiuka.  Kila silku tunasikia na kushuhudia visa vya watoto kupigwa, kunyimwa chakula, kufanyishwa kazi kipunda, kuteswa, kuishi katika mazingira hatari, na hata kuuawa. Kuna watoto wengi wanaolala nje, wengine hawapati chakula licha ya kuwa wanatakiwa kupata chenye lishe bora.  Kwao kutarajiwa mlo awamu tatu kwa siku ni Njozi kwani hata awamu moja ni adimu kupata.

Watoto wengi katika mataifa yenye fujo na ghasia hutekwa na kutumikishwa vitani. Viongozi katika mataifa haya hawafanyi kitu ila kutazama tu wakati watoto wanaotakiwa kuwalinda wanageuzazwa kuwa mibaba ya kuua na kuuana.  Watoto hawa huvishwa magwanda ambayo miili yao minyonge haiwezi kuyahimili.  Pia, huvalishwa mabuti ya kijeshi ambayoo ni mizigo mizito ya kubeba mbali na bunduki zinazokaribia kuwazidi uzani wakati wanatakiwa kuwa wamelindwa majumbani, na shuleni na wazazi wao na serikali.

Jukwaa la vijiji vya mataifa ya ulimwengu wa tatu limesheheni watoto watioenda shule kwa sabani ya lindi la ufukara uliokidhiri.  Elimu ya bure inayogusiwa katika haki za watoto haipo.  Wanaong’ang’ana iwepo ni kana kwamba ni waota ndoto mchana.  Jiulize watoto wangapi sasa hivi wamo majumbani bila kwenda shuleni kutokana na ukosefu wa karo?  Wangapi wamo mitaani wakivuta na kunusa gundi huku wakiombaomba vishilingi?

Hali ilivyo sasa hivi inadai kuwa mimi na wewe tufanye hima kuungana mikono kutafuta suluhisho la kudumu kuhusu haki za watoto.  Twapasa kuhimiza serikali zetu kufanya kila ziwezavyo kuhakikisha kuwa watoto wote wamo shuleni. Nasi tushirikiane kutoa huduma kwa watoto na kukomesha dhuluma, mateso na dhiki kwao.  Haitoshi kupeleka miswada mbungeni kuhusu haki za watoto na kuipitisha kuwa sheria.  Twastahili kubadilisha misimamo yetu kuhusu haki hizi na kuzilinda kwa dhati bali si kwa chati.

**Maswali**

a) Fupisha aya mbili za kwanza (maneno 65 – 70) (alama 8 mtiririko 2)

b) Eleza ni vipi ukiukaji wa haki za watoto unaweza kuepukwa. (maneno 30 – 35) (alama 4, utiririko 1)

**3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

**a)** (i) Sauti ni nini? (alama 1)

(ii) Sauti gani ina sifa ifuatayo? (alama 1)

***Mbele, juu, tandazwa***

**b)** Andika neno moja lenye silabi za muundo ufuatao. (alama 2)

***Irabu, konsonanti + konsonanti, irabu konsonanti, irabu***

**c)** Unda vitenzi kutokana na nomino zifuatazo. (alama 2)

**i.** Hasidi –

**ii.** Karimu –

**d)** Tumia mzizi –ny- kukamilisha sentensi hii. (alama 1)

***Miti ya msitu huo ime______ mvua katika jimbo hili.***

**e)** Ainisha vielezi katika sentensi hii. (alama 2)

Msichana Yule aliongea kistadi kisha akaondoka kwa madaha.

**f)** Tambua na ueleze aina za vitenzi katika sentensi. (alama 3)

***Mwalimu angali mgonjwa hata kama amekuwa akifunza darasani.***

**g)** Tunga sentensi kwa kutumia kihisishi cha kutakia heri.

**h)** Kanusha sentensi ifuatayo katika hali ya wingi. (alama 2)

***Mimi nikikosa nitakuja***

**i)** Akifisha sentensi ifuatayo. (alama 2)

***Lo mwalimu alimchapa vibaya hivyo waziri aliuliza***

**j)** i)Onyesha kijalizo katika sentensi ifuatayo. (alama 1)

***Wambua ni mwanafunzi***

(ii) Onyesha (CH) chagizo katika sentensi ifuatayo. (alama 1)

***Tulitoka asubuhi na mapema***

**k)** Tumia neno 'fika' kutunga sentensi katika hali ya kinyume. (alama 2)

**l)** Andika sentensi ukitumia kauli iliyoko mabanoni, (alama 2)

i. Hukumu (tendewa) –

ii. La (tendeka) –

**m)** Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mstari. (alama 3)

***Huyu na Yule walicheza mpira mbele ya nyumba.***

**n)** Andika katika usemi halisi. (alama 3)

***Sista alisema kuwa angemwarifu endapo angemwona.***

**o)** Bainisha kiima na yambwa katika sentensi ifuatayo. (alama 3)

***Mama alimpikia mgeni wetu nyama ya kuku.***

**p)** Andika sentensi ifuatayo katika hali kanushi

***Viwavi wengi walikuwa wanavamia maneno.*** (alama 2)

**q)** Bainisha virai katika sentensi ifuatayo (alama 3)

***Pikipiki iliyonunuliwa jana iliharibika karibu na mto.***

**r)** Taja methali inayoafiki maelezo yafuatayo. (alama 2)

***Mtu anayetegemewa katika jamii akiondoka wanaomtegemea huwa mashakani.***

**4. Isimu jamii (alama 10)**

a) Eleza maana ya; (alama 2)

i. Lugha rasmi

ii. Lugha ya taifa

b) Eleza majukumu manne ya lugha ya taifa. (alama 8)

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: ……………………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ………………DARASA: …...........**

# STAREHE GIRLS' CENTRE MOCK EXAMINATION

**102/2**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA PILI**

**Maagizo**

- ***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
- ***b)*** *Jibu maswali yote.*
- ***c)*** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*
- ***d)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. UFAHAMU | 15 | |
| 2. UFUPISHO | 15 | |
| 3. SARUFI | 40 | |
| 4. ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**SEHEMU A: UFAHAMU**

**Soma kifungu kufuatacho kisha ujibu maswali**

Watu wengine hawawezi kunywa chai au uji bila kutia sukari.Wanatumia sukari kwa hamu na ghamu bila kutambua kuwa hiyo ni sumu wanayojiongezea mwilini.

Ni ukweli usiopingika kuwa wazee wa jadi waliishi muda mrefu wakiwa na siha njema kuliko sisi. Hii ni kwa kuwa waliishi katika kipindi ambacho sukari inayotengenezwa viwandani haikuweko. Iwapo ilikuweko, ilikuwa bidhaa ya wateule wangwana kutengnezea vitu kama keki, mahamri, vitumbua na kadhalika na akina yahe hawangeweza kuigharamia.

Watafiti wa masuala ya afya wamegundua kuwa sukari inayotayarishwa viwandani sasa haina virutubishi vyovyote. Hali kadhalika, utaratibu wa viwandani wa kutayarisha sukari ili iwe nyeupe na kuichuja,huharibu virutubishi vinavyoweza kuwa muhimu mwilini. Umuhimu wa sukari ni kutia ladha tamu tu.Umuhimu huu hauwezi kulinganishwa na madhara yanayoletwa na sukari hii. Baada ya kusagika mwilini, sukari hii huacha masalio ya asidi mwilini yenye sumu inayoathiri siha.

Matumizi ya sukari kwa wingi husababisha madhara mbalimbali mwilini. Kwanza, huchangia kuoza na kuharibika kwa meno pamoja na matatizo ya meno kuuma. Pili, sukari nyeupe imehusishwa na ongezeko la maradhi ya sukari, moyo na hipoglisimia au upungufu wa sukari mwilini. Matumizi holela ya sukari huleta kipanda uso au ugonjwa wa ghafla wa kuumwa upande mmoja wa kichwa unaoambatana na kichefuchefu, kutapika na matatizo ya kuona. Pia, sukari huleta maradhi ya ngozi na figo, pamoja na ongezeko la kemikali iitwayo kolestroli, ambayo ni ufuta unaonata na ambao unatokana na kutoyeyuka kwa mafuta yote mwilini. Kemikali hii ya kolestroli inaporundikana moyoni, hufanya mishipa inayotoa damu moyoni na kuisambaza mwilini kuwa myembamba na sugu. Moyo hulazimika kusukuma damu kwa nguvu na huenda moyo ukachoka na kukoma kufanya kazi.

Madhara haya ya sukari ndiyo yanayowafanya watu wengi kukiri kuwa sukari, ingawa ni tamu, ni sumu mwilini. Wataalamu wa lishe wamependekeza ulaji wa vyakula kama nafaka, matunda, mboga na miwa ambavyo vimejaa sukari asilia.

Fauka ya hayo, sukari inayotoka katika asali ni bora zaidi kwa mwili wa mwananadamu. Asali huwa na sukari asilia, vitamini, madini na amino asidi. Hivi vyote huwa na manufaa mbalimbali mwilini. Mathalani asali huupa mwili nishati inayohitajika kuendesha shughuli za viungo. Licha ya hayo, asali huuchangamsha mwili.Asali huwa na kemikali ambazo husaidia watoto kukua vizuri. Huweza kuzidisha kiwango cha himoglobini, hivyo kupunguza uwezekano wa chakula iwapo itatumiwa kabla ya mlo. Matumizi ya kijiko kimoja cha asali kila siku husaidia mwili kujikinga dhidi ya magonjwa ya kukohoa. Asali husaidia pia kuondoa harufu mbaya kinywani.

Asali pia inaweza kutumiwa kujipaka. Inapotumiwa kwa njia hii, hutunza ngozi na kuifanya ing'are, huondoa vipele na ugumu wa ngozi, pamoja na kutibu kule ngozi ilikokatikakatika. Hali kadhalika, asali hutibu vidonda.Viwanda vingi vya vipodozi vile vile hutumia asali kama malighafi muhimu katika utengenezaji wa bidhaa hizo.

**Maswali**

a) "Wazee wa jadi waliishi muda mrefu wakiwa na siha njema kuliko sisi." Fafanua kauli hii kwa kurejelea taarifa. (alama 2)

b) Watafiti wa masuala ya afya wamegundua nini kuhusu sukari inayotayarishwa viwandani? (alama 1)

c) Taja matumizi **mawili** ya sukari nyeupe. (alama 2)

d) Fafanua madhara **manne** ya sukari nyeupe mwilini? (alama 4)

e) Wataalamu wa lishe bora wanapendekeza aina ipi ya sukari itumike? (alama 1)

f) Eleza manufaa ya asali ndani na nje ya mwili. (alama 5)

**<u>SEHEMU B: UFUPISHO</u>**

Tunapinga na kulaani vikali visa vya ugaidi vinavyoendelea kutetemesha usalama wa wananchi.Hivi ni vitendo vya kinyama vinavovyotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu na utu kabisa.Inakera mno kwa vitendo vya kigaidi .Inagadhabisha kuona Wakenya wasio na makosa wakiteswa na kuuwawa kinyama bila huruma na watu wasio na utu. Hatuogopi wala hatuna fedheha kuamba magaidi hawa wameelaaniwa na siku zao zimehesabiwa hapa duniani, damu ya mwananchi asiye na makosa katu watailipia. Napinga vikali pale magaidi hawa wanapohusisha vitendo hivi kuwa vita vya kidini, vita hivi si vya kidini kwani hakuna dini yoyote iliyo na imani ya kumwua kinyama binadamu asiye na makosa.

Kando na tishio la ugaidi, Wakenya pia wanakabiliwa na hatari za ujambazi, mauaji, unajisi, ubakaji na maovu mengine. Katika juhudi za kudumisha usalama, polisi wana jukumu la kutumia kila mbinu kuhakikisha kuwa haki ya kikatiba ya Wakenya kuhusu kulindwa kwa maisha na mali yao. Lakini cha kusikitisha ni kuwa, mbinu ambazo polisi wamekuwa wakitumia hasa ile ya kufanya misako inayoishia kuwanasa mamia ya raia wasio na habari kinachoendelea, inawaongezea Wakenya mateso. Hali hii inawaacha kwenye hatari ya kunaswa na majambazi ama polisi.

Matumizi ya mbinu hii ya misako imeishia kunasa raia wengi wasio na makosa.Wanaponaswa, hurundikwa kwenye seli usiku mzima ama siku kadha na hata kama wanaaachiliwa huwa tayari wameteseka. Huu ni ukiukaji wa haki za raia. Kadhalika, mbinu hii yanaonekana kama hila ya polisi kutaka kuonyesha wanafanya kazi lakini sio mwafaka kwani wanapokuwa wakiwanasa raia mijini na mitaani, magaidi na majambazi wanaendelea na shughuli zao.

Badala ya kusaka wakora kwa kubahatisha kwenye umati, polisi wanapaswa kubuni njia ambazo zitawapa mwelekeo mwafaka zaidi kuhusu wahalifu ili waweze kuwafuatilia. Ushirikiano baina yao na majasusi uwepo. Hii itawezesha polisi kupata habari muhimu kuhusu vitisho vya uhalifu. Maafisa wa usalama pia wanaweza kupata habari muhimu kutoka kwa raia.

**Maswali**

i) Ni nini maoni wa mwandishi kuhusu suala la ugaidi. (maneno 60-70) (alama 7, 1 utiririko)

ii) Kwa kutumia maneno yasiyozidi 50 fupisha aya mbili za mwisho. (alama 6, 1 utiririko)

## 3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) **Tambulisha ngeli za nomino zifuatazo:** **(alama. 2)**

(i) Upana ……………………………………………………………………...

(ii) Pesa ……………………………………………………………………..

b) **Kanusha:** **(alama. 1)**

Niliondoka pamoja naye, nikaenda mjini na nikamuaga.

c) **Tunga sentensi kwa kutumia kivumishi kiashiria kisisitizi katika ngeli nomino ya I-I.** **(alama.2)**

d) **Tumia kirejeshi 'o' cha tamati badala ya 'amba' katika sentensi ifuatayo: (alama. 1)**

Jengo ambalo ni dhaifu huanguka.

e) **Bainisha aina za vishazi katika sentensi hii:** **(alama. 2)**

Wote walipita mtihani ulipofanywa.

f) **Andika kwa udogo na wastani katika hali ya wingi.** **(alama. 2)**
Gombe lilichinjwa jana kwa jisu kali.

g) **Eleza matumizi ya 'kwa' katika sentensi ifuatayo:** **(alama. 2)**
Alipigiwa kwake kwa kuwazuia wezi walionipiga kwa panga kwa ukatili mkubwa.

h) **Andika kinyume cha:** **(alama. 2)**
Vigoli watatu wameingia kwa shaibu kwa kasi.

i) **Pambanua sentesi ifuatayo kwa njia ya jedwali:** **(alama. 4)**
Vijana werevu wanasoma ilhali wahuni wanacheza mafichoni mle.

j) **Andika visawe vya:** **(alama. 1)**

(i) bendera______________________________________________

(ii) jicho______________________________________________

k) **Vitamkwa vifuatavyo ni vya aina gani?** **(alama. 1)**

(i) /ng/______________________________________________

(ii) /r/______________________________________________

l) **Tambua yambwa katika sentensi ifuatayo.** **(alama. 2)**
Mjomba alimnunulia zawadi mpwa wake.

m) **Tunga sentensi ukitumia alama za uakifishaji zifuatazo.** **(alama. 2)**

(i) Parandesi______________________________________________

(ii) Kibainishi______________________________________________

n) **Eleza matumizi ya 'po' katika sentensi zifuatazo:** **(alama. 3)**

(i) Atembeapo, Jane huimba______________________________

(ii) Atembeapo Jane pana miiba______________________________

(iii) Anapotembea Jane huimba______________________________

o) **Bainisha mofimu katika maneno haya na utaje ni ya aina gani.** **(alama. 2)**

(i) Uzuri______________________________________________

(ii) Sana______________________________________________

p) **Bainisha virai katika sentensi ifutayo:** **(alama. 2)**
Mtu mwenye lile duka kubwa aliaga dunia jana usiku.

q) **Geuza maneno yaliyopigiwa mstari yawe katika hali uliyopewa mabanoni.** **(alama. 1)**

(i) Alimtia <u>hasira</u> aliposema hivyo. (kitenzi)
(ii) Likono anapenda <u>kucheka.</u> (kivumishi).

r) **Eleza tofauti kimaana katika sentensi zifuatazo:** **(alama. 2)**

(i) Angekuwa na mdahilishi angenitumia ujumbe
(ii) Angolikuwa na mdahilishi angalinitumia ujumbe.

s) **Tofautisha:** **(alama. 2)**

(i) mahali kote kunafaa.
(ii) mahali kokote kunafaa.

t) **Tunga sentensi kwa kutumia mizizi ya vitenzi ulivyopewa katika kauli zilizomo mabanoni.** **(alama. 2)**

(i) –fa (tendea)

(ii) –pa (tendeka)

u) **Akifisha:** **(alama. 2)**

tutakapofika kwenye manyatta nitawapa maziwa ya mursik mama aliwaambia wanawe.

4. ISIMU JAMII **(alama. 10)**

**Eleza maana ya istilahi zifuatazo**

1. Sajili (alama 2)

2. Isimu jamii (alama 2)

3. Lugha ( alama 2 )

4. Isimu (alama 2)

5. Lugha rasmi (alama 2)

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(Kcse)*

**MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025**

**JINA: ……………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ……DARASA: …............**

# SHULE YA UPILI YA MARANDA

**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**
MAAGIZO
**Maagizo**

- ***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
- ***b)*** *Jibu maswali yote.*
- ***c)*** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*
- ***d)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. UFAHAMU | 15 | |
| 2. UFUPISHO | 15 | |
| 3. SARUFI | 40 | |
| 4. ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**1. UFAHAMU**

***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata***

Uchumi ni mfumo wa mapato na matumizi ya watu katika nchi fulani.Uchumi huu huhusisha sekta mbalimbali kama vile utalii,kilimo,sanaa,miongoni mwa sekta nyingine muhimu.Ukuaji wa kiuchumi hutegemea mambo kadha.Katika nchi zote ulimwenguni, sera za kisiasa huamua jinsi uchumi utakavyokua na kunawiri.Kama siasa hazitilii maanani sera za ukuaji wa kiuchumi, basi mapato ya nchi hiyo hugubikwa katika wingu kubwa la uchochole.

Nchini Kenya, kwa mfano, kuna ulinganifu mkubwa kati ya siasa na ukuaji wa kiuchumi.Ukuaji wa kiuchumi hutegemea uteuzi wa maafisa wanaosimamia asasi muhimu sana katika usimamizi wa uchumi.Asasi hizi ni kama vile Wizara ya Fedha, Wizara ya Mipango ya Kitaifa na Ruwaza ya 2030, Mamlaka ya Ukusanyanji wa Ushuru(KRA), Benki Kuu ya Kenya (CBK), na Tume ya Kupambana na Ufisadi (KACC).Usimamizi wa asasi hizi huwa muhimu sana katika kuamua hatima ya uchumi wananchi hii.

Katika mwezi wa Juni kila mwaka, Waziri wa Fedha husoma bajeti kwa wabunge.Katika maelezo yake iitwayo nakisi ya bajeti hujitokeza.Kabla ya bajeti kuandaliwa, Wizara ya Mipango huandaa hati iitwayo Usoroveya wa Kiuchumi.Baada ya kusomwa kwa bajeti, ni jukumu  la wabunge kupitisha mswada wa kifedha unaohusisha wizara zote au kuutupilia mbali.Jukumu hili linafaa kutekelezwa kufikia tarehe 31 Oktoba ya kila mwaka kulingana na sheria.

Wakati huo huo afisa anayejulikana kama Mhasibu Mkuu wa serikali huwa na jukumu la kuchunguza na kutathmini matumizi ya fedha ya wizara mbalimbali na kutoa ripoti yake kwa Kamati ya Uhasibu wa Umma bungeni (PAC).Kamati hii hutoa mapendekezo yake kwa Mkuu wa Sheria na pia kwa tume ya kupambana na ufisadi ili haki iweze kutekelezwa mahakamani iwapo dosari za kifedha zimefanyika.

Benki kuu ya Kenya kupitia kwa gavana wake huwa na jukumu la kutoa ushauri kwa serikali kuhusu usimamizi wa kifedha, kuchunguza nguvu za shilingi ya Kenya dhidi ya sarafu za kigeni, kutoa sarafu za Kenya kwa umma na usimamizi wa benki zote nchini miongoni mwa majukumu mengine.

Kwa upande mwingine, mamlaka ya ukusanyaji ushuru nchini huwa na jukumu la kuhakikisha kuwa malengo ya ushuru yamefikiwa na pia kuhakikisha kuwa hakuna mtu binafsi au kampuni yoyote inayokwepa kulipa ushuru.Iwapo kuna udanganyifu wowote, basi swala hili linafaa kuangaliwa na mahakama zetu kutekelezwa.

Kwa jumla, sisi kama wananchi tunafaa kusaidia asasi hizi zote kufikia malengo yake ili tupate ukuaji wa kiuchumi utakaofaidi watu wote.Jambo hili litahakikisha kuwa pengo lililo kati ya walalahai na walalahoi walalahoi limezibwa.Sisi kama wananchi, tunafaa kuonyesha uzalendo wetu kwa nchi yetu kwa kulipa ushuru unavyotakikana, tukifuata mwito wa KULIPA USHURU NI KUJITEGEMEA.Mwisho tusaidie viongozi wetu katika kuendeleza sera mwafaka za kiuchumi ili nchi yetu ipige hatua kubwa katika ukuaji wa kiuchumi.Iwapo

afisa yeyote atatuhumiwa kushiriki katika kashfa yoyote ya kuhujumu nidhamu ya kifedha, basi anafaa kukabiliwa vilivyo kisheria bila kujali hadhi yake ya kijamii au kisiasa.

***MASWALI***

(a) Ipe habari hii kichwa mwafaka. (alama 1)

(b) Uchumi ni nini? (alama 1)

(c) Ukuaji wa kiuchumi nchini Kenya hutegemea nini? (alama 1)

(d) Benki Kuu ya Kenya ina majukumu yepi? (alama 2)

(e) Mhasibu mkuu ana dhima ipi serikalini? (alama 1)

(f) Pendekeza hatua tatu za kufufua uchumi. (alama 3)

(g) Ufisadi umehujumu vipi ukuaji wa kiuchumi? (alama 2)

(h) Ni vipi Wakenya wanaweza kuonyesha uzalendo? (alama 1)

(i) Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumiwa katika taarifa: (alama 3)

(i) Hatima . …………...............................................................................................

(ii) Walalahai……………………………………………………………………….

(iii) Walalahoi………………………………………………………………………

## 2. UFUPISHO

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Visa vya dhuluma za kinyumbani vimeongezeka hivi majuzi, huku wanawake wakiangaziwa zaidi kwa kuwapiga waume zao.Kwa muda mrefu, visa ambavyo vimekuwa vikishuhudiwa ni vya wanaume dhidi ya wake zao.Ni wazi kwamba wanaume kwa mara nyingi wanaopitia matatizo huogopa kuyatangaza hadharani.

Hali ya kiuchumi imeathiri pakubwa familia nyingi.Pesa za kugharamia mahitaji muhimu kama chakula, mavazi na makazi zimekuwa adimu.Jambo hili linasababisha mivutano baina ya mume na mke inayoishia vita na wahusika kujeruhiwa.Wengine wameyapoteza maisha yao na wengine kulemaa kwa mili yao daima dawamu.

Wake kwa waume wameyapuuza majukumu yao katika ndoa.Kuna waume ambao wanatumia mapato yao na ya familia kwa kupiga maji.Waume kama hawa hujigamba kuwa wao ni wakwasi na huwanunulia wenzao mvinyo huku familia zao zikiteseka kwa umaskini.Waume na wake walevi huwatukana wenzao na kwa hivyo migogoro katika ndoa kama hizi huwa haikomi.

Wanandoa wengine wanajihusisha na mapenzi nje ya ndoa licha ya kula kiapo cha uaminifu wakioana.Usaliti huu hufanya watu wengine kulipiza kisasi kwa kuwapiga wenzao au kutomakinika katika ndoa.Matatizo ya

kisaikolojia yamewafanya watu kushindwa kuzithibiti hisia zao.Kutoelewana kunapozuka, wao hupandwa na hamaki na huenda wakakawatesa wake na waume zao.

Ukosefu wa nasaha kwa wanandoa wengi umeleta shida nyingi.Wengi hawaelewi namna ya kutatua matatizo ya nyumbani.Kuna njia tofauti za kuepuka dhuluma nyumbani.Wanandoa wanafaa kudumisha upendo wa dhati kila wakati.Wake kwa waume sharti watekeleze majukumu yao nyumbani bila kuyaepuka.Mapenzi nje ya ndoa lazima yatupiliwe mbali ili muamana unaofaa uwepo.

Licha ya changamoto tofauti katika ndoa, wanaohusika wanafaa wavumilie na kujaribu kuzika tofauti zao katika kaburi la sahau.Hawafai kuweka rekodi ya makosa ambayo wametendeana.Wosia unafaa kutolewa kwa wake na waume wote ili waelewe mikakati ya kukabiliana na matatizo mbalimbali yanayokumba ndoa.

Viongozi wa kidini wafundishe watu maadili ili watu waepuke tamaa za kimwili zinazowasonga na kujihusisha na mapenzi nje ya ndoa.

Ndoa inafaa iheshimiwe na watu wote kwani ndio msingi wa taasisi zile zingine kama jamii na nchi.Mawasiliano yanafaa yaimarishwe katika ndoa.Kukiwa na mazungumzo, matatizo mengi yatajadiliwa na kusuluhishwa ili kuepukana na dhuluma za aina zozote.

***MASWALI***

(a) Eleza kiini cha dhuluma za kinyumbani.(maneno 40-50).(alama 6;alama 1 ya mtiririko)

(b) Fupisha aya nne za mwisho ukizingatia ujumbe muhimu.(Maneno 60 – 70) (alama 9;alama 1

**MATUMIZI YA LUGHA**

(a) Andika vitamkwa vyenye sifa zifuatazo. (alama 2)

(i) Kipasuo ghuna cha ufizi

(ii) Kikwamizo sighuna cha menoni

(b) Ainisha mofimu katika neno hili; (alama 3)

Wanawalisha

(c) Tambua na ueleze aina za vitenzi katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Kalamu aliyokuwa nayo mwalimu ni ya mwanafunzi.

(d) Andika sentensi ifuatayo katika wingi (alama 1)

***Ua wake una ua zuri na kubwa.***

(e) Tunga sentensi ukitumia vivumishi vya pekee kudhihirisha maana ya: (alama 2)

(i) Kutobagua

(ii) Kumiliki

(f) Andika katika hali ya udogo (alama 2)

Mbwa mwenye ukali alimfukuza mtoto.

(g) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa

" Tutaondoka mwezi ujao kuelekea ughaibuni," wambunge walisema. (alama 3)

(h) Eleza matumizi ya 'po' katika sentensi zifuatazo: (alama 3)

(i) Anapotembea, Mumo huimba.

(ii) Atembeapo, Mumo huimba.

(iii) Atembeapo Mumo, pana miiba.

(i) Yakinisha sentensi ifuatayo; (alama 1)

Usipobisha hutafunguliwa wala kukaribishwa.

(j) Andika nomino mbili zinazoweza kuwekwa katika ngeli mbili tofauti na ubainishe ngeli hizo: (alama 2)

(k) Andika kinyume cha; (alama 2)

Watoto wameombwa waanike nguo.

(l) Badilisha sentensi zifuatato ziwe katika kauli ulizopewa mabanoni. (alama 2)

(i) Mshtakiwa atatoa faini ya shilingi elfu moja.(Kutendwa)

(ii) Ugonjwa wa saratani huwafanya watu wengi wafe.(Kutendesha)

(m) Bainisha yambwa na chagizo; (alama 3)

Mkulima alivuniwa mahindi mwezi uliopita.

(n) Tumia neno "vizuri" katika sentensi kama: (alama 2)

(i) Kielezi

(ii) Kivumishi

(o) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia jedwali.

Japo alifanya kazi zote, hakulipwa mapema. (alama 3)

(p) Eleza matumizi ya ritifaa katika:N'shamchukua. (alama 2)

(q) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo; (alama 2)

Usalama ukiimarishwa watalii wengi watakuwa wanazuru humu.

(r) Onyesha muundo wa silabi katika neno lifuatalo. (alama 1)

Mdau

(s) Tunga sentensi moja kudhihirisha tofauti kimaana kati ya vitate vifuatavyo.(alama 2)

(i) guna

(ii) kuna

**4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

(a) Eleza sababu zinazowafanya watumizi wa lugha fulani kufanya makosa katika mazungumzo. (alama 5)

(b) Eleza sifa TANO za matumizi ya lugha katika muktadha wa maabadini. (alama 5)

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(Kcse)*

**MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025**


**JINA: ……………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ……DARASA: …............**

# SHULE YA UPILI YA MASENO

**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**
**MAAGIZO**
**Maagizo**

***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

***b)*** *Jibu maswali yote.*

***c)*** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*

***d)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. UFAHAMU | 15 | |
| 2. UFUPISHO | 15 | |
| 3. SARUFI | 40 | |
| 4. ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |


**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**Ufahamu (Alama 15)**

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata***

Wahenga walisema kutoa ni moyo usambe ni utajiri. Iwapo wangefufuka leo hii wangeongezea kuwa ujasiri ni moyo usiseme ni umri. Kauli hii kama ile ya kwanza imesheheni ujumbe muhimu. Katika jamii nyingi, mtoto haruhusiwi kukaa au kuzungumza mbele ya watu wazima. Akiwa wa kike ndiyo basi. Ni ajabu basi kwa mtoto wa kike kutoka jamii yenye imani kali za jadi zinazomdunisha mwanamke kuweza kupata tuzo yenye staha ya juu zaidi.

Malala Yousafzai alishinda Tuzo ya Nobel mwaka 2014 akiwa na umri wa miaka 17. Aliyeshinda naye tuzo hii adhimu ni Kailash Satyarthi. Kigoli huyu alituzwa tunu hii kwa kupigania haki za wasichana kupata Elimu nchini Pakistan. Harakati hizi hakuzianza juzi. Mwaka 2012 alipigwa risasi na mijibaba ya ugaidi ya kundi Fulani linaloegemea mrengo wa siasa kali kwa 'hatia' za kuwatetea mabanati. Inasemekana alishambuliwa alipokuwa akisafiri kwenye basi la shule. Kilichochochea mashambulizi ni tuhuma kuwa alikuwa ameanzisha jukwaa kwenye mtandao wa Shirika la Utangazaji la BBC alilokuwa akichangia maandishi alipokuwa na umri wa miaka 11. Maandishi yake yalikuwa na ujumbe wa kupinga juhudi za makundi Fulani kuwanyima wanawake Elimu.

Haikuwezekana hata baada ya kupona kurudi Pakistani. Alihamia Uingereza alipofadhiliwa na wahisani. Licha ya kuwa aliishi ugenini na bila aila yake mwana huyu hakupoteza makali ya ari yake ya kuendelea kutetea maslahi ya kielimu ya wenzake wa kike.

Yeye ndiye mwenye umri wa chini zaidi katika historia kupata tuzo hili. Baadhi ya wale walioshinda Nobel katika umri mkubwa ni Desmond Tutu, Nelson Mandela na Wangari Maathai. Kila mmoja wao alitambuliwa kwa sababu mahususi zinazohusu jitihada za kuboresha maisha ya wanajamii.

Njia nyingine kuu aliyoitumai Malala ni hotuba. Mwaka 2013 alihutubia Kongamano la Vijana la Umoja wa Mataifa katika hafla iliyoandaliwa kwa heshima yake. Aliwashangaza wengi kwa ufasaha na uweza wake wa kutongoa hoja. Kila mtu aliguswa na dhati ya kauli zake. Katibu Mkuu hakuwa na jingine ila kulipa kongamano hilo jina Malala. Mtoto huyu wa kimaskini alipewa taathima ambayo watu wachache sana wamepata kutunukiwa. Hii ni heshima inayotengewa marais na wafalme. Na wanapoipata huruhusiwa kuhutubia kwa dakika tano tu.

Mwaka 2014, viongozi wenye sifa za ubabe wa kuwabinya wapinzani wao lakini wameshindwa kuwaokoa wanyonge walipokuwa wakilaza damu, yeye alisafiri hadi Naijeria kudai kuachiliwa kwa wasichana 200 waliotekwa nyara na kundi haramu.

Katika hotuba iliyojaa hisia ambazo huhusishwa tu na akina mama wenye uzazi mkubwa aliyoitoa Naijeria , aliwaasa watoto wenzake wasimruhusu mtu yeyote awaambie kuwa wao ni wanyonge au hawana

uwezo. Aliwanasihi kuwa wao sio wadhaifu kuliko wavulana na wasijione wanyonge kuliko watoto wa kitajiri wala wale wanaotoka nchi zenye uwezo mkubwa . Alihitimiza kuwa wao ndio watakaoijenga jamii na kuwa wana uwezo wa kuyaendesha mambo.

Mshindi wa tuzo hii yenye thamani ya dola za kimarekani milioni moja ameitabaruku kwa watoto wenzake ulimwenguni. Bila shaka mwanzilishi wa tuzo ya Nobel ameguswa na tendo la mtoto huyu huko kuzimuni. Kama kumbukizi tunu hii hutolewa wakati wa kuadhimisha kifo cha Mwanaviwanda wa

Kiswidi aliyeasisi tuzo hii kufuatana na wosia wake mwaka 1895. Kama Alfred Noble mwenyewe, kwake Malala, ngwenje au darahimu si muhimu . Lililo muhimu ni ukombozi wa watoto na

hasa wa kike kielimu. Malala bado anavaa mtandio wake huku akidhihirisha adabu na unyenyekevu wa kupigiwa mfano.

**Maswali**

1. Eleza mtazamo wa jamii ya Malala kuhusu watoto wa kike. (alam.2)
2. Unafikiri Malala alistahili kutuzwa Tuzo ya Nobel? Toa sababu tatu. (alama.3)
3. Ni njia zipi alizozitumia Malala kutetea haki ya watoto wa kike kupata Elimu? (alama 3)
4. Malala anawapa ushauri upi watoto wenzake? (alama. 1)
5. Kwa nini inasemekana kuwa Tuzo ya Nobel ina staha ya juu zaidi? (alama.2)
6. Andika kichwa kifaacho kwa kifungu hiki. (alama.2)
7. Eleza maana za maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa: (alama. 3)
   a) Tunu
   b) Wahisani
   c) Ubabe

1. **UFUPISHO**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Ukame ni tukio hatari la kimaumbile. Athari zake hutofautiana kutoka eneo moja hadi lingine. Kwa sababu hiyo, si rahisi kuielewa dhana ya ukame; kwa hakika si rasihi kuifafanua dhana hii. Katika eneo la Bali, kwa mfano, isiponyesha kwa muda wa siku sita wenyeji huchukulia hali hiyo kuwa ukame japo kiasi hicho cha mvua ni kikubwa mno ikilinganishwa na Libya ambayo hupata kiasi kidogo cha chini ya milimita 180 ya mvua kwa mwaka.

Katika hali ya kawaida ukame hutokana na kipindi kirefu cha uhaba wa mvua hasa katika mzima au zaidi. Uhaba huu wa mvua huweza kusababisha uhaba wa maji kwa shughuli, kundi au sekta Fulani. Shughuli

za binadamu huweza kufanya hali ya ukame mbaya zaidi.Shughuli hizo ni pamoja na kilimo, unyunyiziaji maji na ukataji wa miti.

Ni vigumu kubaini wakati mahususi ambao ukame huanza kwa kipindi hicho cha ukosefu wa mvua huwa cha mfululizo, na eneo huendelea kupata mvua iliyopungua kwa miezi au hata miaka. Mimea hukauka na wanyama hufa kutokana na ukosefu wa maji. Ukame basi huwa hatari kwa maisha ya binadamu na viumbe wengine kwa kuwa huweza kusababisha njaa na kuyafanya maeneo kuwa majangwa.

Mbali na ukosefu wa mvua, ukame pia husababishwa na kiangazi. Kiangazi huongeza kiwango cha joto. Joto hilo hufanya maji yaliyohifadhiwa kuwa mvuke haraka, hivyo kiwango chake kupungua. Hali ya *el ninyo* pia husababisha ukame katika baadhi ya maeneo ambayo huwa hayana mvua. Upepo huivutia mvua mahali panaponyesha na kuliacha kame eneo ambalo halina mvua ya aina hii. Hata katika maeneo yenye mvua ya *el ninyo* , kiangazi kikali huifuata na hivyo kusababisha ukame. Hali hii huitwa *la nina*. Mambo yanayotokana na mabadiliko ya hali ya anga ulimwenguni pia yanaweza kuchangia ya ukame. Ongezeko la joto duniani linafanya hali ya ukame kuwa mbaya zaidi.

Ukame una mdhara chungu nzima kwa binadamu. Madhara hayo huweza kuwa ya kiuchumi, kimazingira, kimazingira au hata kijamii. Ukame husababisha kupungua kwa mimea na mavuno. Huweza pia kutokea dhoruba za mchanga. Dhoruba hizi hutokea palipo na jangwa. Ukosefu wa maji ya kunyunyizia mimea husababisha njaa na magonjwa kama vile utapiamlo yanayotokana na ukosefu wa lishe bora. Makazi ya wanyama wanchi kavu na wale wa majini pia huathiriwa vibaya. Hali kadhalika, ukame husababisha uhamaji. Hii inamaanisha kuwa jamii huweza kutoka katika makazi asilia na wakati mwingine huweza hata kuwa wakimbizi.

Ukame husababisha ukosefu mkubwa wa maji. Ukosefu huu huwa na athari hasi kwa maendeleo ya viwanda kwa kuwa vingi huhitaji kiasi kikubwa cha maji. Juu ya hayo, maji huhitajika katika kuzalisha umeme. Umeme una matumizi mengi katika viwanda, nyumbani, afisini na hata hospitalini. Ukosefu wa umeme basi huwa ni tatizo kuu.

Aidha, ukame husababisha madhara mengi, binadamu wanaweza kujikinga kutokana na uhaba wa rasilimali za asili kama vile chakula na maji. Pia mioto mikubwa huweza kuenea haraka wakati wa ukame na hivyo kusababisha vifo vya binadamu na wanyama na uharibifu wa rasilimali nyingine.

Ingawa ukame husababisha madhara mengi, binadamu wanaweza kujikinga kutokana nao kwa kupunguza makali ya ukame. Jambo la kwanza wanaloweza kufanya binadamu ni kuhifadhi maji. Maji

ya mvua yanafaa kuhifadhiwa katika mabwawa na mapipa. Haya yanaweza kutumiwa wakati wa ukame hasa katika kukuza mimea. Mkakati mwingine ni kutumia mbinu za kupunguza chumvi na kemikali nyingine zilizomo kwenye maji ya bahari ili yaweze kutumika katika unyunyiziaji wa mimea. Hili litapunguza tatizo la ukosefu wa chakula. Pia ni muhimu kufanya utafiti kuhusu hali ya anga ili kupanga  na kuweka mikakati ifaayo kukabiliana na hali hiyo.

Ni muhimu kuwa na mipangilio mizuri ya matumizi ya ardhi. Mathalani upanzi wa mimea itakayozuia mmomonyoko  wa udogo, kubadili aina ya mimea inayokuzwa sehemu fulani pamoja na upanzi wa mimea isiohitaji mvua nyingi katika kame ni hatua mwafaka. Aidha, ni vizuri kupunguza matumizi ya maji hasa katika mazingira ya nyumbani kwa mfano tunapofua na kuosha. Njia nyingine ya kukabiliana na tatizo hili ni kusafisha maji yaliyotumiwa ili kuyatumia tena.

a) Kwa maneno **50**, eleza visababishi vya ukame kwa mujibu wa taarifa (alama 5)

b) Fupisha ujumbe wa aya ya **tano** hadi **saba** kwa maneno 70. (alama. 5)

**c)** Eleza masuala ambayo mwandishi ameibua katika aya mbili za mwisho kwa maneno **60**. (alama.5)

**2. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA    ALAMA 40**

a) Andika maneno yenye miundo ifuatayo . (alama.2

i) Kipasuo ghuna cha midomoni, irabu ya chini, kati, kipasuo sighuna cha ufizi, irabu ya juu mbele.

ii) Nazali ya ufizi, kipasuo ghuna cha kaakaa laini, irabu ya juu, nyuma, irabu ya nyuma wastani.

b) Bainisha silabi zinazowekwa shadda katika maneno yafuatayo (Alama. 1)

i) Waliotusifia

ii) Sherehekea

c) Andika sentensi ifuata katika wingi. (Alama.2)

Wayo wa mguu wangu wa kulia umeungua

d) Geuza sentensi ifuatayo katika hali ya udogo. (alama. 1)

Njia hii yetu inapitiwa na mtu mnene

e) Tunga sentensi moja yenye kivumishi cha pekee kinachoonyesha idadi jumla. (alama.1

f) Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maagizo

i) Maafisa hao walipewa uhamisho. Maafisa wengine hawakupewa uhamisho

(unganisha kuunda sentensi ambatano) (alama.2)

ii) Hadithi hiyo <u>ilitungwa</u> vizuri <u>ikawavutia</u> wengi

( badilisha vitenzi vilivyopigiwa mstari kuwa nomino) (alama.2)

iii) Tunda halitaoshwa vyema. Tunda halitalika .

(unganisha kuwa sentensi moja kwa kutumia ‘po’) (alama.2)

iv) Kengewa alitoa ahadi .Wengi waliiamini ahadi hiyo. (unganisha kuwa sentensi moja inayoanza kwa . Ahadi….) (alama .2)

g) Tunga sentensi ya masharti inayoonyesha kwamba kitendo kilifanikiwa kutokana na kufanikiwa kwa kingine. (alama. 2)

h) Tunga sentensi yenye kishazi kirejeshi ambacho ni kielezi. (alama.2)

i) Ainisha maneno ya liyopigwa mstari katika sentensi ifuatayo. (alama. 3)

<u>Mwenyewe hakuwa amekupa</u> ruhusa kuitumia

j) Akifisha sentensi ifuatayo.

Kiwango cha umasikini katika kaunti ya homabay kinasikitisha sana itabidi sote wakatizi wa hapa tujizatiti ili tutimize malengo ya millennia seneta mteule alituhimiza

k) Andika maneno yenye mofimu zifuatazo. (alama. 2)

i) Umoja (ngeli ya u-i), mzizi, kiisho

ii) Kikanushi, kiambishi ngeli (ki-vi, Umoja)
Mzizi, kauli tendeka, kiisho

l) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. (alama. 2)

KN (N+RH) + KT (T+RE)

m) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya kukanusha . (alama. 2)

Ngoma hizo zilihifadhiwa ili ziuzwe mjini.

n) Andika sentensi ifuatao katika wakati uliopita hali ya mazoea. (alama.2)

Ekapolon atawashauri wanafunzi kuhusu umuhimu wa kufanya bidii

o) Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendesha kwa kuzingatia maneno yaliyopigiwa mstari(Alama. 2)

Alimfanya mtoto <u>anywe</u> uji ukamfanya <u>ashibe.</u>

p) Tunga sentensi ukitumia mzizi, ingineo kumaanisha “mbali na”. (Alama. 1)

q) Hewala ni kwa kukubaliana na jambo, ……………………… .ni kwa kutoka kitu kinusurike, na…………….ni kwa aliyefanya vyema katika jambo. (alama.1)

r) Zito ni kwa jepesi, ……………………..ni kwa choyo na, ……………………ni kwa kali. (alama.2)

s) Andika visawe vya kauli zi zilizopigiwa mstari.

Atyang <u>alikumbwa</u> na matatizo mengi lakini <u>hakukata</u> tama.

3. **ISIMU JAMII**. (Alama.10)

Eleza sababu tano zinazowafunga watu kufanya makosa ya kisarufi katika mazungumzo.

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(Kcse)*

## MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: ……………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ……DARASA: …............**

# SHULE YA UPILI YA MANGU

**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**
**MAAGIZO**
**Maagizo**

- ***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
- ***b)*** *Jibu maswali yote.*
- ***c)*** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*
- ***d)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE**

| **SWALI** | **UPEO** | **ALAMA** |
|---|---|---|
| 1. UFAHAMU | 15 | |
| 2. UFUPISHO | 15 | |
| 3. SARUFI | 40 | |
| 4. ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**1. UFAHAMU (ALAMA 15)**

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuatia</u>*.**

Nchi yetu imeraukia mawio ya machafuzi ya kisiasa baada ya shughuli za uchaguzi zilizogonga mwamba mkuu. Hili lilijiri baada ya Tume ya uchaguzi kukosa kuendeleza uchaguzi kwa njia inayostahili. Jambo hili lilizaa msukosuko wa kisiasa usiomithilishwa katika historia ya taifa letu.

Hivi sasa wakenya wanaishi kwenye kambi za watu wasio na makazi. Hiki ni kinaya kikuu kwani matukio haya yamezuka baada ya miongo minne ya uhuru. Vilio vya wakenya vimeshamiri na kupaasa sauti vikalalamikia kukosa makazi, lishe na ndoa kusambaratika. Ndoa zimevunjika baada ya'wenyeji' kuwatimua 'wageni na damu kumwagika.

Kenya imekuwa miongoni mwa mataifa yanayowapa faraja wakimbzi kutoka nchi jirani zinazokumbua na vita vya wenyewe. Vita katika Somalia vimesababishwa na koo mbali zinazopigania uongozi hali ambayo imekwamisha shughuli zote za kiuchumi.

Hali ya sasa ya Kenya imechochewa na msururu wa sababu; ukabila na tama ya uongozi zilionekana wazi katika miundo ya vyma viku vya kisiasa na katika kampeni zao. Wakenya walipiga kura kwa misingi ya kikabila upande ukitazamia mtu wao kushinda uchaguzi huo.

Kwa upande mwingine , viongozi hao kutokana na tamaa ya uongozi walikuwa wamesmua kushinda uchaguzi huo kwa vyovyote vile. Leo tunavuna matunda ya siasa za ukabila na tamaa ya mamlaka.

Maelfu ya wakenya ni makimbizi nchini na katika nchi jirani ya Uganda. Wakenya hao wanahitaji msaada wa chakula na mahitaji mengine ya kimsingi. Serikali na shirika la msalaba mwekundu zimefanya juhudi kuwasaidia wahasiriwa lakini kuna tetesi kwamba ubaguzi umejipenyeza katika ugawaji wa msaada huo.

Waliopewa jukumu la kugawa msaada huo ni sharti waelewe kuwa waathiriwa ni wakenya wenzao na hawafai kubaguliwa kwa misingi ya makabila yao. Matukio kama hayastahili asilani katika taifa hili.

Twahitaji zao <u>aali</u> la viongozi wasiojitwika ubabe bali wawe watumishi wa wananchi wanastahili kutupilia mbali tamaa za kujilimbikiza mali na kung'ang'ania uongozi. Pia katiba inafaa irekebishwe. Wakenya wanastahili kuelimishwa kuhusu undugu na utaifa. Fauka ya haya masuala yanayohusiana na hatimiliki za ardhi yanafaa <u>kutandaraukiwa kwa dhati.</u>

a) Taja madhara manne ya ukabila. (al.4)

b) Shughuli za ugawaji wa misaada zimekumbwa na changamoto gani. (al.2)

c) Eleza tofauti ya chanzo cha vita nchini Somalia na Kenya. (al.2)

d) Mwandishi anatoa mapendekesho gani ya kutatua tatizo hili la ukabila. (al.3)

e) Eleza kinaya cha maisha ya wakenya kwa sasa. (al.2)

f) Eleza maana ya maneno haya yalivyotumika katika kifungu cha ufahamu. (al.2)

i. Mawio.

ii. Tandaraukiwa kwa dhati.

**2. UFUPISHO**

***Soma makala haya kishaujibu maswali yanayofuata*.**

Tangu asili –na jadi nasikitika kusema kuwa tumekuwa tukiwakandamiza mabanati wetu na kuwateka bakunja ilhali wameonyesha kuwa mikono miepesi. Siku mojanilikuwa nikitembea na babu yangu mkongew tulipoliona tapo lawanawake kwambali. " Funika kombe mwanaharamu apite!" akininong'onezea, wanahusudu uwezo tu. " Kwa uchungu watu wa fikira sikuelewa yakini alichotazamia lakini hii leo nang'amua. Basi imenibidi kutupilia mbali dhana hiyo hafidhina kwani asifuye mvua aghalabu imemnyea.

Jina nzuri hung'aa gizani na bila shaka majina ya wanawake watu yameremeta kama nyota.

Kwanza, wamejitolea mhanga katika nyanja za masomo. Si baba ambao wamehitimu kutoka vyio vikuu vya humu nchini na vile vile vya ughaibuni na kujipa shahada kadha wa kadha. Wamepata ujuzi wa kutosha katika maswala tatizo kama vile udaktari na uanasheria. Hivi ni kumaanisha kuwa tuna madkari shupavu, basi tuwape nafasi tusiendelee kuwa nyuma mithili ya koti katika kipengele hiki muhimu cha maisha. Ni wanawake ndio, lakini mgalla muue na haki umpe!

Vile vile wanawake wenu wamejitokeza kifua mbele katika hatamu za uongozi. Mfano mwafaka katika serikali yetu, ambapo mawaziri ni wanawake. Nani asiyewafahamu, Cecily Kariuki, Racheal Omamo na Amina Mohamed? Wote wanafanya bidii za mchwa kustawi maisha ya wananchi. Ingekuwa ida na inadi kama tungewanyima viongozi hawa nafasi hizo na bila shaka jambo hili lingeathiri sana ujenzi wa taifa kwani ujuzi ndio nguzo ya kila kitu.

Kwa upande mwingine wanawake ni walezi waliomakinika.Kama tujuavyo udongo hupatilizwa ungali maji na usipoziba ufa huna budi kujenga ukuta. Nani ndio wamepokezwa jukumu mahiri la malezi? Nina zetu hujitolea kwa hali na mali kuwakuza watoto kwa tajriba zinazofaa na kuwafunza maisha ndiposa wasifunzwe na ulimwengu. Aliyemakinika atakubaliana name kuwa malezi si jambo la kufanyiwa mzaha katika harakati za ujenzi wa taifa. Na huu wajibu wote ni wa mwanamke.

Siwezi kuwasahau wanamke wanamuziki. Sote twaelewa kuwa kwa uchumi kama wetu, kutengemea kazi ya kuajiriwa ni kutaka muhali, chambilicho wahenga mchagua jembe si mkulima. Nashukuru wanadada wetu kwa kutia bidii katika uwanja wa mziki badla ya kuwa viruka njia. Kupitia kwa sauti nyororo kama kindanda wameweza kuwavutia hata watalii kuitembelea nchi yetu na kutuachia pesa za kigeni. Nawahimiza wengi kama iwezekanavyo wajaribu bahati yao…………jambo hili linajuza sana katika ujenzi wa taifa imara.

Katika kitengo cha spoti, waawake wamejizatiti vilivyo na kutokea wanashati kweli kweli.
Wamezika katika kaburi la sahau kuwa mchezo ni uawala wa wanaume. Kwa mfano katika michezo ya Olimpiki au jimuiya ya madola timu zetu za wanawake zimefanya vyema na kurudi nyumbani na nishani chungu nzima.Kwa wale wasiohusika katika michezo ningewasihi wajikakamue kisabuni basi wasiwaonee kijicho wenzao, kwani nyote ya mwenzio usilalie mlango wazi. I wapo tutazingatia ufanisi katika michezo, taifa hili halina budi kuendeleza uchumi wake.

Kwa kukunja jamvi, ningetaka kusisitiza kuwa hata ingawa jitihada haziondoi kudura, wanawake wetu wamefanya bidii za kutosha na inafaa wapewe nafasi sawa na wanaume katika ujenzi wa taifa.
Ningewahimiza wanaume wasiwe na kinyongo dhidi ya wamawake bali chanda chema huvishwa pete. Huu ndio wito wangu na kama tujuavyo kuro hasemi uongo na mbiu ya mgambo ikilia haikosi ina jambo.

***MASWALI***

a) Fafanua dhima ya mwanamke kulingana na makala haya. (maneno 70-80) (al.6)
b) Bila kubadilisha maana fupisha aya ya pili nay a tatu. (maneno 50- 55) (al.7)

**3. MATUMIZI YA LUGHA**

a) Andika maneno yanayoafiki maelezo haya: (al.2)
   i. Nazali ya midomoni, kipasuo sighuna cha midomoni, kiyeyusho, irabu ya chini kati.
   ii. Kipua ghuna cha kaakaa laini, irabu ya chini kati, kimadende ghuna cha ufizi, irabu ya chini kati.

b) Ainisha mofimu kwa kurejelea majukumu ya kisarufi katika neno hili. (al.3)
   Alijipelekea

c) Tunga sentensi ya swali ukitumia kiwakilishi nafsi ambata nafsi ya pili wingi. (al.2)

d) Kwa kutolea mifano, andika miundo miwili ya ngeli **ya LI-YA**. (al.2)

e) Andika sentensi ifuatayo kwa udogo wingi. (al.2)
   Mtoto mkaidi aliiba kitabu cha mwenzake.

f) Tunga sentensi ukitumia nomino dhahania katika wakati ujao hali ya kuendelea. (al.2)

g) Andika katika usemi halisi mtindo wa kitamthilia. (al.4)

Khaemba Ouma alitaka kujua ni kwa nini Wandera Otieno alipenda Hisabati, Wandera Otieno akamweleza alipenda Hisabati kwa kuwa babake alikuwa mwalimu wa somo hilo.

h) Unda nomino tatu kutokana na kitenzi **safari**. (al.3)

i) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya **daka** na **taka**. (al.2)

j) Tunga sentensi mbili tofauti kuonyesha matumizi ya lama za mtajo. (al.2)

k) Yakinisha katika umoja. (al.1)

Msipofanya bidii hamtapita mtihani.

l) Tunga sentensi ukitumia ka kuonyesha mfulilizo wa matukio ya matukio ya wakati uliopita.(al.2)

m) Unda sentensi changamano kutokana na tungo zifuatazo: (al.2)

Mtoto alikuja nyumbani jana.

Mtoto ndiye huyu.

n) Jibu swali kulingana na agizo. (al.2)

Halima alimbebea mwalimu mzigo kwa gari. (Anza kwa yambwa tendewa)

o) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielezo cha visaduku. (al.5)

Kile kizuri kilikuwa kikitumika ba baba Yule

p) Tunatumia shabaha tunapofurahishwa na jambo…………………………..tunapokula kiapo na yarabil…………………… (al.2)

q) Andika maana ya maneno yafuatayo: (al.2)

i. Kula kalenda

ii. Kula njaro.

4. **ISIMUJAMII.** (al.10)

Janga tandavu la korona limeathiri maisha ya kila mtu duniani, umepewa nafasi kama muuguzi kuzungumza na wanafunzi kuhusu suala hii. Andika sifa za lugha utakayotumia katika hotuba yako.

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(Kcse)*

**MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025**

**JINA: ……………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ……DARASA: …..........**

# SHULE YA UPILI YA WAVULANA WA STAREHE

**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**
**MAAGIZO**
**Maagizo**

- ***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
- ***b)*** *Jibu maswali yote.*
- ***c)*** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*
- ***d)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. UFAHAMU | 15 | |
| 2. UFUPISHO | 15 | |
| 3. SARUFI | 40 | |
| 4. ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**1. UFAHAMU** **(Alama 15)**

**Soma kifungukifuatachokishaujibumaswali**

.Ithibati ya maendeleoy a kiteknoloJia nchini Kenya tayari ipo.

Binafsi, nimeshuhudia teknolojia ya juu katika miundo ya simu na kompyuta, mifumo ya malipo ya kidijitali, mawasiliano na matumizi ya roboti yakizidi kurahisisha kazi katika sekta nyingi humu nchini.

Kila mwanauchumi atakubaliana nami kwa kuwa teknolojia ni nguzo muhimu katika kuongeza kiwango cha uzalishaji.

Lakini mbona uzalishaji umepungua katika miongo michache iliyopita ,katika kipindi ambapo teknolojia nyingi zilivumbuliwa? Sababu ni nini?

Nikichunguza data katika mataifa mengi ,hasa ya kiafrika,uzalishaji umepungua tangu mwanzo wa karne ishirini ya moja(21). Kumekuwa na sababu nyingi zilizochochea kushuka kwa utengenezaji wa bidhaa viwandani.

Sababu si teknolojia zenyewe bali ukosefu wakueneza teknolojia hizo kufikia kila mwananchi kwa mfano, program ya “my dawa” ni nzuri lakini ni wakenya wangapi wana uwezo wa kumiliki simu ya kisiasa ilikufaidika na huduma zake?

Ili kila mkenya aweze kumudu bei ya simu ya kisasa, basi uchumi wafaa kuimarika kiasi cha kuwa na hela za ziada za kununua vifaa vya kiteknolojia.

Kila mkenya na tambua kuwa ufisadi umelemaza kila sekta ya uchumi wetu,lakini hiki si kikwazo pekee cha teknolojia kukosa kuwafikia wananchi wamatabaka ya chini.

Hali hii pia inasababisha kampuni saba zilizokuwa zimeorodheshwa katika soko la hisa la Nairobi (NSE) kuondolewa kutokana na mapato ya chini kama licha ya kutumia teknolojia kuimarisha uzalishaji.

Kudorora kwa uzalishaji kunahusiana moja kwa moja na kupanuka kwa pengo na mapato baina ya matabaka mbalimbali ya kiuchumi. Kwa mfano ,kampuni ya Safaricom inapata faida kubwa zaidi kwa sababu teknolojia yake ya M-pesa imeenea kote,huku kampuni pinzani zikiumia.

Hivyo ,serikali kupitia mamlaka ya ushindani yafaa kuondoa vikwazo vinavyozua ushindani,nakuweka kanuni zinazozima ukiritimba.

Tukiachia kampuni chache umiliki wa soko husika, tutakuwa tunazuia kufurahia matunda yateknolojia, hakuna haja ya wagonjwa kukwama mashinani eti kwa sababu hawana simu za kupata huduma za kiafya kidijitali.

Teknolojia haitakuwa na maana iwapo mamilioni ya wakulima hawana uwezo wamiliki simu yenye apui na ya waunganishana soko la mazao yao pamoja na kuwaelekeza kwa maduka yenye dawa na mbegu za bei nafuu. Utazidi kuumia iwapo tutaachia Safaricom idhibiti soko la kutuma hela kidijitali.

Sera kuhusu teknolojia nchini zafaa kuboreshwa ilikuvumisha ubunifu na kueneza hadi mashinani.Kuna raha gani kuwa teknolojia nyingi zisizo saidia kukuwa kwa uchumi wetu? Teknolojia isiyoenea itazidi kulemaza uzalishaji tusipochukua hatua.

Maswali

a).Yape makala uliyoyasoma anwani mwafaka. **(alama.1)**

b). Toa sababu za teknolojia kulemaza uzalishaji wa mali. **(alama. 4)**

c) . Kwa mujibu wa makala haya ni nini umuhimu wa teknolojia.? **(alama.2)**

d) .Ni hatua ipi serikali inastahili kuchukua ilikuzuia ukiritimba **(alama.2)**

e).Ni nini msimamo wa mwandishi kuhusu teknolojia **(alama.2)**

f) .Fafanua msamiati huu kimuktadha **(alama.2)**

(i) Idhibati……………………………………………………………………………………………..

(ii) Ukiritimba…………………………………………………………………………………………..

**2. UFUPISHO** **(alama 15)**

**Soma taarifaifuatayokishaujibumaswali.**

Ajira ya watoto ni tatizo sugu linalo kumba ulimwengu wa sasa, hasa katika nchi zinazoendelea. Jambo la kusikitisha ni kwamba hivi ndivyo ilivyo katika nchi nyingi za ulimwengu huu. Kuna idadi kubwa ya watoto wanaoajiriwa katika nyanja mbalimbali za jamii. Zipo sababu nyingi zinazo wasukuma watoto kutafuta ajira barani Afrika kwa mfano, familia nyingi huishi maisha ya ufukara hivi kwamba hushindwa kuyatimiza mahitaji muhimu hususan kwa watoto. Kupanda kwa gharama ya maisha kuna zidisha viwango vya umasikini. Ukosefu wa lishe pia huwafanya watoto kutoroka nyumbani kutafuta ajira. Janga la UKIMWI limesababisha kuwepo kwa idadi kubwa ya mayatima wanaoishia kutafuta ajira ili kuyakimu maisha. UKIMWI umezifanya familia nyingi kuwaondoa watoto shule iliwaweze kuajiriwa kwa lengo la kuanzisha pato la familia hizo. Watoto wengine hutoroka makwao kwa sababu ya maonevu. Maonevu haya ni kama vile kupigwa, kutukanwa kila wakati, kunyanyaswa kijinsia na kadhalika. Huko nje hutaabishwa kimwili na kiakili. Hufanyizwa kazi za sulubu zenye malipo duni au wasilipwe kabisa. Hili huwasononesha na kuathiri afya yao.

Uundaji wa umoja wa Afrika hivi majuzi ni hatua muhimu ya kushughulikia matatizo ya Afrika kama vile ajira ya watoto, kuzorota kwa miundo misingi, magonjwa, njaa, umaskini, ufisadi na ukabila. Katika kushughulikia haki za watoto, nchi za Afrika hazina budi kuzingatia masharti yalivyowekwa na umoja wa mataifa kuhusu haki za watoto. Nchi nyingi za Afrika ziliidhinisha mkataba wa masharti hayo ikiwemo nchi ya Kenya.

Nchi hizi basi lazima zishughulikie haki za watoto kupitia sheria za nchi. Watoto ni rasilmali muhimu na ndio tumaini la kuwepo kwa kizazi cha binadamu.

Maswali.

(a) Eleza mambo yote muhimu anayozungumzia mwandishi katika aya ya kwanza.

**(maneno 6, 1 mtiririko)**

(b) Bila kubadilisha maana aliyokusudia mwandishi, fupisha aya mbili za mwisho. (**maneno50 - 55**)

**(alama 7, 1 mtiririko)**

**MATUMIZI YA LUGHA** **(ALAMA 40)**

**a)** Andika maneno yenye miundo ifuatayo**(alama 2)**

*(i)* ***Kikwamizo hafifu cha ufizi,irabu ya mbele kati,nazali ya midomoni,irabu ya chin ikati***

*(ii)* ***Nazali ya ufizi,Irabu ya juu mbele, kipasuo hafifu cha midomo,irabu ya nyuma kati***

**b)** Ainisha mofimu katika maneno yafuaatayo: **(alama 2)**

(i) Asemavyo

(ii) Mwangwi

**c)** Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili ya kiambishi `ni` **(alama 2)**

**d)** Ainisha vitenzi katika sentensi: **(alama 3)**

Ndege yu taabani, hata hivyo anajaribu kujinasua.

**e)** Tunga sentensi ukitumia kirai kihusishi kama kielezi. **(alama 1)**

**f)** Unapo adhirika na jambo unasema hewala! Unaposhangilia timu yako kwa kupata ushindi unasema……………………………………..na unapotaka kitu kinusurike unasema…… **(alama 2)**

**g)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya kinyume: **(alama 2)**

Wakimbizi walihama na wakavunja kambi.

**h)** 8.Tunga sentensi yenye muundo ufuatao **(alama 2)**

Nomino ya jamii, kirai kihusishi ,kitenzi kishirikishi, kielezo cha mahali.

**i)** Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo: **(alama 2)**

Mtoto huyo mzuri alifika shuleni asubuhi na mapema.

**j)** Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Wachezaji walishinda mechi wakatuzwa.

**k)** Tunga sentensi na ubainishe shamrisho kitondo, kipozi na ala . **(alama 3)**

**l)** Onyesha miundo miwili ya nomino katika ngeli ya A-WA **(alama 2)**

**m)** Yakinisha sentensi ifuatayo katika nafsi ya pili umoja. **(alama 2)**

Hataenda shuleni kesho.

**n)** Eleza dhima ya tatu za viambishi tamati mbali na kauli ya kutenda/kiishio. **(alama 3)**

**o)** Tunga sentensi moja katika wakati uliopita hali ya mazoea. **(alama 2)**

**p)** Changanua sentensi zifuatazo kwa kielezo cha mistari.

(i) Huyu wake alikuwa amefika lakini hatukumjua. **(alama 2)**

(ii) Mtoto wa Shangazi hucheka sana. **(alama 1)**

**q)** Eleza maana tatu zinazojitokeza katika sentensi. **(alama 3)**

Niliona mamba.

**r)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo. **(alama 2)**

Madebe hayo yatasafirishwa pamoja na nyundo hizi.

**ISIMU JAMII** **(ALAMA 10)**

Wewe ni mfanyibiashara katika Soko la Kongomawe. Fafanua sifa **kumi** za lugha utakayotumia ilikuwavutia wateja wako.

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(Kcse)*

**MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025**

**JINA: ……………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ……DARASA: …............**

# SHULE YA UPILI YA WASICHANA WA ASUMBI

**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**
**MAAGIZO**
**Maagizo**

- ***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
- ***b)*** *Jibu maswali yote.*
- ***c)*** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*
- ***d)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE**

| **SWALI** | **UPEO** | **ALAMA** |
|---|---|---|
| 1. UFAHAMU | 15 | |
| 2. UFUPISHO | 15 | |
| 3. SARUFI | 40 | |
| 4. ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

1. **UFAHAMU: (alama 15)**

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali**

Mageuzi yanayotarajiwa katika idara ya polisi nchini yameanza **kubisha hodi** baada ya kuzinduliwa kwa mtaala mpya wa kutoa mafunzo kwa maafisa wa polisi.

Mtaala huo uliozinduliwa rasmi na Waziri wa Usalama wa ndani Prof. George Saitoti Jumatatu iliyopita, unalenga kuimarisha utendakazi katika kikosi ambacho kwa muda mrefu kimelaumiwa kwa kukolewa ufisadi na uvunjaji wa haki za kimsingi.

Akihutubu katika hafla ya kuzindua mtaala huo iliyofanyika katika makao makuu ya shirika la ndege nchini mtaani Embakasi, Nairobi, Jumatatu iliyopita, Waziri Saitoti alisema, kuzinduliwa kwa mtaala huo kuliashiria mwanzo wa mageuzi makubwa yanayonuiwa kukipatia kikosi hicho sura mpya.

"Nyakati zimebadilika na tutawapa maafisa wa polisi mafunzo mapya. Tunataka kuunda kikosi imara chenye nidhamu na kinachoheshimu haki za kibindamu. Tunataka kuwa na kikosi kinachoakisi sura ya karne hii na kinachoafikia hadhi ya kimataifa," Waziri Saitoti alisema.

Mtaala huo mpya wa kutoa mafunzo kwa maafisa wa polisi ni matunda ya jopo lililoteuliwa na Rais mwaka wa 2003 kutathmini mageuzi katika kikosi hicho. Uliandaliwa na taasisi ya elimu nchini ikishirikiana na wanafunzi kutoka chuo cha mafunzo ya polisi cha Kiganjo kwa usaidizi wa wataalamu wa masuala ya usalama kutoka Uswizi.

Chini ya mtaala huo, maafisa wa polisi watapokea mafunzo kwa kipindi cha kati ya miezi 15 na 21 kinyume cha awali ilipowachukua miezi 9 tu kukamilisha mafunzo.

Aidha, alama za kujiunga na kikosi hicho zimeongezwa. Katika mtaala huo, wanaonuia kujiunga na idara ya polisi wa kawaida, kitengo cha G.S.U au polisi wa utawala ni lazima wawe wamepata alama ya C katika mtihani wa K.C.S.E na itawachukua miezi 15 kukamilisha mafunzo ikiwa ni pamoja na miezi 3 ya kujifahamisha na huduma ya kikosi.

Hii ni tofauti na awali ambapo alama ya kujiunga na kikosi cha polisi ilikuwa ni D katika mtihani wa KCSE. Mtaala mpya unasema ni sharti asilimia 10 ya makurutu wawe na digrii kutoka chuo kikuu na watapokea mafunzo kwa miezi na kuhitimu cheo cha Naibu wa Inspekta wa Polisi.

Kuanzia sasa, ni sharti usawa wa kijinsia uzingatiwe kikamilifu katika uajiri wa maafisa wa polisi. Wachanganuzi wa masuala ya usalama wanasema ukizingatiwa ipasavyo, mtaala huo utasaidia kuunda msingi dhabiti wa kikosi imara ambacho Wakenya wamekuwa wakihitaji.

**Maswali**

1. a) Ni dalili ipi inayoonyesha mwanzo wa mageuzi? **(alama 1)**

   b) Mtaala mpya unalenga nini? **(alama 4)**

   c) Eleza lawama zinazoelekezewa kikosi cha polisi **(alama 2)**

d) Kwa mujibu wa taarifa eleza mageuzi matatu yaliyofanywa katika kikosi cha polisi **(alama 3)**

e) Taja makundi mawili yaliyohusika katika kuandaa mtalaa mpya **(alama 2)**

f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika kifungu **(alama 3)**

i) Kubisha hodi

ii) Kukolewa

iii) Makurutu

2. **UFUPISHO** **(alama 15)**

**Soma makala haya kisha ujibu maswali yanayofuata**

Mwezi jana serikali ya kitaifa na zile za kaunti ziliwasilisha makadirio yao ya bajeti, miezi miwili kabla ya mwaka wa kifedha kuisha kama zinavyohitajika na katiba. Serikali hizo zilieleza jinsi zinavyonuia kutumia mabilioni ya pesa kufadhili shughuli za mwaka ujao wa kifedha wa 2013/2014.

Serikali ya Rais Uhuru Kenyatta ilisema itatumia shilingi 1.6 trilioni kufadhili maendeleo na shughuli za sekta na idara zake tofauti. Makadirio haya yaliwasilishwa na kiongozi wa walio wengi bungeni, Bw. Aden Duale. Hata hivyo yalikosa kueleza jambo moja muhimu – jinsi kitita hicho kitakavyopatikana. Nasema hivi kwa sababu kuna habari ambazo zimenipa tumbojoto na wasiwasi mkubwa. Imebainika kuwa kufikia mwishoni mwa
Machi mwaka huu, Kenya ilikuwa inadaiwa shilingi 1.8 trilioni na wafadhili wa humu nchini wa kigeni. Kama habari hizi hazijakushtua sitakulaumu kwa sababu huenda ukuwa hujui ukubwa wa kiasi cha fedha. Ili uweze kuelewa, nitazigawanya fedha hizi miongoni mwa Wakenya milioni 40 ili tujue kila mkenya anadaiwa kiasi gani. Kila Mkenya nchini, wakiwemo watoto na wazee wakongwe, anadaiwa shilingi 45,000! Hivyo basi ili deni hili liweze kulipwa, kila Mkenya atalazimika kutoa kiasi hicho cha fedha.

Ni deni ambalo Rais Uhuru Kenyatta alirithi kitoka kwa mtangulizi wake, Rais Mwai Kibaki ambaye utawala wake ulivunja rekodi ya kukopa. Wahenga hawakukosea dawa ya deni ni kulipa. Deni hili linapaswa kimkosesha usingizi Rais Kenyatta ambaye anapaswa kutafuta njia za kulilipa bila kuathiri uchumi, maendeleo na utekelezaji wa ahadi nyingi alizowapatia Wakenya wakati wa kampeni.

Hili halitafanyika kama Serikali itatenga fedha nyingi kuwalipa maafisa wake mishahara na marupurupu minono pamoja na kuwapa mabilioni ya pesa kununulia magari ya kifahari. Pengine Rais hajafahamiswa kuwa mwaka ujao wa kifedha serikali itajipata pabaya kwani Halmashauri ya Ukusanyaji Ushuru nchini (KRA), haitaweza kukusanya kiwango kilichowekwa na serikali baada ya shughuli ya ukusanyaji ushuru kutatizwa na hofu iliyotanda wakati wa uchaguzi mkuu.

KRA ilikuwa imekusanya shilingi 560 bilioni kufikia mwishoni mwa Machi ilhali ilikuwa imeagizwa kukusanya. Baada yake zimeomba serikali kuu ujaze pengo hilo au zipewe idhini ya kukopa.

Rais Kenyatta hana budi kuchukua hatua za dharura kuhakikisha kuwa wakenya hawataendelea kuandamwa na madeni maishani mwao.

(imenukuliwa kutoka Taifa Leo – Mei 9, 2013)

a) Kwa maneno yasiyozidi 70, fupishsa aya za kwanza nne. **(alama 9)**

Nakala ya matayarisho

Nakala safi

b) Kwa nini serikali haitaweza kulipa madeni yake. (maneno 40-50) **(alama6)**

Nakala ya matayarisho

Nakala safi

**3. MATUMIZI YA LUGHA**

a) Toa maelezo ya jinsi ambavyo hewa huzuiliwa wakati wa kutamka sauti **inzi** **(alama 2)**

i. /P/
ii. /ch/
iii. /m/
iv. /r/

b) Bainisha mofimu katika neno : Tuliyemcheza. **(alama 3)**

c) Tunga sentensi moja yenye kitenzi kishirikishi kikamilifu na vitenzi sambamba **(alama 3)**

d) Tumia neno msiri kama kielezi cha mfanano**.** **(alama 1)**

e) Onyesha namna tatu za kutumia “na” katika sentensi moja, kisha neleze matumizi husika. **(alama 4)**

f) Ziweke nomino hizi katika ngeli zake .

i. Kiwavi-
ii. Vita-

g) Tambua virai vilivyopigiwa mstari ni vya aina gani na uonyeshe miundo yake **(alama 4)**

i. <u>Ndege iliyotengenezwa jana</u> itapelekwa Ulaya.
ii. Wenzetu <u>walikuwa wakijinaki kabla ya dimba</u>

h) Eleza maana ya sentensi hizi kwa kuzingatia sehemu zilizopigiwa mstari **(alama 2)**

i. Mgonjwa alinywe<u>sheka</u> uji-
ii. Mvua ilim<u>nyia</u> jana-

i) Tambua shamirisho na chagizo katika sentensi hii **(alama 4)**

Juma alinjengea nyanya nyumba kwa mawe nzuri sana.

j) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo bila kuambisha na ku **(alama 2)**

i. Shika

ii. Shona

k) Tumia njia ya matawi kuchangana sentensi ifuatayo **(alama 4)**

Alipotuona alituangalia lakini sisi tulimuona

l) Kamilisha kwa viingizi mwafaka

i. Gari la Mwangeka lilisukumwa ------------------------ **(alama.1)**

ii. Jiwe lilianguka majini--------------------------- **(alama.1)**

m) Tumia vitate vya baba, sara na toa katika sentensi tatu tofauti **(alama 3)**

n) Yakinisha:- usipocheza vizuri hautachaguliwa **(alama 2)**

o) Onyesha jinsi ya kutumia nukta pacha katika sentenzi **(alama 1)**

p) Andika sentensi ifuatazo kwa lugha ya tafsida **(alama 1)**

Mwanafunzi ameenda kwenye choo.

q) Amrisha katika nafsi ya tatu wingi

Cheza **(alama 1)**

**4. ISIMU JAMII (alama 10)**

**Soma kifungu kifuatacho halafu ujibu maswali.**

“Naona “Horsepower” mwenyewe ndiye atakayepiga, atakayecheza foul hiyo. Wachezaji wa……”

i) Tambua sajili inayorejelewa **(alama 2)**

ii) Tambua sifa zinazobainisha sajili rejelewa **(alama 8)**

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(Kcse)*

**MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025**

**JINA: ……………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ……DARASA: …............**

# SHULE YA UPILI YA WAVULANA WA ALLIANCE

**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**
**MAAGIZO**
**Maagizo**

- ***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
- ***b)*** *Jibu maswali yote.*
- ***c)*** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*
- ***d)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE**

| **SWALI** | **UPEO** | **ALAMA** |
|---|---|---|
| 1. UFAHAMU | 15 | |
| 2. UFUPISHO | 15 | |
| 3. SARUFI | 40 | |
| 4. ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**1. UFAHAMU (ALAMA 15)**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Ufisadi ni uhalifu unaohusu kuzitumia njia za ulaghai kujipatia pesa, mali au vitu hasa vya umma. Nchini Kenya ufisadi hujitokeza kwa njia mbalimbali na kila mojawapo ina athari zake. Kwa mfano, kuna maafisa wa serikali wajipatiao pesa kwa kuuza stakabadhi za serikali kama vile pasi, vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya kumiliki mashamba, vitambulisho na nyinginezo kwa raia, kuna hatari kubwa kwa sababu watu wasio raia wa Kenya wameweza kusajiliwa kama wakenya na kuendeleza uhalifu kama ugaidi, wizi na ulanguzi wa dawa za kulevya.

Wengine hujipatia vibali vya kufanya kazi na kuajiriwa kazi ambazo zingefanywa na wakenya. Hii imechangia ongezeko la uhaba wa kazi nchini. Watumizi wengine wa umma huuza mali ya serikalikama vile magari, nyumba na ardhi na kufutika pesa za mauzo mifukoni mwao. Wengine wao hujinyakulia na kufanya vitu hivyo kuwa mali yao. Ufisadi wa aina hii umegharimu serikali kiasi kikubwa cha fedha. Serikali imelazimika kununulia maafisa wake magari baada ya muda mfupi, kulipia wafanyikazi wake kodi za nyumba na kukosa viwanja vya upanuzi na ujenzi wa shule hospitali, vituo vya polisi na taasisi zingine maalumu.

Baadhi ya wataalamu kama madaktari huiba dawa kutoka hospitali za umma kupeleka vituo vyao vya afya. Pia hutumia wakati wao mwingi katika kazi zao za kibinafsi na kuwaacha wagonjwa katika hospitali za umma wakihangaika. Sio madaktari tu, kuna masoroveya, wahandisi, mawakili, walimu na mahasibu ambao hukwepa majukumu yao serikalini na kufanya kazi za kibinafsi. Wengine wasio wataalamu huendesha biashara za aina tofauti, na huku wanaendelea kupokea mishahara.

Wanafunzi wanaotaka kujiunga na vyuo na shule bora za umma na hawakuhitimu wakati mwingine hulazimika kusalimu amri na kutoa hongo hili wapate nafasi za kusoma. Kiasi cha pesa kinachohitajika huwa kikubwa hivi kwamba ni wachache humudu hizo rushwa. Wale wasiojimudu kifedha hubaki wakilia ngoa. Kuna wazazi ambao hutumia vyeo vyao na 'undugu' kupata nafasi zilizotajwa, jambo ambalo huwanyima wanafunzi werevu kutoka jamii maskini nafasi ya kupata elimu. Matokeo huwa ni kuelimisha watu wasiostahili na ambao mwishowe hawaziwezi kazi wanazosomea wakihitimu na kuanza kuhudumia jamii.

Ufisadi umekita mizizi na kushamiri katika sekta za umma za kibinafsi kwa upande wa kuajiri wafanyakazi. Ni vigumu kupata kazi ikiwa hujui mtu mkubwa katika shirika linalohusika au uzunguke mbuyu. Matokeo ni kuajiri wafanyakazi wasiohitimu na wasiowajibika kazini.

Vyeo na madaraka katika baadhi ya mashirika hutolewa kwa njia ya mapendeleo na ufisadi. Kwa hivyo, wafanyakazi wenye bidii hufa moyo kwa sababu hawasaidiwi ipasavyo. Badala yake wale wasioleta bidii hupandishwa vyeo na kuwaacha palepale.

Hata hivyo, mbio za sakafuni huishia ukingoni. Serikali imetangaza vita dhidi ya ufisadi. Tayari tume kadhaa zimebuniwa kuchunguza visa vya ufisadi uliotekelezwa hapo mbeleni. Mojawapo ya tume hizo ni Tume ya kuchunguza Kashfa ya "Goldenberg" ambapo pesa za umma (mabilioni) ziliporwa na mashirika na

watu binafsi kwa njia siziso halali. Watakaopatikana na hatia ya kushiriki ufisadi huo watahitajika kurudisha pesa hizo.

Serikali pia imeunda kamati ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi waliohasiriwa na mawakili walaghai ambao hupokea ridhaa kwa niaba ya wateja wao na kukosa kuwalipa au kuwatetea mahakamani ilhali wamekwishalipwa. Ni matumaini yetu kuwa ulaghai huu utaangamizwa kabisa kwani hakuna refu lisilokuwa na ncha.

**Maswali**

a) Eleza aina nne za ufisadi zilizotajwa katika kifungu ulichosoma. (alama 4)

b) Kulingana na kifungu ulichosoma,ufisadi umeathiri nchi yetu kwa njia gani ? (alama 2)

c) Serikali inafanya jitihada gani ili kukomesha ufisadi ? (alama 3)

d) Kwa maoni yako, unafikiri ufisadi husababishwa na nini ? (alama 2)

e) Toa msamiati mwingine wenye maana sawa na rushwa (alama 1)

f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa kifunguni: (alama 3)

i) shamiri ____________________________________________________________

ii) waliohasiriwa ______________________________________________________

iii) wakilia ngoa _______________________________________________________

**<u>2. UFUPISHO ( ALAMA 15)</u>**

*Soma Makala haya kisha ujibu maswali.*

**<u>Umuhimu wa vyombo vya habari</u>**

Vyombo vya habari hutumika kupasha watu habari kutoka upande mmoja hadi mwingine. Vyombo hivi vina manufaa kwetu. Vyombo hivyo ni kama vile runinga, redio, magazeti, tarakilishi na vinginevyo. Umuhimu mmoja wa vyombo hivi ni kueleimisha. Watu huelimishwa kuhusu jinsi ugomvi unaweza kuepukika katika familia. Pili huelimishwa juu ya magonjwa tofauti kama vile ukimwi, kipindupindu na mengine na jinsi ya kujikinga au kupata matibabu.

Mbali na hayo, vyombo hivi hutumika kuarifu. Watu huarifiwa kuhusu serikali yao, hususan jinsi mambo yanavyoendeshwa, uhusiano kati ya wajumbe serikalini na hapo kuwaacha watu na maarifa ya kufanya uamuzi bora utakaowanufaisha. Vyombo hivi pia huarifu kuhusu matukio kama ajali za barabarani, majumba kuchomeka na hata mashambulizi ya kigaidi pamoja na matukio mengine. Hiini muhimu kwani watu huwa na habari kuhusu yanayoendelea.

Vyombo hivi, kwa upande mwingine, huchangia kwa kiwango kikubwa umoja wa wananchi. Watu waishio sehemu mbalimbali wanaweza kufahamu vile wenzao katika sehemu nyingine waishivyo kutokana na lelemama, michezo ya kuigiza na kadhalika kutoka sehemu moja hadi nyingine. Chambilecho wahenga umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

Fauka ya hayo, vyombo hivi ni muhimu kwani kupitia kwavyo watu wengi wameweza kupata gange. Watu hawa ni kama vile waandishi wa habari, wahandisi wa mitambo, watangazaji na

kadhalika. Wao huweza kujimudu, kumudu familia zao na hata kukuza uchumi.

Vyombo vya habari ni muhimu kwa kuwa ni vyombo vya kutumbuiza vilvile. Kutokana na kutumbuizwa, waliotoka kufanya kazi za sulubu hata kazi zingine zozote huweza kupumzika vyema kwa kuburudishwa na hivyo kuwa wachangamfu tena. Mbali na kupumzisha wanaoandaa burudani kama vile muziki na maigizo kupitia kwa vyombo hivi vya habari hasa vijana huweza kupata hela za kujikimu na hivyo basi kujiepusha na visa vya uhalifu, mihadarati na hata uasherati.

Mwisho, vyombo vya habari hutumiwa na wanasiasa wakati wa uchaguzi ili kueneza manifesto zao na za vyama vyao. Kupitia kwa vyombo hivi, wananchi kote nchini wanaweza kujua kujua wanasiasa ambao wananuia kuleta maendeleo na hivyo kufanya maamuzi yao wakati wa uchaguzi.

Aidha, kupitia kwa vyombo hivi tume ya uchaguzi inaweza kuwaeleza wananchi kuhusu mambo ambayo wanafaa kujiepusha nayo, kwa mfano kupokea hongo ili kutovunja sheria za uchaguzi.

Kwa jumla vyombo vya habari ni muhimu katika maisha ya jamii. Vyombo hivi vinafaa kutumiwa ipasavyo ili navyo viwatumikie wananchi kwa njia mwafaka. Vyombo hivi vikitumiwa visivyo vinaweza kuleta hasara kubwa na hata maangamizi.

**MASWALI**

a) Kulingana na Makala, vyombo vya habari vina wajibu gani katika jamii? ( maneno 60)
b) Mbali na umuhimu wa vyombo vya habari, vyombo hivi vinaweza kuletea jamii hasara kwa njia nyingi. Eleza ( Maneno 50) ( Alama 7, moja mtiririko. )

## <u>3. *MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)*</u>

(a) Tambua na utolee sababu sauti ambazo hazifai kuwa miongoni mwa zile zilizotajwa hapo chini ( alama 2)

/ch/, /g/, /j/, /k/

(b) Bainisha mofimu katika utungo ufuatayo: ( alama 3)

Hakumjia

c) Kwa kutolea mifano, taja matumizi manne ya kiambishi m (al 2)

d)Eleza majukumu mawili ya sentensi ifuatayo. ( Al2)

Panda mtini na uangue matunda kwa vile yameiva vizuri.

e) Tunga sentensi kwa kutumia kitenzi cha silabi moja chenye maana ya kuogopa katika kauli ya kutendeka. (alama 2)

f)Ainisha kielezi katika sentensi ifuatayo na ukibadilishe kiwe kiwe kielezi igizi (al 2)

Mbwa yule mweusi alibweka kwa hasira

g) Bainisha mwingiliano wa maneno katika sentensi hii (al 2)

Wanafunzi walifanya haraka japo haraka yao iliwatia taabani.

h) Ainisha maneno yaliyopigiwa mstari (al 1)

<u>Naam</u>... ameleta <u>machache.</u>

i)Tunga sentensi moja kwa kutumia kihisishi cha masikitiko (al 2)

j) Yakinisha katika udogo wingi (al 2)

Ng'ombe yuyu huyu hajazaa ndama mkubwa

k) Tunga sentensi moja kudhihirisha matumizi mawili ya kibainishi (al 2)

l) Andika katika usemi halisi. (al 2)

Mama aliwahimiza warudi siku hiyo la sivyo wangekosa tuzo.

m) Maneno yafuatayo yamo katika ngeli zipi (al 2 )

wembe___________________________________________________________________

mnyoo___________________________________________________________________

n) Tambua kiima na yambwa katika sentensi ifuatayo (al 2)

Daktari yule hupigiwa nguo pasi na halima

o) Ainisha fungu la maneno lenye muundo wa kiima na kiarifa ambalo linakamilika au lisilokamilika kimaana katika sentensi ifuatayo (al 2)

Mtoto huyu atapita mtihani iwapo atasoma kwa bidii

p) Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu (al 2)

Msomi hakutuzwa siku hiyo

q) Pambanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha vishale (al 4)

Letu lililopaliliwa limetuletea mazao mengi.

r) Amechanjiwa kuni ina maana ya kutenda kwa niaba ya.Eleza maana nyingine mbili zinazobainishwa na sentensi hii. ( Al 2)

s)Tia nanga ni fika na____________ ni kuwa na wivu (al 1)

t)Andika sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo (al 1)

Kupanda mchongoma,kushuka ndio ngoma

Anza kwa Kushuka...........

## 4. ISIUMUJAMII (ALAMA 10)

a) Taja mambo manne yanayopelekea kufa kwa lugha (al 2)

b) Kwa mifano minne,elezea namna muktadha unavvyoathiri mitindo ya lugha (al 4)

c) Ukiwa mkaguzi mwakilishi katika mashindano ya kiswahili ,fafanua na kueleza mambo yanayochangia wanafunzi kufanya makosa ya kisarufi na ya kimatamshi katika lugha ya Kiswahili ( al 4)

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(Kcse)*

## MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: ……………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ……DARASA: …............**

# SHULE YA UPILI YA WASICHANA WA ALLIANCE

**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**
**MAAGIZO**
**Maagizo**

- ***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
- ***b)*** *Jibu maswali yote.*
- ***c)*** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*
- ***d)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE**

| **SWALI** | **UPEO** | **ALAMA** |
|---|---|---|
| 1. UFAHAMU | 15 | |
| 2. UFUPISHO | 15 | |
| 3. SARUFI | 40 | |
| 4. ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**<u>UFAHAMU (ALAMA 20)</u>**

**Soma taarifa ifuatayo kasha ujibu maswali**

Inasemekana kuwa uongozi hutoka kwa Maulana. Siku hizi, kauli hii inaonekana kinyume na inapingwa vikali na mahuluki wengi. Hali hii imetokana na ukweli kuwa viongozi wengi wamekuwa katili. Wengi wao hutekeleza maovu bila kujali wala kubali. Kiongozi yeyote Yule anayedai kuwa mwema hana budi kuwa **mwongofu** na wa kuaminika; anafaa kuwa kielelezo kwa wafuasi wake. Hili lisipotendeka **vurumai** huzuka miongoni mwa watu.

Kiongozi bora sharti awe mnyenyekevu. Mtu mwenye mashauo si kiongozi bora. Kiongozi wa aina hii huwahudumia watu kwa moyo wake wote. Jambo hili huwafanya watu waridhike. Watu wengi hawapendi viongozi wanaojipigia debe kila wakati. Viongozi kama hawa huwachosha na hata kuwachusha wafuasi wao. Matokeo ya haya yote huwa ni majuto kwa raia huku wakijiuliza kilichowafanya wawachague.

Maadili ni sifa nyingine inayomtambulisha kiongozi bora. Kiongozi wa aina hii hafai kujihusisha na vitendo vya kikatili kama matumizi ya mabavu, mauaji na hata ufisadi. Anafaa kuwajibika kazini na kuwa tayari kuyasikiliza malalamishi ya watu anaohudumia. Inamlazimu kiongozi bora kuwaheshimu wananchi bila kuzingatia vyeo vyao; asidharau maoni yao kuhusu jinsi ya kuuboresha uongozi wake.

Pia, kiongozi bora anastahili kuwa na huruma. Hii inamaanisha kuwa anafaa kuwa tayari kuwaonea **kite** wananchi wanaotatizika maishani. Anafaa kubuni mikakati ya **kuwaauni** watu kama hawa. Hali hii huwafanya watu waongeze imani yao kwa kiongozi kama huyu. Ikiwa kiongozi atajitia hamnazo anapofahamishwa kuhusu **masaibu** ya wananchi, watu watatamani siku ya kumtoa mamlakani ama kwa kupiga kura au kumwomba Jalali ahitimishe uongozi wake haraka iwezekanavyo.

Utetezi wa kazi za wanyonge ni sifa nyingine muruwa ya kiongozi bora. Kiongozi kama huyu anapaswa kuwa tayari kuhakikisha kuwa sheria inafuatwa katika himaya yake. Hali hii huwafanya wanajamii kupata haki zao bila **kubughudhiwa**. Wale wasiopata haki wanazostahili wanastahili kuchungiwa maslahi na kiongozi kama huyu.

Hakuna mtu anayestahili kuitwa kiongozi bora kama si mpenda amani. Kiongozi anayepalilia rabsha katika jamii hafaulu hata kidogo kuitwa kiongozi bora. Ni wajibu wa kiongozi kusuluhisha ugomvi wowote uliomo miongoni mwa wanajamii. Jambo hili huifanya kunawiri na kuzagaa kote kote.
Wanajamii wakiishi katika mazingira yenye amani huweza kutekeleza shughuli zao bila hofu wala kindubwendumbwe.

Kiongozi bora anastahili kujitenga na ubaguzi kama ardhi na mbingu. Ni ukweli usiopingika kuwa baadhi ya viongozi huwabagua wananchi kwa misingi ya kitabaka, kijinsia na kikabila. Ni muhimu kwa kiongozi yeyote Yule kuhakikisha kuwa kuna umoja wa wananchi katika jamii. Hii ni kutokana na ukweli kuwa jifya moja haliwezi kuinjika chungu. Astahili kuhubiri umoja katika hatamu ya uongozi wake. Nao wananchi humkumbuka daina dawamu.
Uwajibikaji ni kitambulishi kingine cha kiongozi aali. Kiongozi bora anafaa kuwajibika kazini. Kiongozi anaystahili ni Yule ambaye anatekeleza majukumu yake kikamilifu. Suala la upigaji zohali ni muhali kwa kiongozi wa aina hii. Ni mtu anayefanya kazi kimhanga ili kuboresha maisha yake naya wateja wake.

Kiongozi yeyote asiye na hulka tulizozungumzia huishia kuwa hasimu wa watu. Viongozi wote wanastahili kuyapa kipaumbele maslahi ya umma. Hawafai kuwa wabinafisi. Ni watu wenye utu, maarifa, waongofu na wenye bidii. Wananchi wana wajibu wa kuwachagua viongozi wanaofaa bila kupofushwa na ahadi za uongo.

**Maswali**

(a) Kwa nini kauli kuwa, 'uongozi hutoka kwa maulana', yaonekana kinaya na kupingwa na watu wengi. (ala.1)

(b) Eleza kiini cha watu wengi kuchukia viongozi wanaojisifu kila wakati. (alama 2)

© Eleza matokeo ya kiongozi kuwasaidia wananchi wanaotatizika maishani. (alama 1)

(d) Taja misingi mitatu inayotumiwa na baadhi ya viongozi kuwabagua wananchi.(alama 3)

(e) Eleza maoni ya mwandishi kuhusu jukumu la wananchi kuhakikisha kuwa uongozi bora umedumu. (alama 1)

(f) Taja vitambulishi vine vya kiongozi bora. (alama 4)

(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu. (alama 3)

(i) Mwongo:

(ii) Kuwauni:

(iii) Kite:

**2. UFUPISHO**

Ni dhahiri shahiri kwamba **uharamia** umechipuka kama desturi na mfumo wa maisha katika siku za hivi karibuni. Janga hili limeshamiri hususan pembeni mwa bara la Afrika na kanda ya Afrika Mashariki.
Taarifa za uharamia zimetawala vyombo vya habari, kiasi kwamba haipii siku bila kuripotiwa visa vipya vya matendo haya mabovu ambayo yanaweza tu kumithilishwa na uhayawani. Matukio haya yamewalimbikizia mabaharia wan chi husika, simanzi na masaibu yasiyoweza kuatiwa kwenye mizani.

Yamkini tatizo hili halitokei pasi na kumotishwa na kitita kikubwa cha fidia kinachodaiwa na maharamia hawa. Aghalabu suala hili lahusishwa pakubwa na azma na ari ya kuendeleza ujambazi wa kimataifa sawia na ulipuaji wa bomu mjini Nairobi na Dar –es salaam mnamo Agosti 7,1998 na tukio la Septemba 11, mwaka wa 2001 kule Marekani. Maafa na uharibifu wa mali si hoja, la mno kwa maharamia ni kutosheleza matakwa yao. Kwa upande mwingine, ukosefu wa tawala- wajibika katika maeneo kunakotokea unyama huu ni thibitisho tosha la mazingira yanayowezesha na kuruhusu kuchipuka kwa janga hili.

Mchipuko wa baa la uharamia umelengwa jamii ya kimataifa ambayo ni mhudumu mkuu wa harakati za kusitisha majanga makubwa kama vile njaa, umasikini na magonjwa yaliyosheheni pakubwa barani. Bila shaka, hili ni suala linalosawisishwa na 'kinyume mbele'. Maharamia wanatishia utangamano wa kimataifa wanapotibua usafiri na shehena zinazoelekezwa sehemu tofauti ulimwenguni.

Matumizi ya kidiplomasia na mashauriano hayaelekei kuzalisha matunda katika juhudi za kudhibiti uharamia. Zaidi ya hayo, matumizi ya nguvu yahusishayo mashambulizi pamoja na maharamia kufunguliwa mashtaka nchini Kenya na Ufaraansa kunaelekea kuzipiga jeki juhudi za uharamia ulimwenguni. Aidha, utawala wan chi kunachipuka uharamia haujajizatiti kuharamisha doa hili linalotisha ustawi wa kimataifa.

Mathalan, ni jambo lisilopingika inapobainika kuwa uharamia umedumaza biashara ya kimataifa, hali inayochangia upungufu wa ucheleweshaji wa bidhaa muhimu zinazoendeleza ustawi wa uchumi.
Dosari hii inaelekea kukwamiza mojawapo wa malengo ya maendeleo ya millennia yanayosisitiza uimarishaji na ushirikiano wa maendeleo na upanuzi wa masoko ulimwenguni. Harakati za kitalii katika kanda mashariki ya

bara la Afrika zimehujumiwa. Ni muhali kwa utali kustawi kwenye maeneo yaliyo na tishio la usalama. Itakumbukwa bayana kwamba watalii hawasafiri tu kwa ndege bali hata kwa meli.

Jitihada za kuweka laini za mawasiliano chini ya bahari ili kurahisisha na kupunguza gharama za mtandao ulimwenguni ni ndoto ambayo haijatimia hadi hivi sasa, kufuatia juhudi za maharamia katika bahari ya Hindi. Kwa mujibu wa hali hii, mawasiliano mepesi na nafuu yasitarajiwe hivi karibuni. Licha ya hayo, shughuli za uvuvi na biashara nyinginezo kwenye kanda ya mmwambao zimetiliwa shaka si haba.

Itabidi mikakati kabambe na suluhisho la kudumu liweze kupatikana ili vitendo vya uharamia viweze kusitishwa.

**Maswali**

**a)** Fupisha aya mbili za kwanza kwa maneno 70. (alama 8,1 ya mtiririko)

**b)** Onyesha jinsi ambavyo Kenya imeathiriwa na uharamia na namna hali hii inatia hofu. Maneno 60. (alama 7,1 ya mtiririko)

**<u>SEHEMU YA SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)</u>**

**(a)Taja sauti zenye sifa zifuatazo. (alama 2)**

(i) King'ong'o cha mdomo:-------------------------------------------------------------------------------------------

(ii) Irabu ya mbele kati

(iii) Kipasuo ghuna cha kaakaa laini

(iv) Kikwamizo sighuna cha menoni

**(b) Dhihirisha miundo ya silabi katika maneno yafuatayo. (alama 2)**

(i) itwa:

(ii) Mchwa:

**© Tunga sentensi mbili ili kuonyesha matumizi ya kiakifishi (alama 2)**

Vifungo

**(d) Andika sentensi ukitumia: (alama 2)**

(i)Kihusishi cha ulinganisho

(ii)Kihisishi cha furaha

**(e) Tunga sentensi ya neno moja iliyo na muundo ufuataao.(alama 2)**

(i)Nafsi

(ii)Mzizi

(iii)kauli

(iv)Kirejeshi

**(f)Eleza matumizi ya maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo. (alama 2)**

(i)Chakula <u>chochote</u> kitaliwa na watoto.

(ii) Chakula <u>chote</u> kitaliwa na watoto.

**(g) Kwa kutunga sentensi mwafaka onyesha aina tatu za yambwa. (alama 3)**

**(h)Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika usemi wa taarifa.(alama 3)**

“Tutamtia mbaroni mhalifu huyo sasa hivi” Askari akasema.

**(i)Ainisha matumizi ya kiambishi “ji” katika sentensi (alama 3)**

Jibwa hilo liliweza kujinusuru kutokana na hasira za mkimbiaji.

**(j) Changanua kwa Jedwali. (alama 4)**

Otii ambaye hucheza mpira ni kijana mkali.

(k)Tofautisha vitate vifuatavyo kwa kuvitungia sentensi moja. (alama 2

(i)Hawara

(ii) Hawala

(L) Bumba ni kwa nyuki-------------------------------------------------------------ni kwa samaki na-----------------------------ni kwa siafu. (alama 2

**(m) Andika methali inayojumuisha ujumbe ufuatao.(alama 1)**

Hata mtaalamu huhitaji kutafuta msaada wa wataalamu wenzake.

**(n) Unda kitenzi kutokana na nomino zifuatazo. (alama 2)**

(i)Aina

ii)Moto

**(O)Onyesha matumizi ya ‘<u>kwa’</u> katika sentensi. (alama 2)**

(i)Kwao kunawaka moto.

(ii) Magaidi walitoroka kwa kasi.

**(P) Nyambua katika kauli kwenye mabano. (alama 2)**

(i)Tua (tendama)

(ii) Pwa (tendeka)

**(q) Badilisha sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu. (alama 2)**

Mama huwapikia watoto chakula.

**(r) Tumia neno ‘kesho’ kutungia sentensi kama: (alama 2)**

(i)Nomino:

(ii) kielezi:

**<u>SEHEMU D: ISIMUJAMII (ALAMA 10)</u>**

Lugha ya magazeti husheheni upekee wa aina fulani. Eleza sifa za lugha hii kisha ueleze upekee huu hukusudia nini?

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(Kcse)*

**MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025**

**JINA: ……………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ……DARASA: …............**

# SHULE YA UPILI YA KISII

**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**
**MAAGIZO**
**Maagizo**

***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

***b)*** *Jibu maswali yote.*

***c)*** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*

***d)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. UFAHAMU | 15 | |
| 2. UFUPISHO | 15 | |
| 3. SARUFI | 40 | |
| 4. ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

**ULEVI**

Ilikuwa Jumamosi ya mwisho wa mwezi, wakati wa magharibi, nikiwa kwenye tembeatembea zangu za kupunga hewa. Nikaona kilee, kijitu si kijitu, mtu si mtu. Kinakuja kwa kuyumba huku na huku kama kwamba kikiendeshwa na upepo.

Kukaribiana nacho, nikaweza kukiona vizuri zaidi. Kilikuwa kirefu, lakini kilichokonda na kukondeana mithili ya kiuno cha nyigu. Shati kiliyovaa ilionekana kama kwamba imetundikwa tu kijitini. Kukikazia macho, nilitambua. Maskini! Mwili wake ulidhoofika na kuwa kitu kama vile mfuko tu wa mifupa.Kufumba na kufumbua, kilianguka bwup! Chini. Nikajikuta nakitikisa kichwa.

"Vipi Mlachake bwana we?" Nikamtupia, huku nikijaribu kumsaidia ainuke.

"Vi-vi-vipi ni-nini?" Akanirudia.

"Umerudia he?"

" La-lakini kwa pe-pesa zangu, si-si-siyo kwa-kwa-kwa kudoea."

"Daktari alikushauri vipi?

"A-ach-ch-chana naye yeye hu-huyo. Ati nina-naji-jipunguzia maisha.Kwa ni-ni-nani ha-hata-ta-kufa?"

Kuzidi kumyanyua ili nimwinue kutoka chini, akatitazama kwa macho yake malegevu na kuniuliza, "Ha-hata wewe pia una-na-nataka kuniibia?"

"Nani amekuibia?" Nikamwuliza kwa mshangao. Kimya. Aliweza kuinuka na kubaki akiyumbayumba mfano wa mcheza rumba. Kisha yakamtoka matusi mfululizo.

"Mlachake!" Ikanitoka sauti ya mshangao baada ya kushuhudia yale niliyoyatia machoni.

"Ni aibu gani hii ya kujitapikia ovyo?"

"Ni me-jiji-jitapikia ni-ndiyo. Sikumta-tapikia mtu."

"Sikiza Mlachake bwana."

"Ndi-ndiyo bwana m-mkubwa," akasema na kunipigia saluti. Kisha, kwa mara nyingine tena, huyoo akasalimu amri.

"Mlachake! Pesa, ulizifanyia, kazi mwezi mzima ili zije kukutesa namna hii he?"

"Ndi-ndiyo. Cha m-m-mgema hu-uliwa na mle-levi si-si ndiyo?"

Kwa mara nyingine tena, nilijikuta natikisa kichwa. Papo hapo, akili ikanipa kuwa nimsaidie kwa kumfikisha nyumbani kwake.

Kufika mlangoni tu, alipaaza sauti akisema, “Fungua!” Ilhali mlango ulikuwa umekomewa kutoka nje. Kisha dwa!Akaupiga teke, halafu “Huuwi!” akapiga nduru huku akishika mguu na kutandwa na wingu jeusi usoni. “Nita-ta-charaza mtu le-le leo mimi,” akatisha. Akichutama na kubwagizika chini mfano wa gunia tupu. Nikatikisa kichwa na kujiendea zangu.

**Maswali**

a) Taja sababu mbili za Mlachake kuonekana akiyumbayumba. (Al 2)

b) Mbali na kumletea mtu aibu kama vile ya kujitapikia ovyo, taja athari au hasara nyingine tatu za ulevi kwa mlevi (Al 3)

c) Mwandishi anasema, “Kwa mara nyingine tena huyoo, akasalimu amri.” Anamaanisha nini hasa kwa kusema “akasalimu amri?” (Al 1)

d) Ni aina gani mbili za ushihidi zinazotudokezea kuwa Mlachake hakuishi pekee nyumbani kwake? (Al 2)

e) i) Ni methali gani iliyomjia Mlachake kichwani wakati alipozungumza na msimulizi wa makala hii? (Al 1)

ii) Eleza jinsi methali hiyo inavyoingiliana na maudhui ya makala hii. (Al 2)

f) Eleza matumizi yafuatayo ya lugha kama yanavyojitokeza katika makala uliyosoma. (Al 4)

i) Wakati wa magharibi

ii) Kukutesa

iii) Kudoea

iv) Akili ikanipa

**2. UFUPISHO (ALAMA 15)**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Tangu kuripotiwa kwa maambukizi na vifo kutokana na Tandavu la Korona nchini Kenya, Wakenya wengi wamekuwa wakiishi kwa hofu. Vifo vinavyohusishwa na ugonjwa huu hatari vimekuwa vikiongezeka kila kukicha. Ugonjwa huu sugu unawafisha watu kwa muda mfupi baada ya kuambukizwa. Kutokuwepo kwa dawa za kutibu ugonjwa wenyewe kunaongeza wasiwasi miongoni mwa wanajamii. Nchi ya Kenya kama ilivyo mataifa mengine ulimwenguni imehimiza raia wake kupata chanjo dhidi ya tandavu hili. Hata hivyo, hatua ya serikali kutumia vitisho ili kuwashinikiza watumishi wa umma kupata chanjo ya korona haifai kwani huenda ikatatiza mpango wa kuchanja watu milioni kumi mwaka huu. Licha ya serikali kujaribu kuwalazimisha watumishi wa umma bado chanjo haijakubalika na wengi nchini. Kutokubaliwa kwa chanjo hii kumesababishwa na ukosefu wa elimu ya kutosha kuihusu. Watu wengi wanahofia kuwa huenda waliochanjwa wakapata madhara baadaye.

Mamilioni ya watu wameathiriwa kwa njia moja au nyingine na ugonjwa huu. Kenya imeshuhudia hoteli nyingi za kifahari kufungwa. Hii imetokana na usafiri wa ndege kusitishwa kote duniani. Kutokana na hali hiyo, hoteli zilizotegemea wateja watalii zilisimamisha shughuli zake kwa muda. Kwa mfano, ya *Intercontinental* ilifunga milango yake kabisa mwaka wa 2020. Jambo hili liliwafanya watu wengi kupoteza ajira.

Usafiri wa umma umekumbwa na changamoto si haba kutokana na tandavu la korona. Serikali ilipunguza wasafiri katika magari ya abiria kwa thuluthi moja. Wasafiri hao walilazimika kulipa nauli maradufu kwa safari ile ile. Watu wengi walilazimika kufutilia mbali mipango yao ya usafiri. Kafyu vile vile iliathiri usafiri huu wa umma. Magari mengi yalilazimika kusitisha safari njiani kwa kupatikana na kafyu. Wafanyabiashara katika sekta ya matatu wanahesabu hasara kubwa kwa kukosa abiria. Wengine wamelazimika kuuza magari yao kwa kutamaushwa na changamoto iliyowakumba ghafla.

Aidha, shule zililazimika kufungwa mnamo Machi 2020. Wanafunzi walikaa nyumbani hadi Januari 2021. Hii iliharibu kalenda ya masomo nchini. Serikali ilijaribu kuwasihi walimu kufunza mtandaoni lakini hii haikufaulu hata. Wanafunzi wa kike kadhaa waliishia kupata ujauzito hivyo basi kukatiza masomo yao. Ibada zote pia zilisitishwa. Nao waumini hawakusazwa. Baada ya serikali kufunga makanisa, misikiti na vyumba vingine vya ibada, waumini wengi walilazimika kufuatilia ibada zao katika runinga au mtandaoni. Waliokosa mitandao waliomba na jamaa zao na wengine kupuuza ibada hizo kwa muda.

Shida zilizindikana ugonjwa wenyewe ulipozidi kuenea. Hospitali za umma zililemewa na idadi ya wagonjwa waliokuwa wakienda kule kutafuta matibabu. Vitanda vilijaa na hata wengine wakalala chini katika wadi mbalimbali. Huduma za afya zikazidi kudidimia kutokana na ukosefu wa wahudumu wa afya na vifaa vya kutumiwa na wagonjwa. Vifo vingi vikaripotiwa katika hospitali hizi za umma. Kila sehemu nchini ikaathirika. Majonzi yakajaa kila mahali.

Licha ya haya mabaya yote yaliyokuja na ugonjwa huu wa corona, kuna wale waliochuma riziki kwa kuzuka kwa ugonjwa huu. Mambo mapya yalijitokeza katika ulimwengu wetu. Msamiati wa lugha ukaongezeka. Hii ilitokana na haja ya kuwepo kwa istilahi au misamiati ya kufafanua hali mpya iliyoibuliwa na tandavu hili. Vilevile Kutokana na watu kulazimika kufanya kazi nyumbani, ujuzi wa matumizi ya mtandao umeimarika. Kwa mfano, ufundishaji mtandaoni umefaidi vyuo vingi vinavyofundisha masomo ya mbali.

Wanabiashara wengine wakaanza kuuza barakoa. Barakoa ilikuwa kitu kigeni huku kwetu na duniani kwa jumla. Wengi walipata faida kubwa sana kwa kuwa soko la barakoa lilikuwa pana. Hata hivyo,

barakoa zinazotumika na wananchi wengi hazijathibitishwa kuwa bora kuzuia korona. Hali hiyo inawafanya watumiaji wake kuwa na usalama wa bandia kwani wanaweza kuambukizwa ugonjwa wa korona kwa urahisi licha ya kuwa wamevalia barakoa hizo.

Kadhalika, viyeyushi vikaanza kutumika kwa wingi humu nchini na duniani kote. Wachuuzi wengi waliingia biashara hii na kufaidika kiasi. Wengi hawakujua viyeyushi ni nini kabla ya wakati huo. Hivi sasa hata watoto wadogo wanajua viyeyushi na kutumia kwa njia mwafaka.

Kundi lingine lililonawiri kwa korona ni hospitali za kibinafsi. Wengi wa matajiri walioambukizwa ugonjwa huu walijipeleka hospitali hizi kwa matibabu. Wenye hospitali hizo nao wakapandisha bei ya matibabu kwao. Ikawa ni biashara inayonoga kabisa. Hawakujali kuhusu wale wasio na pesa.

Korona imefanikisha juhudi za maafisa wa afya kuhimiza usafi kila mara. Hii ni kwa sababu watu wanalazimika kunawa mikono yao kila mara. Usafi huu wa mikono unapunguza visa vya magonjwa kama vile kipindupindu katika jamii. Aidha, gharama za sherehe zimepungua mno kutokana na sheria za kudhibiti idadi ya watu wanaohudhuria sherehe za mazishi au matanga. Hali hii ni nafuu kwa wale wachochole ambao wakati mwingine hulazimika kuuza kidogo walicho nacho ili kugharamia sherehe za matanga au arusi

**Maswali**

a) Kwa kuzingatia aya tano za kwanza, eleza shida zilizoletwa na korona. (Maneno 100) (Al 9)

b) Fupisha aya nne za mwisho kwa maneno 60. (Al 6)

**3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) Andika neno lenye muundo ufuatao wa sauti: (Al 2)
Kipua cha kaakaa laini, irabu ya kati tandazwa, kipasuo sighuna cha ufizi, irabu ya chini tandazwa

b) Eleza maana ya silabi. (Al 1)

c) Tambua muundo wa silabi katika neno MAKTABA. (Al 1)

d) Ainisha vipengele vilivyopigiwa mstari: (Al 2)

i) Genge <u>la</u> wezi limetiwa mbaroni....................................................................

ii) Genge <u>la wezi</u> limetiwa mbaroni....................................................................

e) Tunga sentensi moja ukitumia neno hili ili litumike ulivyoelekezwa mabanoni. (Al 2)
Enzi (nomino na kitenzi)

f) Eleza maana mbili ya sentensi hii: (Al 2)
Watu wa pwani hawaogopi bahari kama watu wa bara.

g) Taja matumizi matatu ya kiambishi ‘i’ na utolee mifano: (Al 3)

h) Ainisha mofimu za neno: Kitandani (Al 3)

i) Tunga sentensi moja ukitumia wakati ujao hali ya kuendelea. (Al 2)

j) Katika sentensi moja, tumia **papa** na **bapa** ili kudhihirisha maana ya kila neno. (Al 2)

k) Changanua kwa vishale: Wale wageni wetu watakuwa wamewasili leo jioni. (Al 4)

l) Amrisha katika nafsi ya pili wingi: **La**....................................................... (Al 2)

m) Yakinisha katika umoja: Msingalisoma nyakati zile msingalipata zawadi kemkem. (Al 1)

n) Tambua kauli iliyotumika: Ametwikwa jukumu la kuwalea yatima wale. (Al 1)

o) Bainisha yambwa na chagizo katika sentensi inayofuata. (Al 2)

Vibarua wamefanya kazi hiyo haraka ipasavyo.

p) Akifisha: (Al 2)

   i) Hako katoto kalipoletwa kila mtu alikahurumia

   ii) Jama ni kweli umemkosea mzazi wako heshima?

q) Andika katika usemi wa taarifa. (Al 3)

"Ninataka kuanza kupendekeza majina ya watakaosafiri sasa", Afisa alisema.

r) Vishazi tegemezi vina uamilifu gani? Taja kwa hoja mbili na utungie sentensi. (Al 2)

s) Andika kisawe cha: enda arijojo (Al 1)

t) Andika kinyume: Ajitahidiye husifiwa kwa bidii yake na hupandishwa madaraka. (Al 2)

**4. ISIMUJAMII (ALAMA 10)**

a) Eleza majukumu matano ya Kiswahili kama lugha ya kitaifa (Al 5)

b) Eleza changamoto tano zinazokabili lugha ya Kiswahili kama somo katika shule za upili nchini Kenya (Al 5)

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(Kcse)*

**MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025**

**JINA: ……………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ……DARASA: …............**

# SHULE YA UPILI YA KENYA HIGH

**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**
**MAAGIZO**
**Maagizo**

- ***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
- ***b)*** *Jibu maswali yote.*
- ***c)*** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*
- ***d)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. UFAHAMU | 15 | |
| 2. UFUPISHO | 15 | |
| 3. SARUFI | 40 | |
| 4. ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

1. **UFAHAMU ( Alama 15)**

*soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

"Yakobo, eti babu yako ndiye mnyama? Siamini na sitaamini maneno hayo."

"Uliuomba ukweli."

"Kwa nini hukuniambia mambo haya zamani, Yakobo? Kwa nini mama yako hakunifunulia? Kwa nini aliisoma barua hii akaificha?"

"Yote hayo yalifanywa ili uwe na maisha bora. Ulipata wazazi wema waliokulea na kukutunza. Ulipelekwa shuleni, Chaanasa, mimi sikukanyaga shuleni. Ikiwa ungeachwa kinyongo, huenda hungekuwa na maendeleo uliyo nayo. Labda ungeingilia maisha mabaya na kuwa mtu bure kabisa. Zipo siri zinazowekwa ili kuwalinda watu."

Lakini, Yakobo, inaniuma sana. Miaka yote hii tumetembea pamoja, tumekuwa tukitembeleana, tumekula meza moja, tumefanya mambo mengi pamoja wala huniambii mimi ni mjomba wako."

Naomba msamaha, kwa moyo wangu wote, kwa kukosa kueleza mambo hayo mapema. Hata hivyo, ni vizuri kuona mambo kwa njia nyingi, si mtazamo mmoja tu. Tuseme, ningekuambia mambo hayo mapema, je, ungekuwa na furaha zaidi? Huenda jitihada zako za kumtafuta baba yako zingekutia chuki. Pengine hata ungetamani kulipiza kisasi kwa dhiki alizokuletea ukafungwa jela au hata kuhukumiwa kifo. Wakati mwingine, ni salama kutojua. Jambo usilolijua halikunyimi usingizi. Hata hivyo, naomba radhi kwa kutokuambia. Ukweli wa mambo ni kwamba hata Mzee Johari muungwana, yaani, babu yangu, au baba yako, hakujua mambo haya yote. Alikufa bila kujua sura au jina la mtoto wake: Chaanasa."

Bwana Chaanasa, bila kujua, alilia na kudondokwa na machozi kupukupu. Nikaona aibu kubaki hapo, lakini sikuondoka. Nilitaka kusikia hatima ya mazungumzo hayo.

"Yakobo, mpwa wangu," Bwana Chaanasa aliita huku akilia. Akanyoosha mikono yake na kumkumbatia Yakobo.

"Nimekusamehe. Nimekusamehe. Lazima nitekeleze ombi la mamangu. Alinisihi nisiwe na chuki na mtu yeyote. Siwezi kukuchukia mpwa wangu. Naahidi sitakuchukia kamwe. Asante kwa kuniambia ukweli wote. Asante pia kwa hekima yako kwani pia ulingoja hadi wakati unaofaa kunifunulia mambo haya. Ungaliyafunua zamani, kama ulivyosema awali, huenda nisingaliitikia jinsi nilivyofanya leo. Huenda mambo yangekuwa mabaya. Labda ningelipuka kwa hasira na kusababisha hasara, pengine hasara isiyolipika. Sasa ninaelewa kwa nini tunalandana sana nawe, na mzee Busara. Sisi ni wa damu moja. Baba yangu angalikuwa hai, ningalienda nikamwone na kujitambulisha kwake. Ningalimwita 'baba' na huenda angaliniita 'mwanangu.' Ningalimsamehe kwa kumwacha mamangu na kunitelekeza."

"Bado unaweza kumsamehe."

"Jinsi gani?" Bwana Chaanasa akauliza.

"Kwa kusahau yaliyopita na kuganga yajayo. Yazike mambo yote hayo katika kaburi la sahau. Acha ya kale yawe ya kale, ya nyuma yawe ya nyuma, ya zamani yawe ya zamani. Kilichotendeka kimekwishatendeka. Yaliyofanyika yamefanyika. Yamemwagika na hayatazoleka kamwe hata kwa kuchimbua ardhi. Lililopita limepita, si uwele tena.

"Naam, Bwana Chaanasa, lipitalo hupishwa."

(a) Eleza sababu za Chaanasa kufichwa taarifa kuhusu babake. (Alama 2)

(b) Thibitisha kuwa babu yake Yakobo alikuwa mnyama. (Alama 2)

(c) Eleza umuhimu wa maswali balagha katika kifungu hiki. (Alama 2)

(d) Je, ni kweli kuwa kama si kuweka siri mambo yangemharibikia Chaanasa? Tetea jibu lako. (Alama 3)

(e) Ni jambo lipi lililomfanya Chaanasa kumsamehe mpwa wake? (Alama 2)

(f) Kwa mujibu wa kifungu, kusamehe kuna matokeo gani? (Alama 2)

(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu. (Alama2)

(i) hayatazoleka

(ii) tunalandana

**2. UFUPISHO ( Alama 15)**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*

Maadili ni desturi, utamaduni au hulkaa mbazo hubainisha na kulipa kundi fulani la watu upekee wake. Maadili ni muhimu katika kuonesha imani na kanuni za maisha ambazo kundi Fulani la watu huchukulia kuwa chanya na zile wanazozichukulia kuwa hasi. Maadili ndio mwongozo unaothibiti matendo na hulka za kila mmoja.

Kila jamii huwa na maadili yake ambayo yanamhitaji kila mwanajamii kutenda na kuishi kama jamii inavyotarajia. Pia, yaliweza kulegeza mielekeo au mitazamo yao. Hata leo, maadili hutusaidia kubainisha sisini akina nani, mtazamo wetu maishani, pamojana matarajio yetu.

Katika Katiba ya Kenya, maadili ya jamii ya Wakenyayameangaziwavyema. Kwanza, ni wazi kuwa Kenya ni taifa la wacha Mungu, kwa hivyo, kila Mkenyaanatarajiwa kuabudu na kumheshimu Mwenyezi Mungu. Hili limeshadidiwa hata katika wimbo wetu wa taifa. Pamola na hayo, katika kuimarisha umoja wa kitaifa, tofauti zetuWakenya kirangi, kikabila, kitabakana hata kidini hazipaswi kutugawanya.Maadili yanatuhimiza kuzichukulia hizo kuwa sifa za kipekee na kuzionea fahari. Ule utaifa wetu kama wakenya unapaswa kuwekwa mbele daima ili kuzima juhudi zozote za kututenganisha kwa misingi hiyo.

Kama taifa, tunahitaji kudumisha uzalendo wetu kwa kujitolea kuhakikisha kuwa mahasidi hawaporomoshi maadili ya jamii zetukwa kuiga hulka zao potovu. Uzalendo unatuhumiza kuripoti vitendo vyote vya kuihujumu nci au watu wake kwa asasi za dola. Asasi hizo zitachunguza na kuzima

utekelezaji wa uhalifu kabla haujatikea, na iwapo utakuwa umetokea, asasi hizo zitawapa adhabu wahalifu ili waweze kubadili mienendo mibaya na kuwa kielelezo kwa wengine wenye nia mbaya.

Maadili, vilevile, humwongoza mtu kuhusu namna za kutatua mizozo na kudumisha amani. Hatuwezi tukajivunia uhuru pasi na kuwepo amani. Amani ndio msingi wa umoja, ustawi na maendeleo ya taifa lolote. Ukosefu wa amani hudumaza na hata kurudisha nyuma maendeleo kwa kuwahini watu nafasi za kushiriki uzalishaji mali. Ukosefu wa amani vilevile husababisha kuongezeka kwa visa vya uhalifu kama vile mauaji, kulememazwa kwa watu, unajisi, uharibifu wa mali na kusambaratika kwa familia, hali ambayo huchangia mporomoko wa maadili katika jamii.

Uadilifu unakwenda kinyume na methali, amani haiji ila kwa ncha ya upanga. Ukweli ni kwamba, tunaweza kusuluhisha tofauti zetu bila kutumia silaha. Matumizi ya silaha aghalabu huzidisha uhasama na kuchochea haja ya kulipiza kisasi. Njia pekee ya kutatua migogoro ni kuelewa chanzo cha migogoro yenyewe, wahusika kufanya kikao na kuizungumzia kwa uwazi na kwa utulivu. Pande zote husika zinafaa kukubali makosa au madhara yaliyotokana na matendo yao na kuomba msamaha ili kupata maridhiano. Kuomba msamaha kusidhaniwe kuwa kujishusha hadhi, bali ni unyenyekevu katika kutatua tofauti kwa manufaa ya muamala wa vizazi vijavyo. Anayeombwa msamaha naye anapaswa kuwa tayari kutoa shifaa kwa dhati na kusahau kosa alilofanyiwa. Yote haya yakishindikana, mgogoro wapaswa kupelekwa mahakamani. Haki za kila mmoja zimelindwa katika katiba yetu na mahakama zipo ili kutetea haki hizi bila kupendelea upande wowote.

Utiifu wa sheria vilevile ni njia mojawapo ya kukuza maadili ya kijamii. Kwa kuwa sheria hulinda haki za kila mtu; wake kwa waume, wakubwa kwa wadogo, kila mmoja ana wajibu wa kuheshimu sheria. Hii ni pamoja na kulinda rasilimali zetu kama jambo la wajibu bila ya kutegemea kuwepe wadumisha sheria. Uongozi wa kisheria huwapa watu hakikisho kuwa maisha yao hayatakuwa kama ya mahayawani nyikani bali yatafuata utaratibu Fulani. Hivyo basi, sheria ni hakikisho la jamii inayolinda haki na kuendesha mambo yake kwa uwazi, haki na ushwari.

Bila shaka, tukizingatia na kuimarisha maadili, taifa letu litakuwa jamii bora na kivutio cha kila mtu. Kiu ya Wakenya ya kutaka kuhamia nchi nyingine, hasa zilizostawi, itapungua. Wote watakuwa na ari ya kuliendeleza taifa lao.

MASWALI

a) Eleza umuhimu wa maadili kwa jamii na taifa kwa ujumla. (maneno 60-70) ( alama 7 , 1 ya utiririko)
b) Fafanua jinsi mizozo inaweza kutatuliwa kwa uadilifu. (Maneno 75-80) (alama 8, 1 ya utiririko)

**3. MATUMIZI YA LUGHA ( Alama 40)**

(a) (i) Kwa kutoa mfano mwafaka, fafanua dhana ya kiambishi. (Alama 2)

(ii) Eleza dhima ya viambishi katika neno lifuatalo. (Alama 3)

lililolilia

(b) Andika neno lenye muundo wa IKKKI. (Alama 1)

(c) Tambua na ueleze aina za vivumishi katika sentensi zifuatazo.

(i) Mwanagenzi mwenyewe aliimba wimbo vizuri. (Alama 1)

(ii) Vyakula vyetu vina ladha nzuri sana. (Alama 2)

(d) Andika vitamkwa vyenye sifa zifuatazo: (Alama 2)

(i) Kikwamizo cha meno hafifu

(ii) Kikwamizo cha kaa kaa gumu

(iii) Irabu ya chini kati

(iv) Nazali ya kaa kaa laini

(e) Andika sentensi ifuatayo katika hali tegemezi. (Alama 1)

Watakapokuwa wakicheza kandanda tutakuwa tumelala fo fo fo.

(f) Onyesha ngeli za maneno haya. (Alama 2)

(i) nyavu

(ii) wizani

(iii) miadi

(iv) mwalishi

(g) Mbali na kuorodhesha, onyesha matumizi mengine mawili ya koloni. (Alama 2)

(h) Ainisha shamirisho na chagizo katika sentensi. (Alama 2)

Wapishi wameandika meza haraka ipasavyo.

(i) Andika sentensi moja ili kuonyesha maana mbili za neno **ila.** **(**Alama 2)

(j) Andika sentensi ukitumia vitenzi vitokanavyo na nomino zifuatazo. (Alama 2)

(i) hofu

(ii) somo

(k) Andika sentensi yenye kishazi tegemezi vumishi cha wakati ujao. (Alama 2)

(l) Pigia mstari kihusishi na uonyeshe kinaashiria nini? (Alama 2)

(i) Mwalimu amesimama karibu na mlango.

(ii) Mzee anapoketi huona mbali kuliko kijana anaposimama.

(m) Changanua sentensi ifuatayo kwa mtindo wa matawi. (Alama 3)

Mbuzi na kuku walikuwa wakiuzwa sokoni.

(n) Badilisha katika kauli ya ketendua. (Alama 2)

Tulitundika picha hiyo na kuyabandika maandishi ukutani.

(o) Ainisha maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi hii. (Alama 2)

Yeyote atakayefika katika mkutano wa chifu atakaribishwa vizuri.

(p) Andika katika usemi wa taarifa. (Alama 2)

"Ziara ya Rais wetu itakamilika kesho alasiri." Msemaji wa ikulu alimwambia mtangazaji.

(q) Andika sentensi moja ukitumia kihisishi cha kuridhia. (Alama 1)

(r) Onyesha tofauti za kimaana za neno **zuka** na **suka** katika sentensi moja. (Alama 2)

(s) Geuza katika ukubwa. (Alama 2)

Ng'ombe walivunjika miguu yao

(t) Tunasema kishazi cha samaki , __________________ wa samaki au ____________________ ya samaki (Alama 1)

**4. ISIMUJAMII (Alama 10)**

(a) Kwa kutoa mifano mwafaka eleza visababishi vitano vya kuchanganya ndimi. (Alama 5)

(b) Kiswahili ni **lingua franka.** Thibitisha kwa mifano madhubuti. (Alama 5)

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

*Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya(Kcse)*

**MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025**

**JINA: ……………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ……DARASA: …............**

# SHULE YA UPILI YA NAIROBI

**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**
<u>MAAGIZO</u>
**Maagizo**

- ***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
- ***b)*** *Jibu maswali yote.*
- ***c)*** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*
- ***d)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**<u>KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE</u>**

| **SWALI** | **UPEO** | **ALAMA** |
|---|---|---|
| 1. UFAHAMU | 15 | |
| 2. UFUPISHO | 15 | |
| 3. SARUFI | 40 | |
| 4. ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**1. UFAHAMU** (Alama 15)

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali**

Wanawake ndio wanaonyanyasika zaidi katika vyombo vya usafiri hasa kwenye mabasi na matatu. Kwa kiasi fulani, kunyanyasika huku hutokana na maumbile, mavazi, watoto na mizigo mbalimbali wanayoibeba. Kwa upande mwingine utakuta kwamba, wafanyakazi karibu wote katika matatu na mabasi ni wanaume na shughuli zao wanaziendesha kama wanaume na sio vinginevyo.

Wanaume hawa huendesha mambo zaidi kwa kumjali na kumtetemekea mwanamme na sio mwanamke. Mwanamke anashughulikiwa tofauti iwapo tu yeye mwenyewe ndiye mwenye mali hiyo, ni ya jamaa yake au mpenzi wa wafanyakazi katika matatu hizo. Hali ya vyombo vya usafiri inavyoonekana pia ni kuwa vimeandaliwa zaidi katika kumjali mwanamme na siyo mwanamke au watu wenye tofauti au upungufu fulani mwilini.

Iwe ni tabia ya utingo au ya madereva au ni hali halisi ya vyombo vilivyoundwa, yote haya ni mambo yanayoweza kubadilishwa endapo tu wanawake watakuwa na sauti moja na kusimama kidete katika kupigania na kutetea kile wanachostahili kukipata katika huduma za usafiri na uchukuzi mijini na nchi nzima kwa ujumla.

Kama ilivyotajwa hapo juu, kuna tofauti za kimsingi kati ya wanaume na wanawake. Katika jamii inayomjali kila mtu, ni muhimu kwa tofauti hizo kuzingatiwa ili kuhakikisha kuwa kila mwanajamii anapata huduma anayohitaji kwa amani na usalama na bila usumbufu kwake au kwa wale wanaomtegemea. Pamoja na matatizo yote wanayopata wanawake, hakuna chombo kilichojizatiti kutoa sauti ya umoja na kusema kwamba hili au hiki kinachofanyika siyo sawa au siyo haki kwa mwanamke.

Wakati umefika sasa kwa wanawake wenyewe kujiunga pamoja, kuelimishana na kuanza kupigania haki zao ili wasiendelee kunyanyasika katika vyombo vya usafiri. Ninatoa mifano michache. Wale wanaokwenda safari ndefu wanajua fika adha wanayopata wanawake wakati basi limesimama peupe watu wanatakiwa "wakachimbe dawa." Kwa mwanamme si kazi. Lakini kwa mwanamke kuna shida,tena siyo kidogo. Je, kwa nini wanawake waendelee kuvumilia haya? Kuna ugumu gani kwa kila basi ya safari ndefu kuwa na choo ndani? Wenye dini zinazodai tohara nao wanasemaje?

Shida nyingine ni katika kupanda magari haya. Kwenye matatu, ni rahisi (ingawa hatari) kwa mwanamme kupanda gari huku likiwa kwenye mwendo, lakini je, dereva wa matatu anastahili kufanya hivyo kwa mwanamke? Upande wa mizigo hasa kwa wafanyabiashara ni adha tupu kwa wote. Je, nini kifanyike ili kila mtu aweze kufanya biashara yake kwa ustaarabu zaidi? Ni kama kwamba wanawake wamekubali kunyanyaswa kwao ni sehemu ya maisha. Hivi sivyo inavyostahili kuwa. Sote tuna haki sawa kwenye kila aina ya chombo cha usafiri. Tatizo ni pale tunapokubali kugeuzwa mizigo na kubebwa jinsi mbebaji anavyotaka kutubeba. Kama wanawake wana sauti ya pamoja kuhusu maswala haya, nina hakika kuwa tutaanza kuona mabadiliko katika mabasi na matatu zetu.

Muda wa wanawake kuonekana kuwa ni "washamba" na watu wanaoweza kudanganywa kuwa gari lina viti vya kulala nalo kumbe limejaa tele na bado mtu akapanda umekwisha pita. Huduma yoyote lazima iwe na

hadhi ya namna fulani. Na wanaoamua ni hadhi gani huduma hiyo iwe sio wenye basi au matatu bali abiria, maana nauli anayolipa ni kura inayotakiwa kumwezesha kuchagua kilicho bora na sio kilicho duni.

Ni vyema kuelewa kuwa ni wanawake na sio wanaume waliochangia zaidi kumaliza ubaguzi wa rangi huko Marekani na Afrika Kusini. Wanawake kwa sababu wanafikiriwa kimakosa kuwa legelege ilidhaniwa wasingekubali kususia mabasi na kutembea kwa miguu kama mbinu ya kugomea mfumo uliokuwepo nyakati hizo huko Atlanta na Johannesburg. Hata hivyo, wanawake hao waliyagomea mabasi hayo kwa roho moja na kutembea, wakati mwingine hata masafa ya kilomita ishirini kwa miguu kila siku. Wenye mabasi na serikali wakaonja makali ya mgomo huu na huo ukawa mwanzo wa mabadiliko yaliyosababisha kuzuka kwa siasa zisizovumilia ubaguzi wa rangi katika usafiri na hatimaye katika mustakabali mzima kitaifa. Wanawake wa nchi yetu nao wakitaka wanaweza pia kuanzisha vuguvugu litakalosaidia usafiri na uchukuzi nchini kuwa wa heshima, kistaarabu na unaowajali wanawake, wazee na watoto.

**Maswali**

a) Kwa kurejelea kifungu, fafanua namna tatu mwanamke anavyodhalilishwa.(alama 3)

b) Kuna nyakati mwanamke anajipata katika hali nafuu kidogo katika usafiri. Eleza. (alama 1)

c) Ili kujikomboa na madhila anayokumbana nayo, mwanamke anastahili afanye nini?(alama 4)

d) Eleza juhudi zilizofanywa na mwanamke kwingine kupambana na dhuluma katika jamii yake. (alama 1)

e) Mwandishi wa kifungu hiki anapendekeza nini kuhusu namna huduma kwa umma zinafaa kutekelezwa. (alama 4)

f) Eleza maana ya mafungu yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu hiki. (alama 2)

(i) katika mustakabali mzima wa taifa

(ii) wanatakiwa wakachimbe dawa

**2. UFUPISHO (ALAMA 15)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Kwa hali nyingine, tunaweza kusema kuwa uchafuzi wa mazingira ni uharibifu wa vilevitu vinavyowazunguka binadamu na wanyama maishani mwao. Kuna uchafuzi wa aina mbalimbali na kila uchafuzi humhusu binadamu kwa njia fulani.

Maendeleo ya viwanda duniani ni sababu mojawapo ya uchafuzi wa hewa. Mitambo katika karakana huwa inatoa moshi mwingi wakati bidhaa zinapotengenezwa. Moshi husambaa eneo kubwa na kuchanganyika na hewa inayovutwa na binadamu. Uchafu hutupwa ovyo ovyo na kuwa hatari kwa afya ya binadamu. Maji machafu huweza kutiririkia mtoni, maziwani na hata baharini. Yale yanayotiririka mitoni na maziwani huchafua maji ambayo hutumiwa na watu wa eneo hilo kwa kunywa, kupika na kunywesha mifugo wao. Yale yanayotiririka baharini huwa ni hatari kwa samaki wanaotegemewa na binadamu kuwa kitoweo muruwa.

Ongezeko la watu pia ni hali nyingine ya uchafuzi wa mazingira. Halaiki ya watu hufanyauharibifu wa misitu ya asili. Hii ni kwa sababu ya kutaka kuongeza ekari za mashamba. Hili husababisha mmomonyoko wa udongo; hivyo basi kuiacha ardhi bila rutuba yoyote. Katika hali hii, kilimo ambacho ni uti wa mgongo wa nchi nyingi duniani huzoroteshwa. „„Maisha ya binadamu hutegemea kilimo kwa kila hali kwa hivyo kilimo kinapozoroteka hata uchumi nao huathirika. Kila uchao tunasikia kwamba nchi fulani imekabiliwa na njaa.

Ufugaji wa wanyama wengi bila mpango maalum pia huharibu mazingira ya asili kama nyasi na vichaka. Watu wengi hufuga ng"ombe, mbuzi na kondoo. Kwa kuwa hawana mahali maalum pa kuwalisha, huzunguka nao huku na huko kutafuta nyasi na majani ya kuwalisha. Wanyama wanaotangishwatangishwa namna hiyo humaliza majani na nyasi zote na kuacha ardhi tupu ambayo hatimaye huyabisika kwa jua. Ardhi ya namna hii haishiki maji mvua inyeshapo. Nchi iliyoneemeka huweza kuwa jangwa lililo na chungu ya mchanga.

Watu wanapoongezeka huko mashambani huwabidi wakate misitu ili waanzishe maskani mapya pamoja na mashamsba yao. Miti hukatwa bila hadhari na mabiwi ya matawi pamoja na majani huchomwa moto. Jambo la kusikitisha ni kwamba miti hiyo inapokatwa hakuna mingine inayopandwa kuchukua mahali pake.

Mahitaji ya binadamu ya kuendeleza njia za mawasiliano pia huzusha balaa nyingine. Barabara zinazidi kuongezeka na pia watu wanaozidi kuongezeka pamoja na mazao yao. Kwanza, barabara zinapotengenezwa misitu hukatwa mahali zinapopitia. Pili, wingi wa magari huzidi na baadhi ya hayo magari hutoa moshi unaoharibu hewa.

Njia kadha wa kadha za kuzuia uharibifu wa mazingira zimependekezwa. Ingawa suluhisho timamu halijafikiwa, serikali nyingi duniani zimo katika harakati za kutafuta suluhisho la uchafuzi huo.

Njia mojawapo ni kukomesha ujenzi wa viwanda katika miji mikuu na mahali palipo na watu wengi.Wenye viwanda pia wanahimizwa kufikiria jinsi ya kutupa takataka na maji machafu bila kudhuru afya ya binadamu.

Watu wakizingatia suala la upangaji wa uzazi na kuwa na familia ndogo ndogo, idadi ya watu haitaongezeka kwa kasi kwa hivyo itakuwa hakuna haja ya kuanzisha makao mapya mara kwa mara.

Serikali nyingi zimechukua jukumu la kuwaelimisha raia juu ya madhara yanayotokana na uharibifuwa mazingira. Raia wanahimizwa kupanda miti kwa wingi. Aidha, ni jukumu la jamii katika eneo athirika kujenga matuta ya kuzuia mafuriko na kudhibiti mmomonyoko wa udongo.

Jitihada zinazofanywa kuzuia uchafuzi wa mazingira hukumbana na matatizo. Tatizo kubwa ni fedha za kuendeleza miradi inayopendekezwa. Shida nyingine ni kwamba juhudi zingine huwa zinamwingilia binadamu na mali yake.

**Maswali**

(a) Fupisha aya sita za kwanza za taarifa uliyosoma kwa maneno 60. (alama 7)

(b) Fupisha aya za mwisho tano kwa maneno 50-55 (alama 6)

**MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

(a) Andika tofauti moja kati ya sauti zifutazo. (alama 2)

(i) /ny/ na /ng'/

(ii) /g/ na /gh/

(iii) /s/ na /z/

(iv) /ch/ na /j/

(b) Aindika kielezi chenye miundo ifuatayo. (alama 1)

Kipasuo ghuna cha ufizi, irabu ya chini kati, irabu ya mbele juu, nazali ya midomo, irabu ya kati chini na tandazwa.

(c) (i) Silabi ni nini? (alama 1)

(ii) Huku ukitoa mifano, eleza miundo miwili ya silabi za Kiswahili. (alama 2)

(d) Eleza dhima tatu za viambishi tamati mbali na kauli ya kutenda/kiishio. (alama 3)

(e) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili ya kiambishi: **-I-** (alama 2)

(f) Andika sentensi hii katika ukubwa. (alama 1)

***Kijumba chenyewe kilijengwa karibu na mto***.

(g) Taja nomino mbili kutoka ngeli tofauti zinazowakilishwa na kiambishi ngeli kilichopigiwa mstari. (alama 2)

**I**tatumika katika sherehe yake.

(h) Badilisha sentensi katika kauli iliyomo kwenye mabano.

(i) Marie alipewa zawadi yake. (tendeka) (alama 1)

(ii) Tunga sentensi ukitumia kitenzi kishirikishi kipungufu katika ngeli ya KI-VI. (alama 2)

(i) Yakinisha sentensi ifuatayo katika nafsi ya pili umoja. (alama 1)

**Sitaenda nyumbani kesho**.

(j) Tunga sentensi ukitumia nomino dhahania katika ngeli ya U-U kutokana na neno: (alama 2)

**Zusha**

(k) Eleza maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii. (alama 2)

**Mama anatupa mtoto.**

(l) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. (alama 2)

**S – KN(N+S)+KT(Ts+T+E)**

(m) Akifisha: (alama 4)

Akionekana mwenye hasira mkurugenzi huyo alishangaa jameni kwa nini wakenya wanaharibu mali hivi hii si siasa bali ni wendawazimu.

(n) Tunga sentensi kudhihirisha masharti yasiyowezekana katika hali timilifu. (alama 2)

(o) Wanne walituzwa na mwalimu. (Tumia kivumishi cha kuorodhesha). (alama 2)

(p) Taja vitenzi vyovyote viwili vyenye asili ya kigeni katika kauli ya kutendea. (alama 2)

(q) Ainisha yambwa katika sentensi; (alama 3)

***Mwanafunzi alitumiwa barua kwa posta.***

(r) Unda nomino mbili katika hali ya wingi kutokana na kitenzi hiki. (alama 2)

***Sawidi***

(s) Biwi ni kwa taka ……………………ni kwa maji na kikuba ni kwa ………………. (alama 1)

**3. <u>ISIMU-JAMII (ALAMA 10)</u>**

"Leo hii utashi wetu wa kujitosheleza umetusukumiza ukingoni mwa maisha. Vyakula vyetu sasa vina kemikali hatari kutokana na mizizi ya mimea kufyonza virutubisho vyenye naitrojeni. Virutubisho hivi hustawisha mimea. Hata hivyo, mimea hii tunayoila ina kemikali hatari kwa miili yetu. Kemikali hizi husababisha saratani na hili ndilo tatizo la kijiji hiki.

(a) Bainisha sajili ya makala haya kwa kutoa mfano mmoja kutoka kwenye makala. (alama 2)

(b) Fafanua sifa nyingine nane za sajili hii ambazo zingejitokeza katika makala haya. (alama 8)

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: ……………………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ………………DARASA: …...........**

# SHULE YA UPILI YA FRIENDS KAMUSINGA

**102/2**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA PILI**

**Maagizo**

*a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

*b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

*c) Jibu maswali **yote**.*

*d) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

*e) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*

*f) Karatasi hii ina kurasa **9** zilizochapishwa.*

*g) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| Jumla | 80 | |

**1. UFAHAMU** **alama 15**

Nimekaa na kutafakari kwa kipindi kirefu, juu ya mabilioni ya pesa ambayo yametengwa na serikali ili kudhamini miradi ya maendeleo ya wanawake. Kina mama au wanawake wengi wanakiri na kusema kwamba fedha hizo zimewezesha kuwaondoa katika lindi la unyanyasaji kutoka kwa waume zao, kwani kila mmoja anamheshimu mwenzake kwa sababu ya kipato alicho nacho. Wengi wameweza kuanza biashara ndogondogo ambazo huwaletea angaa kipato kidogo. Ukweli ni kwamba fedha hizi zimesaidia kuwatoa wanawake wengi katika unyanyasaji, kwani wengi wanaweza kuanzisha kazi za ujasiramali ni ahata kuendesha shuguli mbalimbali za maendeleo.

Kutokana na mafanikio haya, wabunge waliopitisha hoja bungeni ya kuanzisha mpango huu wa kuwakwanua wanawake kimaendeleo wanafaa kupongezwa. Mafanikio haya yamewafanya akina mama kujikimu kimaisha na hivyo kutowategemea wanaume katika kila jambo.

Ukitaka kujua ukweli kuhusu hili, nenda kwenye masoko utaona akina mama jinsi wanavyohangaika na biashara zao. Kwa hivyo, ujasiriamali huendelezwa na akina mama zaidi na hivyo wanapaswa kuwezeshwa kwa kila hali na mali.

Akina mama pia wanafaa kupongezwa kwani wameamua kujitosa kukopa fedha kutoka kwenye taasisi mbalimbali za fedha. Fedha hizo kiwango kikubwa zimewainua kutoka katika ufukara uliokithiri hadi katika misha ya heshima. Wale ambao hawajajaribu kuchukua mikopo, ni muhimu wafanye hivyo ili wajikimu kimaisha.

Maisha ya sasa ni magumu, hivyo yanahitaji kusaidiana kwa kila hali na mali.

Wanaume kwa wanawake ni vyema wachange bia ili wazumbue riziki. Ushirikiano utarahisisha maisha. Hata hivyo, sio tu akina mama hao wameondokewa na unyanyasaji waliokuwa wakiupata ndani ya nyumba zao, toka kwa akina baba, bali hata masuala ya mrundikano wa kesi za kugonbea ardhi kwa akina mama, zimepungua. Sababu ni kwamba akina mama wengi wameweza kujitafutia ardhi wenyewe kwa fedha walizonazo.

Ukweli ni kwamba hali imebadilika. Kinyume na hapo awali, ambapo majumba ya kifahari na mashangingi yalikuwa hifadhi ya wanaume. Siku hizi wanawake wanamiliki hayo yote.

**Maswali**

a) Onyesha jinsi **tano** ambazo kwazo pesa zimemwinua mwanamke. (alama 5)

b) Eleza uhusiano wa kijinsia unaosawiriwa katika kifungu. (alama 3)

c) Taja na ueleze taasisi zozote mbili zilizochangia kuboresha hali ya kina mama. (alama 2)

d. Eleza kwa nini baadhi ya wanawake wangali wanaishi katika umaskini. (alama 2)

e) Eleza maana ya msamiati na mafungu haya. (alama 3)

i. Riziki ..............................................................................................................

ii. Wachange bia ..................................................................................................

iii. Ujasiria mali ...................................................................................................

**2. UFUPISHO** **(alama 15)**

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Mavazi ni muhimu sana kwa insi kwa sababu hutumiwa kusitiri mwili wa mwanadamu. Fauka ya hayo, mavazi humpa mtu unadhifu au urembo. Mavazi pia humsaidia mtu kujikinga kutokana na baridi kali. Hebu fikiria wakati mvua inanyesha au iwapo unatembea bila nguo katika maeneo kama vile Limuru, Timboroa,Kericho na kwingineko ambapo baridi kali hutamalaki. Je, utaweza kuvumilia au mwili wako utaganda kutokana na barídi hii? Mavazi basi yana faida si haba.

Kuna mavazi aina nyingi katika jamii mbalimbali. Mavazi yaweza kuwa mafupi, wastani au marefu. Fauka ya hayo,kuna mavazi yanayovaliwa na wanawake huku mengine yakivaliwa na wanaume. Mavazi yanaweza kuwa rasmi au si rasmi. Hivi majuzi katibu mkuu wa chama cha mawakili nchini Bwana Mutua,alipendekeza unadhifu miongoni mwa mawakili na majaji ambapo alisisitiza umuhimu wa kudumisha unadhifu na heshima katika taaluma hii kupitia mavazi.Katika shule zetu za msingi na zile za upili pia kuna sheria znazolenga mavazi. Wanafunzi wote wanastahili kuwa na sare.Sare huwafanya wote kuonekana sawa. Iwapo hakungekuwa na sare, basi wale wanafunzi kutoka familia tajiri wangekuwa wakivaa nguo za bei ya juu huku wale kutoka katika familia za walalahoi wakivaa zile duni.Jambo hili huweza kuwavunja moyo wanafunzi na kuleta unyanyapaa miongoni mwa wengine.

Aliyekuwa waziri wa elimu hivi punde, marehemu Mutula Kilonzo, alizua mjadala mkali kuhusu mavazi katika shule za upili za wasichana nchini. Mjadala huu ulihusu urefu wa sketi zinazovaliwa na wanafunzi wasichana.Kulingana na Kamusi ya Karne ya 21, sketi ni vazi la wanawake linaloanzia kiunoni hadi magotini. Hata hivyo, waziri huyo alipendekeza kuwa, sketi za wanafunzi wasichana zinaweza kuwa fupi. Mjadala mkali uliibuka wengi walidai kuwa,zikiwa fupi sana wasichana wetu wa shule huenda wakajipata kuwa windo la walimu wanaume. Wengine walisema kuwa huenda wanafunzi hawa wakapata shida ya kumakinika darasani kutokana na urefu wa sketi hizi fupi hasa wanapoketi au wanapoinama. Wazazi wengi walisema kuwa huenda wasichana hawa wakajiingiza katika vishawishi vya mapenzi ya kiholela.

Katika shule moja ya wasichana huko Thika, kulikuwa na suitafahamu baada ya mwanafunzi mmoja wa kike kujipata katika mzozo baada ya shule hiyo kupinga tabia ya mwanafunzi kuvaa kwa kufuata mtindo wa dhehebu fulani.Shule hiyo ilisimama kidete na kusema kuwa wanafunzi wanafaa kuvaa kama wanafunzi wala si kama waumini. Kumekuwa pia na mzozo katika shule kadhaa hapa nchini kuhusu wanafunzi kuvaa buibui.

Wanafunzi wa kiume pia wamejipata katika utata kwa kuvaa hasa suruali ndefu kwa njia isiyopendeza. Wao huzivuta chini kupita kiasi. Wengine hukosa kufunga mishipi kiunoni badala yao kuziteremsha chini ya kiuno na kuonyesha ukosefu mkubwa wa nidhamu. Wengine wao pia huvaa shanga shingoni. Fauka ya hayo, wengine huvaa bangili ambapo ni kinyume cha sheria. Wanafunzi katika shule hizi wanastahili kuzingatia sheria za shule kuhusu mavazi. Wanafunzi lazima wakumbuke kuwa sheria zilizowekwa shuleni zinakusudiwa kuleta nidhamu katika shule na kuwasaidia kuwa watu wa kufaa katika maisha. Wao ni wa umri mbichi na ni lazima waelekezwe. Wasipewe uhuru wa kuvaa watakavyo kama wafanyavyo wanafunzi katika vyuo vikuu. Hawafai kujilinganisha na wanafunzi hao kwa sababu wale wa vyuo vikuu wana umri wa

kujiamulia mambo yao ikilinganishwa na wanafunzi wa shule za upili au zile za msingi. Ni ombi letu kuwa washikadau katika elimu watazidi kuendeleza nidhamu kupitia mavazi ya wanafunzi shuleni.

a) Fupisha aya za kwanza nne kwa maneno 100 (alama 9, utiririko 1)

b) Fupisha aya ya mwisho kwa maneno 40 – 50. (alama 6, utiririko 1)

**3. MATUMIZI YA LUGHA** **(Alama 40)**

a) i) Andika neno lenye nazali ya kaakaa laini. (alama 1)

ii) Onyesha muundo wa silabi katika neno; (alama 1)

msahaulifu

b) Tofautisha sentensi zifuatazo ukizingatia kiimbo. (alama 1)

i) Tafadhali karibieni hapa.

ii) Karibieni hapa.

c) Ainisha vielezi katika sentensi hii. (alama 2)

Mwanafunzi hodari kabisa aliwapiku wote michezoni.

d) Tumia kiwakilishi cha pekee chenye dhana ya **“baadhi”** katika sentensi. (alama 2)

e) Eleza maana ya viambishi katika neno **mmevipa**. (alama 2)

f) Andika kinyume. (alama 2)

Watoto wamemeza dawa kali wakakashifiwa.

g) Yakinisha katika wakati ujao. (alama 2)

Mikunga hawajakuwa wakivuliwa kwa wingi.

h) Tendua. (alama 2)

Milango iliyofungwa itachomwa mikuki.

i) Andika katika wingi. (alama 2)

Uyoga uliokuwa kwenye kasha umeoza.

j) Andika ukubwa wa sentensi ifuatayo. (alama 2)

Ndama wa ng’ombe yule amevunja ndoo kwa upembe mmoja.

k) Tunga sentensi kuonyesha kitendo kinaendelea kufanyika. (alama 2)

l) Andika sentensi upya ukifuata maagizo. (alama 2)

i) Kaumu alicheza mpira kwa niaba ya Jack. (Anza: Jack…)

ii) Mto ambao umelaliwa na mtoto una kunguni. (Tumia “o” rejeshi ya tamati badala ya “amba”.)

(alama 2)

iii) Waziri Ndiema aliteuliwa baada ya mtangulizi wake kujiuzuru. (alama 2)

(Geuza neno liliopigiwa mstari kuwa nomino.)

m) Andika katika usemi wa taarifa. (alama 2)

“Alaa! Mzee huyu ni mwenye imani hivi?” Amani aliuza.

n) Tambua aina za virai vilivyopigiwa mstari katika sentyensi hii. (alama 2)

Mwanamwali hodari ajabu alitembea kwa madaha kwenda kupojea tuzo lile.

o) Onyesha matumizi ya **ku** katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Yona hakujutia kumchapa mkewe Sara.

p) Andika ngeli mbili za neno **“kucha”**. (alama 2)

q) Changanua kwa njia ya jedwali. (alama 3)

Fumbo alilotufumbia juzi lilifumbuliwa na Khalim.

r) Ainisha yambwa katika sentensi ifuatayo; (alama 2)

Asha alimpikia shangazi yake wali mkavu kule kijijini.

**4. ISIMUJAMII** **(Alama 10)**

“Hawa wachezaji wa Manyuu hawacheki na watu leo. Wameamua kuishambulia timu ya Cheusi bila huruma. Kumbuka kwamba hii ni mara yao ya... Lo! Anauchukua mpira pale, mchezaji nambari tisa... Matiksta. Matiksta, Matiksta na mpira. Anaucharazacharaza pale. Anamwangalia mwenzake. Anaupiga mpira kwa kichwa pale! Lo! Mwenzake anaukosa. Akiushika mpira pale ni mchezaji wa timu ya Cheusi, Romana. Romana, Romana anaelekeza mpira kwenye lango la Manyuu. Anaupiga mpira kwa nguvu! Lo! Hatari sana. Hatari sana katika lango la Manyuu. Hatari! hatari! Gooooaaaaaal! Noooo ooh! Wameukosa! Goal keeper ameudaka mpira huo. Pole sana wachezaji wa ... Mlinda lango anaupiga mpira huo kwa hasira.”

a) Tambua sajili ya dondoo hili. (alama 1)

b) Eleza sifa **sita** za sajili hii kama zinavyojitokeza kwenye dondoo. (alama 6)

c) Fafanua sifa **nyingine tatu** za sajili hii ambazo zingejitokeza. (alama 3)

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: …………………………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ………………DARASA: …...........**

# SHULE YA UPILI YA LENANA

**102/2**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA PILI**

**MAAGIZO**

***a)*** *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***b)*** *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***c)*** *Jibu maswali* ***yote.***
***d)*** *Majibu yako yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
***e)*** *Majibu yote* **lazima** *yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
***f)*** *Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*
***g)*** ***Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

**Kwa matumizi ya mtahini pekee.**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | **15** | |
| 2 | **15** | |
| 3 | **40** | |
| 4 | **10** | |
| **Jumla** | **80** | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

1. **UFAHAMU** **(ALAMA 15)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Zamani wanadamu wa kwanza ambao ni mababu wa vizazi vingi vilivyopita waliishi duniani. Habari kuhusu maisha na maumbile yao haikujulikana kwa hakika kwa sababu hawakuwa na uwezo wa kuandika. Lakini mara kwa mara shughuli za wanaakiolojia kama Louis Leakey na wengine hugundua mifupa yao ardhini na michoro yao katika mapango. Wataalamu hawa hufukua mafuvu, vyombo na silaha zao za zamani. Kwa kuchuguza vitu hivi tunaweza kubahatisha viumbe hawa walivyokuwa na jinsi walivyoishi.

Moja ya mambo yanayofahamika sasa ni kuwa wanadamu hawa wa awali walifanana na sokwe. Aidha, walitembea kwa kupinda mgongo kama kibiongo. Chakula na uhai wao ulitegemea kukusanya matunda, kokwe, majani ya miti na mayai ya ndege. Vilevile, walitegemea wanyama wadogo, kufukua mizizi na kubambua magamba ya miti **walipokabwa** na njaa.

Maisha yao yalikuwa ya hatari. Walikuwa wakiwindwa na wanyama wakubwa. Hii ni kwa sababu mwanzoni hawakuwa na silaha za **kujihami**. Hivyo iliwabidi kujificha katika miti na vilima kuepuka uvamizi. Lakini usalama wao ulitegemea kwa kiasi kikubwa kudura za Mungu au pengine miungu.

Kwa taratibu wanadamu hawa walijifunza kutengeneza silaha. Walianza kwa kutumia fimbo nene zenye ncha au mawe ya kutupia. Baadaye walichonga mawe ili kufanya kuwa visu, nyundo au vigumba vya mikuki. Hatimaye, walivigomoa au kupasua vipande vya mawe na kuvitumia kama mishale. Hapa ndipo walipoanza kuwinda wanyama wakubwa mithili ya swara, nguruwe, nyati na ngiri. Pia waliweza kutumia mikuki kudunga samaki majini.

Mababu zetu hawakuwa na nyumba. Kwanza walikuwa wakijisitiri kwa kukaa chini ya vivuli vya miti au kujenga vibanda vya matawi na majani ya miti. Hawakuweza kuingia mapangoni asilani kwa kuchelea wanyamapori wakali kama chatu, simba na mamba waliokaa humo. Kwa bahati, siku moja mmoja wao aligundua moto alipokuwa akipekecha vijiti. Kabla ya ugunduzi huu, wao pia hawakujua kazi ya moto na walikuwa wakiogopa na kukimbia moto jinsi wafanyavyo wanyama wa mbugani mpaka leo.

Ujuzi wao wa kutumia moto ulileta mabadiliko makubwa. Baada ya hapo waliweza kukaa mapangoni na kukoka mioto milangoni mwa mapango ili kuwaogofya adui. Hali kadhalika, waliweza kuota moto, kumulikia **maskani** yao mapya na kuchoma nyama badala ya kuila mbichi.

Wanadamu wa awali hawakuwa na mavazi. Waliwezaje kuzuia baridi? Inadhaniwa kwamba nywele nyingi walizokuwa nazo kwenye mwili zilisaidia kuwapa joto. Uvaaji wa nguo ulianza walipoanza kutumia

ngozi kutoka kwa wanyama waliowawinda. Walizisafisha ngozi kwa kuzipaa kwa kombe za mawe na kuzianika juani. Zilipokauka walizifunga na kuzishikanisha kwa mifupa au mikanda ya ngozi.

Wanadamu hawa hawakuweza hata kuongea. Waliwasiliana kwa kupiga mayowe, kutoa milio au kuguruma jinsi wafanyavyo wanyama. Polepole walianza kutumia sauti na baada ya muda walipanga sauti kuibua mfumo wa maneno yenye maana za kipekee. Umilisi wa kutumia lugha uliwawezesha kupiga hatua kubwa kimaendeleo. Lugha pamoja na matumizi ya moto na silaha viliwarahisishia maisha na kuwawezesha kupata muda wa kupumzika mapangoni jioni wakiota moto. Kutokana na hali hii waliweza kutekeleza jambo moja kuu waliloturithisha. Walitupokeza Sanaa. Kutoka kwao tulirithi fasihi simulizi na kupata nakshi za michoro yao kwenye mapango. Michoro hii inapatikana katika mapango hata leo hii nchini Ufaransa, Uhispania, Afrika Kusini na hata Afrika Mashariki.

**MASWALI**

a) Msemo "Kudura za Mungu au pengine miungu" inadhihirisha hali gani ya wanadamu wa kwanza.

( alama 2)

------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------

b) Kwa nini wanadamu hawakuishi mapangoni mwanzoni? (alama 1)

------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------

c) Fafanua mambo **matano** yaliyomwezesha mwanadamu wa kwanza kupiga hatua kimaendeleo.

(alama 5)

------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------

d) Taja sifa zilizotofautisha wanadamu wa awali na wa siku hizi? (alama 2)

e) Eleza maana ya? (alama 3)

i) walipokabwa

ii) kujihami

iii) maskani

**2. UFUPISHO** **( ALAMA 15)**

Uwazaji tunduizi ni tendo ambalo huhusisha matumizi ya akili. Uwazaji huu umekitwa kwenye matumizi ya michakato kama makini, upangiliaji, uteuzi na tathmini. Hata hivyo, uwazaji huu si mchakato mwepesi bali ni mchakato changamano.

Mchakato wa uwazaji tunduizi unahusisha stadi na mikabala tofauti. Mathalan, kuweza kutambua na kubainisha misimamo ya watu wengine, hoja wanazozua na uamuzi waliofikia kutathmini au kupima ushahidi uliopo ili kubainisha mitazamo tofauti. Vilevile, uwazaji tunduizi hushirikisha kupima hoja za upinzani na ushahidi uliopo kwa njia ya haki pamoja na kutambua yaliyofichwa au ukweli uliofunikwa na taswira ya juu juu. Hali kadhalika, uwazaji tunduizi hujumisha kutambua mbinu zinazotumiwa kufikia misimamo fulani kwa mvuto zaidi na kwa matumizi ya mbinu za kishawishi. Aidha, uwazaji huu huhitaji kutathmini masuala kwa mtindo ulio wazi, kufikia uamuzi kama hoja zinazotumiwa zina mashiko au zinakubalika kuwa nzuri. Zaidi ya hayo, uwazaji tunduizi unahusisha kuwasilisha mtazamo kwa njia yenye uwazaji mzuri na inayoshawishi.

Uwazaji tunduizi una manufaa anuwai. Mosi, unasaidia kujenga makini ya utendaji. Pili, hupevusha uwezo wa usomaji kwa kuufanya usomaji huo uwe na malengo wazi. Fauka ya hayo unamsaidia mtumiaji kutambua hoja kuu katika matini au ujumbe fulani ya kuzongwazongwa na hoja duni za pembeni. Uwazaji huu unasaidia kuuchonga uwezo wa kuikabili au kuiitikia hali fulani na kukuza stadi za uchanganuzi. Mwanadamu huwa mtu tofauti na bora anapoujenga na kuuimarisha uwazaji tunduizi wake.

***Maswali***

a) Bila kubadilisha maana aliyokusudia mwandishi, fupisha aya mbili za mwanzo. (maneno 70-80)

(alama 8, 1 utiririko)

**Jibu**

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

b) Andika kwa muhtasari mambo muhimu katika aya ya tatu. (maneno 35-40) (alama 5, 1 ya utiririko)

**Jibu**

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

**3. MATUMIZI YA LUGHA** **( ALAMA 40)**

a) Tofautisha sauti zifuatazo. (alama 2)

i) /ny/ na /m/

--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

ii) /a/ na /u/

--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

b) Andika neno lenye muundo ufuatao wa silabi. (alama 1)

K-KKI

--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

c) Ainisha nomino katika sentensi hii.

Kuuza sukari kwa Rehema kulimfanya awe na utajiri. (alama 2)

--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

d) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika hali yakinishi.

Mtoto hakupatiwa chakula wala nguo. (alama 1)

--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------

e) Kwa kutoa mifano, ainisha aina mbili za mofimu. (alama 2)

--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

f) Andika katika hali ya ukubwa wingi. (alama 2)

Mwanamke alibeba kiti chake.

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------

g) Ainisha yambwa katika sentensi hii. (alama 3)

Mtoto alipikiwa chakula kizuri kwa mwiko.

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

h) Tunga sentensi yenye kivumishi cha pekee chenye dhana ya kutojali. (alama 2)

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

i) Kwa kutunga **moja** sentensi tofautisha kati ya vitate hivi. (alama 2)

Mzazi na msasi.

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

j) Eleza maana ya kiambishi **"ji"** katika sentensi hii.

Mcheza**<u>ji</u>** ali**<u>ji</u>**kata kwa kisu. (ala1)

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

k) Taja ngeli za nomino zifuatazo. (alama 1)

Kiwete

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

Maji

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

l) Tunga sentensi ukitumia neno **<u>vile</u>** kama **kitenzi** na **kivumishi**. (alama 2)

m) Ainisha virai tofauti katika sentensi ifuatayo. (alama 3)

Mwalimu yule mzuri sana alikuja darasani mapema sana.

n) Onyesha matumizi ya viakifishi vifuatavyo; (alama 2)

i) kibainishi

ii) vifungo

o) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi. (alama 4)

Kitabu kilichonunuliwa ni hiki.

p) Sahihisha kwa njia mbili tofauti. (alama 2)

Mwanafunzi alifika katika nyumbani

q) Eleza maana ya nahau **kula mwata**. (alama 1)

r) Tambulisha hali katika sentensi hii. (alama 1)

Mtoto acheza.

s) Andika kulingana na maagizo. (alama 2)

Mtoto alipoenda Mombasa alijawa na furaha. (anza kwa: Kwenda…)

**4. ISIMU JAMII** **(ALAMA10)**

a) Umeteuliwa kama mtangazaji wa mashindano ya michezo baina ya shule katika eneo gatuzi ndogo lenu. Eleza sifa tano za lugha utakayotumia. (alama 5)

b) Jadili mambo matano yanayoathiri matumizi ya lugha katika jamii. (alama 5)

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: ……………………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ………………DARASA: …...........**

# MTIHANI WA PAMOJA WA MERU

**102/2**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA PILI**

**Maagizo**

- ***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
- ***b)*** *Jibu maswali yote.*
- ***c)*** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*
- ***d)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. UFAHAMU | 15 | |
| 2. UFUPISHO | 15 | |
| 3. SARUFI | 40 | |
| 4. ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**1 UFAHAMU (alama 15)**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jamii, uainishaji wake na udhihirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dahari ya miaka. Suala hili huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu. Msingi mkuu wa uainishanji wa mahusiano hayo ni kukichuza kipindi cha mahusiano yenyewe. Yapo mahusiano bainaya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache na mengine ambayo huenda yakachukua miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni yale yanayojulikana kama mahusiano ya kudumu. Inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi kikubwa. Watu wengi huitakidi kuwa uhusiano uliopo baina ya mtu na jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwa hiyo ni uhusiano wa kudumu. Hali hii hutokana na uhalisi kuwa tunahusiana na jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiano huuhautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu;tunaendelea kuwasiliana kwa barua au, katika enzi hii ya utandawazi,kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi na kudumisha uhusiano wetuwa kijamaa. Hata hivyo, inawezekana baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalan, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu au wa kipindi kirefu,unaweza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofumbatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili,mahusiano ya kipindi cha wastani,kuna mahusiano yanayohusisha marafiki zetu maishani, shuleni au kwenye taasisi zozote zile, majirani zetu, wenzetu katika mahali mwa kazi,washiriki kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea. Inawezekanakudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya,hususan baina ya marafiki na majirani huweza kuwa ya miongo na daima. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfumo wa jamii. Kwa mfano, kwa wanajamii waoishi kwenye janibu fulani mahsusi, na kwa miaka tawili bila ya kuhajiri,uhusiano wao na majirani huweza kuwa wa kudumu. Hali hii **inasigana** na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini. Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilikabadilika. Isitoshe,kutokana na mfumo wa maisha ya kibepari **yameghoshi** ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi huweza kuumomonyoaukuta wauhusiano wa kudumu.

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na majirani zao. Uhusiano katiya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wamajirani. Vimbunga vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo ya kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasahuweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini.

Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujirikatika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa za dukani, kwenye sehemu za

ibada,kwenye kituo cha mafuta,kwa kinyozi, kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya kuyazungumzia mahusiano ya aina hii kama ya mpito. Kwanza, uwezekanowa mabadiliko ya anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa kinyozi au msusi unatambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo, kuna **vighairi** hususa pale ambapo mtoa huduma anayehusika ni yule yule mmoja.

Mahusiano ya mpito yanatawaliwa na'uhusiano wa chembe chembe.' Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo wa kibepari, unamaanisha kuwa kinachoshughulisha mtu ni chembe ndogo tu ya mwenzake. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma, kwa mfano, gazeti analokuuzia mtu, viatu anavyokushonea,nguo anazokufulia,ususi anokufanyia na kadhalika. Mahussiano ya aina hii yametovukwa na hisia za utu na ni zao la mifumo ya kisasa ya kiuchumi na kijamii. Mtu anayehusiana na mwenzakekwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwenzake amekosa chakula,amefutwa kazi,amefiliwa,ameibiwa na kadhalika.

Suala kuu tunalopaswa kujiuliza ni: je, tunahusianavipi na jamaa zetu, marafiki zetuna majirani zetu? Je, uhusianowetu na raia wenzetu ni wa aina gani? Je, uhusiano wetu na nchi yetu ni wa mpito au ni wa kudumu?

**(a)** Taja kigezo cha kuzungumzia mahusiano. (alama 1)

**(b)** Eleza imani ya watu kuhusu mahusiano ya watu. (alama 1)

**(c)** Fafanua athari ya teknolojia kwenye mahusiano ya watu. (alama 2)

**(d)** Eleza sababu nne kuu za kuharibika kwa mahusiano katika maisha ya leo.(alama 2)

**(e)** Taja sifa kuu za mahusiano ya muda mfupi. (alama2)

**(f)** Je, kifungu hiki kina ujumbe gani mkuu? (alama2)

**(g)** Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. (alama 3)

i. Inasigana

ii. yameghoshi

iii. (vighairi

**2 UFUPISHO (alama 15)**

Jamii ya leo inatawaliwa na kuendeshwa na kanuni ya maarifa. Inawezekana kusema kuwauchumi wa jamii za leo na zijazo utategemea maarifa zaidi kuliko utakavyotegemea uwezo wowote mwingine. Utambuzi wa uwezo mkubwa wa maarifa katika maisha ya binadamu ndio msingi wa watu kusema 'maarifa ni nguvu.'

Maarifa huelezwa kwa tamathali hii kutokana na uwezo wa: kuyadhibiti,kuyaendesha, kuyatawalana kuyaongoza maisha ya binadamu popote pale walipo. Mtu ameyakosa maarifa fulani huwa ameikosa nguvu hiyo muhimu na maisha yake huathirika pakubwa. Kwa msingi huu, maarifa yanawezakuangaliwa kama utajiri mkubwa ambao binadamu anaweza kuutumia kwa faida yake au kwa faida ya wanajamii wenzake. Ukweli huu ndio unaoelezwa na methali ya Kiswahili: 'Elimu ni mali.' Elimu ni chimbuko la maarifa muhimu maishani.

Msingi wa utajiri na maendeleo ya binadamu popote alipo basi ni maarifa. Je, maarifa kwa upande wake yana sifa gani? Maarifa yenyewe hayana upinzani. Maarifa uliyo nayo huweza kuwa na watu wengine pasiwe na upinzani baina yenu kwa kuwa kila mmoja ana maarifa sawa. Kila mmoja ana uhuru wa kuyatumia maarifa hayo kama chanzo cha kuyazalisha mengine. Utumiaji wa maarifa yenyewe hauyamalizi maarifa hayo. Maarifa hayawezi kugusika ingawa mtu anaweza kuyanyumbua maarifa yenyewe kwa kuyatumia kwa namna tofauti.

Maarifa huingiliana na maarifa mengine. Maarifa aliyo nayo mtu huweza kuhusishwa na maarifa aliyo nayo mtu mwingine ili kuvyaza au kuzuka na maarifa tofauti. Maarifa yanaweza kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa namna ambavyo mtu huweza kufanya bidhaa nyingine ile. Kwa mfano, ni muhali mtu kulalamika kuwa hawezi kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa sababu ana mzigo wa maarifa kichwani.

Sifa nyingine muhimu ya maarifa ni kuwa yanaweza kuwasilishwa kwa njia au mitindo mingine ya kidhahania. Ikiwa unataka kukihamisha chombo fulani kutoka sehemu moja hadi nyingine, lazima uwazie ukubwa wake, uzito wake na labda hata umbali wa panapohusika. Maarifa huweza kubadilishwa au kugeuzwa na kuwa ishara ambazo huyafanya kuwasilishswa kwa njia nyepesi kuliko kwa mfano ikiwa mtu atayawasilisha katika muundo wa, kwa mfano,kitabu.

Maarifa yana sifa ya uhusianaji. Kipengele fulani cha maarifa huwa na maana kinapowekwa sambabmba au kugotanishwa na kipengele kingine cha maarifa. Huo huwa muktadha mzuri wa kueleweka au kuwa na maana kwa mfano, neno ‘mwerevu’ huweza kuwa na maana kwa kuwekwa katika muktadha wa ‘mjinga’, ‘ mjanja’, ‘hodari’ na kadhalika.

Maarifa huweza kunifadhiwa katika nafasi ndogo sana. Suala hili linaeleweka kwa njia nyepesi tunapoangalia maarifa katika muktadha wa teknolojia. Data zinazowahusu mamilioni ya watu,ambazo zingehitaji maelfu ya maktaba na lukuki ya vitabu, huweza kuhifadhiwa kwenye kifaa kidogo kinachoweza kutiwa mfukoni.

Maarifa hayawezi kuthibitiwa au kuzuiliwa mahali fulani yasisambae. Maarifa huenea haraka sana. Maarifa ni kitu kinachoepuka pingu za watu wanaopenda kuwadhibiti binadamu wenzao. Hata pale ambapomfumo wa kijamii au wa kisiasa unafanya juu chini kuwadhibiti raia au watu wenyewe,ni muhali kuyadhibiti maarifa yenyewe. Inawezekana kuzidhibiti njia fulani za uenezaji wa maarifa lakini maarifa hayo yatapata upenyu wa kusambaa. Ni kweli kuwa maarifa ni nguvu inayozishinda nguvu zote.

(a ) Fupisha aya ya pilina tatu (maneno 55-60)(alama 5, 1 ya utiririko)

(b) Eleza sifa kuu za maarifa kama zinavyojitokeza kuanzia aya ya nne hadi aya ya nane.

(maneno 100-110) (alama 10, 2 za utiririko)

## 3 MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)

**a)** Taja sauti mbili zinazotamkwa mdomoni. (alama 2)

**b)** Andika visawe vya maneno yafuatayo; (alama 2)

i)doa

ii)omba

**c)** Bainisha shamirisho na chagizo katika sentensi (alama 2)

Vibarua wamefanya kazi haraka ipasavyo .

**d)** Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo;

Hawa ni watoto wa marehemu Bwana Ndovu na Bi.Makombo (alama 2 )

**e)** Eleza matumizi ya alama ya ritifaa kwa neno lifuatalo;N'shamchukua (alama 2)

**f)** Eleza mofimu katika neno lifuatalo (alama 3)

Walichokilalia

**g)** Bainisha vitenzi vilivyo katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Kalamu aliyokuwa nayo mwalimu ni ya mwanafunzi.

**h)** Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari au mishale (alama 4)

Chakula kitamu kimeandaliwa.

**i)** Huku ukitoa mifano mwafaka onyesha matumizi matatu ya kinyota katika sentensi. (alama 3)

**j)** Tunga sentensi moja ukitumia kielezi cha wakati na kielezi cha mahali. (alama2)

**k)** Toa mfano wa neno lenye muundo ufuatao wa silabi. (alama 1)

IK+KI+KI+KI

**l)** Onyesha matumizi ya viakifishi vifuatavyo. (alama 2)

i. kibainishi
ii. parandesi

**m)** Tumia neno –baya kama: (alama 2)

i. Kiwakilishi
ii. kielezi

**n)** Tunga sentensi sahili ukitumia kitenzi 'la' katika kauli ya tendewa. (alama 2)

**o)** Unganisha sentensi zifuatazo ukitumia neno japo;

i. Selina alijitahidi sana.
ii. iSelina hakushinda mbio hizo.

**p)** Kwa kuzingatia maagizo andika upya sentensi ifuatayo: (alama2)

i. Tinga amewafanya ng'ombe wake wanywe maji.
ii. (Anza kwa : Mifugo wangu …………..usitumie 'amewafanya')

**q)** Tunga sentensi moja yenye nomino dhahania na kivumishi kimilikishi. (alama 2 )

**r)** Bainisha maana mbili zinazojitokeza kutokana na sentensi hii. (alama 2)

Umu alimwandikisha mkewe.

**s)** Onyesha dhamira ya sentensi hii; (alama 1)

Huenda mvua ikanyesha leo

## 4. ISIMUJAMII **(Alama 10)**

Kumekuwa na mijadala mingi kuhusu athari ya chanjo dhidi ya ugonjwa unaosababishwa na virusi vya Kovid-19.Wewe ni Afisa wa afya katika eneo lenu umealikwa kutoa hotuba kuhusu usalama wa chanjo hii .Eleza sifa kumi za lugha utakayotumia.

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: ……………………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ………………DARASA: …...........**

# SHULE YA UPILI YA MOI GIRLS ELDORET

**102/2**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA PILI**

**Maagizo**

a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

c) *Jibu maswali **yote**.*

d) *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

e) *Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*

f) *Karatasi hii ina kurasa **10** zilizochapishwa.*

g) *Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| **Swali** | **Upeo** | **Alama** |
|---|---|---|
| **1** | **15** | |
| **2** | **15** | |
| **3** | **40** | |
| **4** | **10** | |
| **Jumla** | **80** | |

**1. UFAHAMU** **ALAMA 15**

*Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali*

Katini alinitazama kwa muda , alinijibu, 'Ndio alioa. Lakini unajua wanawake wa siku hizi walivyo; hawana moyo wa kumlea mwana wa mwenzao. Wanachelea kwamba ule ugwe uliowaunganisha baba na mama mtoto utamea tena. Wanasema kwamba kumlea mtoto wa mwanamke mwingine ni kuhatarisha masilahi yao katika ndoa.'

"Usimulizi wa Katini ulinikatisha tamaa zaidi. Nilijua kwamba hata nikamtafuta mama, huenda naye ameolewa na katika jamii yetu nasikia mtoto ni wa baba. Kwa hivyo, hata huko alikoolewa mama sitakuwa na hadhi yoyote, nikaona nitachukuliwa kama mpitanjia aliyekuja kuvuruga utulivu wa familia yao. Moyo uliniambia niende kwa shangazi yangu, lakini nilijikanya. Nilijiuliza, 'Ikiwa baba na mama hawawezi kunilea, sembuse shangazi? Haihalisi kumwongezea Shangazi Waridi mzigo. Hapo alipo hata ndiye anayegharamia masomo yangu kwa kidogo anachokipata kutoka kwenye vikataa vyake.

**Nilipiga moyo konde**, nikazidi kujiambia, ' Binadamu aliumbwa kupambana na ulimwengu na kutumia rasilimali aliyopewa na Mungu kuyaboresha maisha yake, najua nimepewa akili razini, nina azma ya kujiendeleza masomoni. Najua nitahitimu masomo yangu siku moja na kurudi hapa hapa petu kupajenga upya. Sitarajii kutatokea mtu kunyakua ardhi hii ambapo nimemzika mpenzi nyanya yangu.

Ari hii ilinifanya nijitome kwenye njia nisiyojua kikomo chake. Akili na miguu yangu ilinielekeza katika kijiji kimoja wanakoishi wafanyakazi wa shamba la chai la Shirika la Chai la Tengenea. Kiwanda hiki kinamilikiwa na Mzungu mmoja aliyekuwa mlowezi nchini. Mzungu huyu kwa jina Richard aliaga mara tu baada ya Uingereza kuikabdhi nchi hii uhuru. Hata hivyo, familia yake bado inamiliki shamba hili, kama Wazungu wengine wanavyomiliki mashamba ya michai na mibuni, pamoja na mashirika mengi ya utengenezaji wa mazao ya mimea hii nchini. Kining'inya ya Richard ndiye Afisa Mkuu Mtendaji wa shirika hili hivi sasa.

Ukiniuliza ni kwa nini niliamua kuja hapa nitakwambia kwamba nilijua pana shule hapo hapo shambani. Pili, nilijua kwamba iwapo ingetokea kwamba singekuwa na wa kuyakidhi mahitaji yangu ya kimsingi, nyanya yangu alikuwa amenifunza umuhimu wa kufanya kazi. Hapo shambani ningeweza kuchuna majanichai Jumamosi na hata wakati wa likizo ili kujikimu.

Asubuhi moja ilinipata ndani ya ofisi ya mwalimu mkuu wa shule ya Msingi ya Kilimo. Mwalimu Mkuu Bi. Tamasha, alisikiliza **kadhia** yangu kwa makini . Hakuonyesha kushtuka kwa yaliyonipata katika umri wangu mdogo hivi. Aliniambia kwamba ningeweza kuanza masomo katika darasa la pili. Aliniahidi kuwa angemwomba mzazi mmoja anipe hifadhi. Huo ukawa mwanzo wa maisha yangu mapya katika makao ya wafanyakazi wa mashamba ya chai. Nilichukuliwa na familia ya Bwana Tenge na mkewe Kimai na kunilea pamoja na watoto wao watano. Wenzangu, nyinyi hamjui adha zinazowapata wafanyakazi wa kima kidogo. Mtajuaje na hamjawahi kukilalia kitanda hiki mkawajua kunguni wake? Chumba cha wafadhili wangu kilikuwa hichohicho kimoja; ndicho cha malazi, mapokezi na ndicho jikoni. Sebule na chumba cha malazi viligawanywa

na shuka moja nyepesi. Usiku sisi watoto tulilala juu ya vigodoro ambavyo ni kama viliwekwa mvungni mwa kitanda cha wazazi.

Nilianza kuchuna majanichai kwa malipo kidogo nikiwa katika darasa la tano. Wakati mwingine ningerauka alfajiri na mapema kabla ya kwenda shuleni saa kumi na mbili asubuhi. Jioni nilipita huko huko. Nyakati nyingi nililala humo humo katikati ya michai, wakati mwigine kwa marafiki wangu, kwa Bwana Tenge, na juu ya uchaga mkubwa wa saruji uliotumiwa kama karo na wauza chakula sokoni. Hakuna hata mmoja kati ya walimu wangu aliyejua mabadiliko haya hadi pale nilipounfanya mtihani wangu wa darasa la nane na kufuzu vyema.

**Maswali**

a) Eleza kwa kutoa hoja tano, adha zinazomkumba msimulizi katika taarifa hii. (alama 5)

b) “ Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi, ” Thibitisha kauli hii ukirejelea kifungu hiki. (alama 2)

c) Taja methali moja inayodokezwa katika taarifa hii. (alama 1)

d) Kwa kutoa hoja tatu, eleza kinaya katika kauli “…baada ya Uingereza kuikabdhi nchi hii uhuru.” (alama 3)

e) Thibitisha kuwa msimulizi ni mkakamavu. (alama 2)

f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika kifungu. (alama 2)

i) Nilipiga moyo konde

ii) kadhia

## 2. UFUPISHO ALAMA 15

*Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.*

Chambilecho wahenga, mgaagaa na upwa hali mkavu.Walio na bidii katika jambo fulani mwishowe hufaulu na kufurahia matunda ya bidii zao. Kufaulu huku kwao huwavutia watu wengi kwa sababu wanakuwa kielelezo cha kuigwa na watu hao. Watu wengi waliofaulu katika maisha wana historia ya kufanya bidii na kujitolea kwa udi na uvumba katika majukumu au masomo yao. Ben Carson ni mmoja kati ya watu waliofaulu duniani na kuwa tabibu wa kutajika.Ben alizaliwa katika familia iliyokuwa na changamoto kadhaa. Alipojiunga na shule, alikuwa na matatizo ya kufanya vizuri shuleni.Mara nyingi alikuwa wa mwisho katika mijarabu shuleni. Hata hivyo Ben hakutamauka.Aliamua kutia bidii na kujizatiti katika masomo yake.Baada ya muda,alikuwa bingwa katika masomo yake ambapo baadaye aliibuka kuwa daktari maarufu sana duniani.

Akiwa mwanafunzi katika shule ya upili ya Kagumo, Daktari James Mwangi hakujua kuwa siku moja atakuja kubadilisha maisha ya maelfu ya wanafunzi kutoka katika shule mbalimbali kote nchini kupitia mpango maarufu wa *'Wings to Fly'* unaodhaminiwa kwa kiasi kikubwa na Benki ya Equity. Mradi huu wa mabilioni ya pesa unahusu ufadhili wa wanafunzi werevu hasa kutoka katika familia zisizojiweza. Wanafunzi hawa wamepata nafasi ya kuendeleza masomo yao hadi katika vyuo vikuu vya humu nchini na pia vya huko ughaibuni. Baadhi ya vyuo hivi ni kama kile cha Harvard, Yale, MIT na vinginevyo maarufu kote duniani. Wanafunzi hawa huweza kupata mafunzo katika taaluma mbalimbali kama vile Utabibu, Uhandisi, Uchumi, Usanii na kadhalika.

Katika mwaka wa 2013, Benki hii ya Equity iliwafaidi takriban wanafunzi 5,000 kutoka katika kila eneo la nchi hii tukufu. Wanafunzi hawa wanalipiwa karo yote kulingana na kiasi kinachohitajika kwa kiwango cha shule husika.Hii ni kwa sababu kuna shule ambazo hutoza karo ya juu hasa zile za kitaifa ikilinganishwa na shule zisizo za kitaifa. Fauka ya hayo, wanafunzi hawa hupewa masurufu itakayowakimu wakati wote wa muhula watakapokuwa wakiendeleana masomo yao. Wanafunzi pia hunufaika na nauli ya kwenda nyumbani mwishoni mwa mihula yao. Iwapo watahitajika kwenda nyumbani wakati wa mapumziko ya katikati ya muhula, benki hii vilevile huwapa nauli.

Benki hii hufanya hivyo ili kuonyesha umuhimu wa wanafunzi kufanya bidii katika masomo yao. Bidii hii inahitajika katika daraja zote za elimu, zikiwemo, shule za msingi na katika shule za upili. Wanafunzi wengi werevu ambao wangepoteza nafasi zao za kuendelea na masomo yao wamenusuriwa na mpango wa benki na kupata nuru ya maisha ya baadaye. Iwapo nchi hii ingekuwa na watu kumi walio na maono kama ya Daktari James Mwangi basi nchi hii ingekuwa imepaa na kuambaa katika elimu na kunawiri katika uchumi. Katika kitengo hiki, tuna msaada kutoka kwa Benki ya Ushirika na pia ile ya Family.

Wakfu wa Jomo Kenyatta Foundation ni mfano mwingine wa watu waliojitolea kuimarisha masomo ya wanafunzi werevu kutoka katika familia zisizojiweza hasa katika shule za upili. Wao pia wamejizatiti kuwalipia wanafunzi hao karo na kuwafadhili katika masomo yao kwa njia nyingine nyingi ili kuhakikisha kuwa azma ya wanafunzi hawa inaafikiwa katika maisha ya baadaye.

Mashirika mengine pia yamejitolea katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapaa katika maisha yao kwa kukuza masomo yao au talanta za watoto hao. Kampuni za maziwa kama vile Brookside, kampuni ya Milo, watengenezaji soda wa Cocacola na wengine wengi pia wamejizatiti katika kuboresha maisha ya wanafunzi. Kampuni hizi huchangia katika kudhamini michezo baina ya shule za upili kama vile ile ya kitaifa kila mwaka. Michezo hii huhusisha soka, raga, mpira wa nyavu, riadha, magongo na kadhalika. Mashirika haya hukusudia kuhimiza bidii katika kukuza vipawa kama vile michezo miongoni mwa wanafunzi katika shule za upili. Vipawa hivi huhitaji bidii na ndiposa walio na bidii huvuna matunda ya bidii yao na wao huweza kupaa na kuwanda katika maisha ya sasa na yale yajayo.

Ni matumaini yangu kuwa wanafunzi wengi watajizatiti katika masomo yao na pia katika kukuza michezo ili waweze kupaa na kuwanda katika maisha ya hapo baadaye. Tunawahimiza wanafunzi wanaotoka katika familia maskini kujiamini na kutia bidii katika masomo yao ili waweze kutambuliwa na mashirika kama haya ili waweze kusaidiwa wawe watu watakaofanikiwa katika maisha yao ya usoni. Ili waweze kunawiri na kupaa, basi bidii katika masomo yao na katika masuala mbalimbali ya maisha ni lazima izingatiwe kwa kina.

Maswali

a) Fupisha aya nne za mwanzo bila kupotosha maana kusudiwa kwa maneno 80. (alama 7, utiririko 1)

b) Fupisha aya tatu za mwisho bila kubadili maana kusudiwa kwa maneno 60. (alama 6, utiririko 1)

## 3. MATUMIZI YA LUGHA ALAMA 40

a) Andika neno lenye muundo ufuatao wa sauti. (alama 1)

kitambaza+irabu ya mbele juu+nazali ya ufizi+kipasuo ghuna cha ufizi+irabu ya chini

…………………………………………………………………………………………………………………

b) Onyesha miundo ya silabi katika neno; (alama 1)

machweo

…………………………………………………………………………………………………………………

c) Tofautisha maneno haya kwa kutia shadda. (alama 2)

i) Ala (kifaa)

…………………………………………………………………………………………………………………

ii) Ala! (mshangao)

…………………………………………………………………………………………………………………

d) Tunga sentensi moja katika hali ya mazoea wakati uliopita. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………………

e) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo: (alama 2)

Wanafunzi waliamka walipomsikia mwalimu akiingia darasani.

…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………

f) Kanusha sentensi ifuatayo: (alama 2)

Chakula kilikuwa kimepikwa na mama.

…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………

g) Tumia kiwakilishi cha pekee chenye dhana ya kusisitiza katika ngeli ya U-ZI. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………

h) Andika katika wingi; (alama 2)

Ua wa shule yetu utakarabatiwa upya.

…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………

i) Akifisha ili kuonyesha usemi halisi. (alama 2)

daudi tutafumukana baada ya ibada

…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………

j) Tumia neno ‘salamu’ katika sentensi kama kitenzi. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………

k) Ainisha yambwa na chagizo katika sentensi ifuatayo: (alama 3)

Mkulima alichimbiwa shamba lake kwa uma jana.

…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………

l) Andika visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 3)

<u>Rafiki</u> yangu <u>mvulana</u> alilia kwa <u>hasira</u>.

…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………

m) Changanua kwa njia ya jedwali. (alama 4)

Wahunzi waliokuwa kiwandani juzi walilipwa mishahara yao kwa hundi.

…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………

n) Eleza matumizi ya **ji** katika sentensi ifuatayo; (alama 2)

Wachezaji wetu walijistarehesha uwanjani.

…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………

o) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo; (alama 2)

Wazee wataenda kwao baada ya kazi za mchana kutwa.

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

p) Tumia kitenzi **–w-** katika kauli ya kutendea katika sentensi. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

q) Bainisha viambishi katika fungutenzi; (alama 3)

waliofiwa

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

r) Tunamwambia mtu makiwa anapofiwa, …………………………….. kuonyesha dharau na……………………….kukubaliana na jambo. ( alama 2)

s) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo; (alama 2)

Vyovyote vizuri vitakubalika baada ya kununua gari jipya.

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

## 4. ISIMUJAMII ALAMA 10

"…. Anakwenda, anaenda, anaenda ndiye huyooo…. Hatari kwenye lango la Masimba! Salaaaaale! Amepiga miss kubwa ajabu… nyani naye yuko macho…!"

a) Tambua sajili ya muktadha huu. (alama 2)

b) Fafanua sifa nane za sajili hii. (alama 8)

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: ……………………………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ………………DARASA: …...........**

# MTIHANI WA PAMOJA WA KAUNTI YA NAIROBI

**102/2**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA PILI**

**MAAGIZO**

***a)*** *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***b)*** *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***c)*** *Jibu maswali* ***yote.***
***d)*** *Majibu yako yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
***e)*** *Majibu yote* **lazima** *yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
***f)*** *Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*
***g)*** ***Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

**Kwa matumizi ya mtahini pekee.**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | **15** | |
| 2 | **15** | |
| 3 | **40** | |
| 4 | **10** | |
| **Jumla** | **80** | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**UFAHAMU** (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Muuguzi Salina Jeruto ambaye aliuawa na majangili mnamo jumanne katika kaunti ndogo ya Marakwet Mashariki, alikuwa amehepa kifo mikononi mwa wahalifu hao mara nyingi siku za awali. Bi. Jeruto, aliyekuwa na umri wa miaka arubaini na tano, alikuwa muuguzi katika hospitali ya Endo na alikuwa amenusurika kifo wiki moja iliyopita baada ya majangili kuvamia boma lake na kisha kutoweka na mbuzi arobaini. Wakati wa uvamizi huo Bi. Jeruto aliyekuwa muumini wa kanisa katoliki aliinua rozari yake na kumuomba Mungu anusuru maisha yake.

Hali imekuwa hivyo kwa miaka kadhaa ambapo amekuwa akinusurika kifo wakati wa uvamizi wa majangili hao ambao hubeba silaha kali. Muuguzi huyo hakuwa na bahati Jumanne baada ya majangili kumakabili akielekea nyumbani kwake kutoka shambani ambapo alikuwa ameeenda kuchuma mboga. Kifo chake kilifikisha vifo vinavyosababishwa na majangili katika Bonde la Kerio hadi saba, siku nne zilizopita. Mhudumu wa maabara pia aliuawa katika eneo la Kapkata, Arror Marakwet Magharibi.

Majangili hao walitekeleza uvamizi katika maeneobunge ya Marakwet Mashariki na Magharibi. Kwa mujibu wa binamu wa Bi. Jeruto, Stephen, marehemu alikuwa ameponyoka kifo kila mara uvamizi ulipotekelezwa na majangili hao. Alisema marehemu alikuwa amejitolea sana katika kazi yake, msalihina aliyekuwa akijali familia na watu wengine aliokuwa akiwapa msaada.

“Alipokabiliwa na majangili hao, kama kawaida yake aliinua rozari yake na kuanza kuomba. Majangili walijaribu kumfyatulia risasi mara mbili ila ikafeli. Ni katika jaribio la tatu ambapo ilimpata mguuni na nyingine tumboni. Alikufa kama ameshikilia rozari yake,” akasema Bw. Stephen.

Bi. Salina alikuwa mchapakazi hasa akishiriki ufugaji na pia kilimo cha mazao ambapo alipanda ndizi, nyanya na mboga kati ya mimea mingine. Kwa mujibu wa mtawa Lioba Kibor anayesimamia hospitali ya misheni ya Endo, Bi. Jeruto alibaki huku wahudumu wengine wakitoroka eneo hilo kutokana na ukosefu wa usalama. Hii ilikuwa kutokana na msukumo ndani yake ya kuhudumia jamii. “Kwetu alikuwa mtu aliyependa kazi yake na alikuwa na moyo wa upendo. Katika kazi yake alizingatia sana maslahi ya kijamii,” aliongeza mtawa.

Familia ya Bi. Jeruto nayo ilisema kuwa hakuwa ameolewa ila alikuwa akiwakimu watoto wanane na zaidi kutoka familia maskini pamoja na wakongwe ambao hawajiwezi. Licha ya kuwa na kisomo cha msingi pekee, Bi. Jeruto alifundishwa ukunga mnamo 1991 na wamishenari ambao walitambua juhudi zake za kusaidia jamii. Kutokana na umahiri wake, alipanda ngazi hadi kuwa muuguzi ambaye alikuwa amewahudumia wagonjwa kwa miaka thelathini na moja. Pia wamishenari hao walimfundisha neno la Mungu na alikwa akiwahubiria wenyeji mara kwa mara.

Haya yanajiri wakati ambapo viongozi wa kaskazini mwa Bonde la Ufa wanataka jeshi litumwe kupambana na majangili hao badala ya polisi wanaoongoza oparesheni ya sasa. Wanasiasa hao wanasema kuwa licha ya juhudi za polisi zinazoendelezwa katika oparesheni ya sasa, bado mauaji yanaendelea kuripotiwa katika maeneo mbalimbali.

Mauji hayatokani na majangili tu, kuna vifo vitokanavyo na ajali viwandani. Wafanyakazi katika kampuni ya sukari ya Mumias, wamefichua kuwa wanafanya kazi katika mazingira duni. Wanalalamika kwamba baadhi yao wameumia wakifanya kazi huku wakilipwa mishahara duni. Wafanyakazi zaidi ya mia mbili walioajiriwa na Kundi la Sarai ambalo linasimamia kampuni hiyo wanataka serikali kuingilia kati ili kuwaokoa kutoka kwa ghadhabu ya mwekezaji huyo. Walisema kwamba baadhi ya wafanyakazi katika kampuni hiyo wamekufa kutokana na mazingira yasiyo salama.

Mnamo Agosti 2022, Dickson Inganga, wa umri wa miaka hamsini na nne, alifariki baada ya kuteleza na kuanguka kwenye tanki la kemikali katika kiwanda hicho. Familia yake ilisema bado hawajalipwa fidia kwa kufiwa na mpendwa wao.

“Tunaomba serikali iingilie kati ili kutusaidia kupata haki kwa kifo cha mume wangu,” akasema Beatrice Inganga.

Mnamo Januari, mwanaume mmoja alikufa kwenye uwanja wa miwa baada ya kuangukiwa na trekta iliyokuwa ikisafirisha miwa.

**MASWALI**

a) Uhalifu una maafa chungu nzima. Kwa mujibu wa kifungu toa hoja **tano**. ( alama 5)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………

b) Andika mambo **matatu** yanayoonyesha kuwa Salina alikuwa mwenye imani. ( alama 3)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………

c) Kando na vifo vinavyosababishwa na majangili, taja visababishi vingine vya vifo kwa kurejelea kifungu. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………….……………..

d) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu. (alama 3)

i) Msahilina …………………………………………………………………………….

ii) Fidia ……………………………………………………………………………………….

iii) Anusuru ……………………………………………………………………………………

e) Kipe kifungu hiki anwani mwafaka. (alama 1)

………………………………………………………………………..……………………………

**UFUPISHO** (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Katika umbali wa takriban kilomita sitini kutoka jijini Nairobi, shamba moja la ufugaji samaki linatambulika kwa wengi. Shamba la samaki la Kumuthanga ndilo linalojulikana kwa ufugaji wa samaki kwa kutumia teknojia ya kisasa, linapatikana katika eneo la milima ya Mua, kaunti ya Machakos. Anthony

Ndeto ni mmiliki wa shamba hilo, ambalo ni la kwanza katika eneo la Afrika Mashariki na Kati kuidhinishwa na kukabidhiwa cheti cha Chama cha Kiafrika ya ubora (ARSO) 2019. Ndeto alijitosa katika ufugaji wa samaki 2013. Shamba lote ni ekari tano na lina sehemu ya kuwazalisha samaki wa kiume kwa kuitumia teknolojia ya inayojulikana kama *super male* ama YY. Teknolojia hiyo ni ya kuwazalisha samaki wa kiume pekee.

Hapo awali samaki walikuwa wakizalishwa wakitumia homoni ambazo zinageuza jinsia ya samaki wa kike kuwa wa kiume. Hata hivyo, meneja wa samaki katika shamba hilo, Joseph odhimabo, anasema kuwa, waliacha kutumia homoni, na kwa wakati huu huleta mbegu za samaki kutoka uholanzi. Wakati walipokuwa wakianza hawakuwa wakizalisha samaki kwa kiwango cha juu sana, na walipitia changamoto kadhaa. Hata hivyo, walianza kushiriakina na shirika la chakula cha kiteknolojia Afrika (*FoodTechAfrica*), shirika kutoka uholanzi.

Wakati ushirikiano huu uliopoanza mnamo 2014-2018, shamba hili likawa na uwezo wa kuzalisha mara thelethini zaidi, kwa sababu kwa wakati huo walikuwa wakivua samaki chini ya kilo elfu tano kwa mwaka, na kwa wakati huu wanaweza kupata samaki tani mia moja. Mwanzoni, walikuwa wakitumia vidimbwi katika maeneo yaliyokuwa wazi, lakini kwa wakati huu hutumia majengo makubwa yaliyo na matangi hamsini. Matangi hayo yalijengwa kwa kutumia saruji. Kila tangi lina maji elfu hamsini. Kila moja hutoa tani elfu tatu za samaki. Karibu nusu yao wanatumika kwa sasa, lakini tuna mipango ya kuhakikisha kuwa yote yanatumika. Tunawafuga samaki elfu ishirini kwa nafasi ndogo ya mita tano mraba yenye kina chenye fiti mbili na nusu. Huwalisha kila baada ya saa mbili usiku na mchana.

Meneja wa shamba hili Odhiambo anasema kuwa, kwa kawaida katika ufugaji wa samaki, watu huruhusiwa kuwafuga samaki wanne kwa sehemu iliyo na ukubwa wa mita moja mraba, lakini kwa teknolojia hii, imewawezesha kuwafuga samaki mia moja thelathini na tano kwa mita moja mraba. Anaendelea kusema kuwa, maadamu wanatumia majengo makubwa yanayofanana na vivungulio, wana uwezo wa kudhibiti hali ya hewa ndani, na hivyo kuwa na uwezo wa kuzalisha kila wakati pasi na kukosa kuwawasilisha sokoni. Iwapo hali joto ziko chini, uzalishaji huchukua muda mrefu sana, ilhali wakati hali joto zinapokuwa juu, samaki hukua haraka mno.

Kuna lori ambalo huwasafirisha samaki walio hai sokoni. Wao pekee ndio wanaowauza samaki hai katika eneo la Nairobi meneja huyo alisema. Aliongeza kuwa lengo kuu kwao ni kuwauza samaki walio hai sokoni. Anaongeza kuwa wakulima wengi hupenda kuwafuga samaki wa kiume kwa sababu hukua upesi ikilinganishwa samaki wa kike na hivyo hao hupata hela haraka kwa kuwafuga wa kiume. Meneja huyo alitufichulia kuwa wao hununua lishe kutoka nchini Misri kwa sababu si ghali na ni za kiwango cha juu.

Changamoto kuu kwao ni gharama ya juu ya uzalishaji. Changamoto nyingine ni bili za juu za stima. Odhiambo alisema kuwa uuzaji wa samaki kutoka China, pia huwaathiri wafugaji wa humu nchini, na hivyo serikali inafaa kulingazia swala hilo.Hata hivyo, anasema kuwa samaki wao hawawezi kulinganishwa na wale wanaoletwa kutoka China kwa sababu wanaoletwa kutoka china huwa wamekaushwa ilhali wanaozalishwa katika Shamba la samaki la Kumuthanga huuzwa wakiwa hai. Kwa wakati huo, shamba hilo lina wafanyakazi kumi na watatu kwa idara ya samaki, na kwa kuwa kuna shughuli zingine za kilimo shambani kama vile ufugaji wa nguruwe, kuku na ukuzaji wa mimea ya mboga, wafanyakazi wote wanaweza kufikia arubaini kwa idadi. Shamba hili linapania kuongeza kiwango cha uzalishaji maradufu ifikapo 2025.

a) Fupisha ujumbe wa aya tatu za kwanza kwa maneno 95-100. (alama 8)

Matayarisho

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………..……...

Nakala Safi

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

Eleza masuala yanayojitokeza katika aya mbili za mwisho kwa maneno 80-85.(alama 7)

Matayarisho

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

Nakala Safi

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………

**MATUMIZI YA LUGHA** (Alama 40)

a) Andika sauti zenye sifa zifuatazo. (alama 1)

i) nazali, kaakaalani …………………………………………………………………

ii) mbele juu, tandazwa ……………………………………………………………….

b) Tunga neno lenye muundo wa silabi ufuatao. (alama 1)

K-KKI-KKI-KI-KI ………………………………………………………………………

c) Weka shadda katika maneno yafuatayo. (alama 1)

tulimchosha …………………………………………………………………………….

magharibi ……………………………………………………………………………..

d) Ukitumia mifano mwafaka onyesha matumizi mawili ya alama ya vifungo. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………..

e) Tunga sentensi moja yenye kirejeshi ambacho ni kivumishi . (alama 1)

……………………………………………………………………………………………….

f) Bainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Ng’ombe wangu anapaswa kuwa amekamuliwa nitakapowasili.

.....................................................................................................................................................

...........................................................................................................................

g) Kiambishi -**ku**- hutumika kuundia nomino za kitenzi-jina. Kwa kutoa mifano mwafaka eleza matumizi mengine mawili ya kiambishi hiki. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………..

h) Weka vitenzi hivi katika hali ya kuamrisha wingi. (alama 1)

-p- …..…………………………………………………………………………………..

-lim- ………………………………………………………………………………..

i) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi. (alama 2)
Daktari aliniagiza nimeze tembe tatu asubuhi, mbili mchana na moja usiku kabla ya kulala.

……………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

j) Andika sentensi ifuatayo kwa umoja hali ya mazoea. (alama 1)
Ni nyuta zipi zilinunuliwa asubuhi.

…………………………………………………………………………………………………

k) Unda nomino inayoishia kwa kiishio -e-kutoka kwa mzizi wa kitenzi ulichopewa. (alama 1)

-ham- ………………………………………………………………………………..
-umb- ……………………………………………………………………………….

l) Tumia neno **shamba** kama nomino na kama kielezi. (alama 2)

Nomino: ……………………………………………………………………………..

Kielezi: …………………………………………………………………………….

m) Ainisha mofimu katika maneno yafuatayo: (alama 3)

i) Hawakujulikana.

………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………

ii) mgeni …………………………………………………………………………………

n) Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa wingi. (alama 2)
Ngamia na mbuzi hula nyasi.

……………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

o) Badilisha sentensi ifuatayo katika wakati uliopita hali ya masharti. (alama 2)
Baba amefika shuleni mapema.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………..

p) Kanusha sentensi ifuatayo. (alama 1)
Nyati atokeapo, wakulima huhangaika.

……………………………………………………………………………………………………

q) Andika kinyume cha vitenzi vilivyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo. (alama 1)
Kijana alivaa sare ya shule na kuubana mlango.

…………………………………………………………………………………………………

r) Ainisha virai nomino katika sentensi zifuatazo. (alama 1)
Yule mkubwa sana ameshauriwa na mwalimu.

……………………………………………………………………………………………………

Bandari iliyofungwa itafunguliwa mwakani.

…………………………………………………………………………………………..

s) Ainisha vishazi huru na tegemezi katika sentensi ifuatayo. (alama 2) Alianguka vibaya alipokuwa akifanya mazoezi uwanjani usiku.

…………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………….

t) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi. (alama 4)
Mimi nakupenda ila hunipendi.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………..

u) Bainisha shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
Mamangu alimwandikia baba barua mara chache.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

v) Tunga sentensi **moja** kubainisha maana mbili za neno **mzimu**. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………

w) Una rafiki anayependa kufuata mbinu za wengine ili afanikiwe. Hana mbinu zake mwenyewe. Hutamani kila wakati kupata walichopata wenzake. Andika methali inayoweza kutumiwa kumkanya dhidi ya tabia hiyo. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………

x) Wingu ni kwa nzige,________________ ni kwa nyota na ____________ ni kwa askari. (alama 1)

**ISIMUJAMII** (Alama 10)

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

**Kenya Yaibuka Namba Wani Mbio za Nyika Duniani**

Kenya ilirejesha taji la jumla kwenye mbio za Nyika za Duniani uwanjani nchini Australia…

a) Bainisha sajili ya makala haya kwa kutoa mfano kutoka kwenye makala. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………….

b) Fafanua sifa nane za sajili ambazo zingejitokeza katika makala haya. (alama 8)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: …………………………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ………………DARASA: …...........**

# MTIHANI WA PAMOJA WA CEKANAS

**102/2**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA PILI**

**<u>MAAGIZO</u>**

***a)*** *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***b)*** *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***c)*** *Jibu maswali* ***yote.***
***d)*** *Majibu yako yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
***e)*** *Majibu yote* **lazima** *yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
***f)*** *Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*
***g) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

**Kwa matumizi ya mtahini pekee.**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | **15** | |
| 2 | **15** | |
| 3 | **40** | |
| 4 | **10** | |
| **Jumla** | **80** | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**1. UFAHAMU** **(ALAMA 15)**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Mafuta yanayopatikana kwenye fukwe za bahari, moshi wa magari, takataka na bidhaa nyinginezo zinazotupwa hapa na pale ni vichafuzi vya mazingira. Vichafuzi huathiri afya zetu na kuathiri wanyama pamoja na mimea. Wanadamu wayachafua mazingira yao kwa kila aina ya bidhaa mbaya za kikemikali zinazotoka viwandani au kwenye viwanda vya kawi au nguvu. Bidhaa hizo ni matokeo ya maisha ya siku hizi anayoishi binadamu.

Licha ya ukweli huu, ni muhimu kujua kuwa uchafuzi wa mazingira haukuanza leo. Miaka na miaka iliyopita, viwanda vimekuwa vikitoa mawingu makubwa ya moshi wenye sumu. Hata hivyo, uchafuzi wa mazingira umeongezeka maradufu kutokana na kuongezeka kwa viwanda. Uchafuzi umesambaa ardhini, kwenye anga na majini. Msambao huu unapatikana katika pembe zote za ulimwengu wetu. Je, kuna aina zipi za uchafuzi?

Kwanza kuna uchafuzi wa halianga. Huko juu angani kuna tabaka linalojulikana kama ozoni. Tabaka hili huwa ni kama gesi ya oksijeni na linaunda kinga fulani dhidi ya miale ya jua. Miale hiyo ya jua huweza kusababisha saratani ya ngozi inapomfikia binadamu. Hata hivyo, uchafuzi wa mazingira unaelekea kiliathiri tabaka hili. Vilevile baadhi ya kemikali zinazotumiwa katika friji au jokofu au kwenye mikebe ya marashi ya kupulizia na upakiaji bidhaa, huharibu ukanda huo.

Aina nyingine ya uchafuzi ni ile tunayoweza kuuita uchafuzi wa kiajali. Huu ni uchafuzi ambao hutokea kama ajali, yaani binadamu hatendi kimakusudi. Mfano mzuri ni meli inayovuja mafuta baharini. mafuta haya huwaathiri na kuwaua wanyama wanaoishi baharini kama samaki na ndege na hata kuyaharibu mazingira yenyewe.

Miji mikubwa hukumbwa na uchafuzi mwingine unaohusiana na kuwako kwa idadi kubwa ya magari. Magari haya hutoa moshi unaochanganya gesi ambazo huungana na nyingine zinazoletwa na viwanda vikumbwa. Mchanganyiko huu unapoungana na maji, husababisha mvua ya asidi. Mvua hii huweza kuiua mimea, kuathiri majengo na hata kuwaua wanyama pori ambao huenda wakayatumia maji hayo. Magari hutoa moshi uliochanganyika na madini aina ya risasi ambayo huweza kuathiri siyo tu mazingira bali pia mfumo wa akili wa binadamu.

Uchafuzi mkubwa unaopatikana katika mazingira mengine yetu ni utupwaji ovyo wa takataka. Fauka ya hayo, watu hufukia ardhini takataka ambazo huweza kuwa na matokeo mabaya kwa sababu ya kupenyeza kwenye udongo na maji yanayotumiwa na watu na mimea. Kila siku tunatupa takataka bila ya kujali wala kubali. Takataka hizi ni kama makopo, mifuko ya plastiki, mabaki ya sigara au maganda ya matunda. Baadhi ya takataka ni hatari kwa wanyama na nyingine huweza kusababisha majanga kama moto. Aidha, takataka hizi hufanya mazingira yetu yaonekane machafu.

Sote tunajukumu kubwa la kuchangia kupunguza uchafu wa kimazingira ya kwanza ni kuelimishana na kutambua umuhimu wa usafi wa mazingira yetu. Tunapaswa kutia takataka zetu katika vijalala maalum au mahali tunapoweza kuzichoma na kuziteketeza. Njia nyingine ni kuhakikisha kuwa tunatunza vitu kama mifuko, chupa na kadhalika ambavyo huweza kuunda upya na kutumiwa tena. Hali kadhalika, katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwapo na juhudi za kuwahimiza wenye magari kutumia mafuta ya gari ambayo hayana madini ya risasi. Kwa njia hii tutasaidia kuyaboresha mazingira yetu. Vilevile pana umuhimu wa kutilia mkazo utumiaji wa bidhaa ambazo zinaweza kuoza na kuvunjikavunjika au kusagika na kuwa sehemu ya udongo. Hatua ya kwanza ya kupambana na uchafuzi wa mazingira ni kujielimisha na kuwajibika. Kila mmoja akitoa mchango wake tutafanikiwa. Kumbuka kuwa kinga na kinga ndipo moto uwakapo.

**Maswali.**

a) Vichafuzi ni nini? (alama 1)

b) Ongezeko la viwanda limechangiaje uchafuzi wa mazingira ? (alama 2)

c) Tabaka la ozoni huathiriwaje na uchafuzi ? (alama 2)

d) Athari zipi zitatokea iwapo mazingira hayatatunzwa? Fafanua. (alama 4)

e) Kwa nini miji mikubwa hukumbwa na uchafuzi kuliko sehemu zingine ? (alama 2)

f) Eleza nui mbili za uchafuzi wa mazingira zilizotajwa katika kifungu hiki. (alama 2)

g) Eleza maana za misamiati ifuatayo kama ilivyotumiwa katika kifungu. (alama 2)

i) Msambao

ii) Mazingira

**2. UFUPISHO. (ALAMA 15)**

Mwezi jana, Serikali ya kitaifa na zile za kaunti ziliwasilisha makadirio yao ya bajeti, miezi miwili kabla ya mwaka wa kifedha kuisha kama zinavyohitajika na katiba. Serikali hizo zilieleza jinsi zinavyonuia kutumia mabilioni ya pesa kufadhili shughuli zao mwaka ujao wa kifedha wa 2013/2014.

Serikali ya Rais Uhuru Kenyatta ilisema itatumia shilingi 1.6 Trilioni kufadhili maendeleo na shughuli za sekta na idara zake tofauti. Makadirio haya ambayo yaliwasilishwa na kiongozi wa walio wengi bungeni, Bw Aden Duale. Hata hivyo yalikosa kueleza jambo moja muhimu – jinsi kitita hicho kitakavyopatikana. Nasema hivi kwa sababu kuna habari ambazo zimenipa tumbojoto na wasiwasi mkubwa. Imebainika kuwa kufikia mwishoni mwa Machi mwaka huu, Kenya ilikuwa inadaiwa Shilingi 1.8 Trilioni na wafadhili wa humu nchini na kigeni.

Kama habari hizi hazijakushtua sitakulaumu kwa sababu huenda ukawa hujui ukubwa wa kiasi hiki cha fedha. Ili uweze kuelewa, nitazigawanya fedha hizi miongoni mwa wakenya milioni 40 ili tujue kila mkenya anadaiwa kiasi gani. Kila mkenya nchini, wakiwemo watoto na wazee wakongwe, anadaiwa Shilingi 45,000 ! Hivyo basi ili deni hili liweze kulipwa, kila mkenya atalazimika kutoa kiasi hicho cha fedha.

Ni deni ambalo Rais Uhuru Kenyatta alirithi kutoka kwa mtangulizi wake, Rais Mwai Kibaki ambayo utawala wake ulivunja rekodi ya kukopa. Wahenga hawakukosea waliposema dawa ya deni ni kulipa. Deni hili linapaswa kumkosesha usingizi Rais Kenyatta ambaye anapaswa kutafuta njia za kulilipa bila kuathiri uchumi, maendeleo na utekelezaji wa ahadi nyingi alizowapatia wakenya wakati wa kampeni.

Hili halitafanyika kama serikali itatenga fedha nyingi kuwalipa maafisa wake mishahara na marupurupu minono pamoja na kuwapa mabilioni ya pesa kununulia magari ya kifahari. Pengine Rais hajafahamishwa kuwa mwaka ujao wa kifedha serikali itajipata pabaya kwani Halmashauri ya ukusanyaji ushuru nchini (KRA), haitaweza kukusanya kiwango kilichowekewa na serikali baada ya shughuli ya ushuru kutatizwa na hofu iliyotanda wakati wa uchaguzi

KRA imekusanya shilingi 560 bilioni kufikia mwishoni mwa Machi ilhali ilikuwa imeagizwa kukusanya shilingi 881 bilioni.

Serikali za kaunti, ambazo zingali changa, zimependekeza kutumia mabilioni ya fedha ambazo hazitaweza kukusanya. Badala yake zimeomba serikali kuu ijaze pengo hilo au zipewe idhini ya kukopa.

Rais Kenyatta hana budi kuchukua hatua za dharura kuhakikisha kuwa wakenya hawataendelea kuandamwa na madeni maishani mwao.

**Maswali.**

a) Kwa maneno yasiyozidi 70, fupisha aya za kwanza nne. (alama 10, 1 mtiririko)

Matayarisho

Jibu

b) Kwa nini serikali haitaweza kulipa madeni yake? (maneno 40 -50) (alama 5, 1 mtiririko)

Matayarisho

Jibu

**3. MATUMIZI YA LUGHA** **(ALAMA 40)**

a) Bainisha sifa zinazotofautisha sauti zifuatazo: (alama 2)

/e/ na /u/

b) Pigia mstari silabi inayowekwa shadda katika tungo lifuatalo: (alama 1)

Walituchochea

c) Tunga sentensi moja kubainisha kiwakilishi kiambata nafsi ya kwanza wingi. (alama 2)

d) Taja matumizi manne ya kiimbo. (alama 2)

e) Tunga sentensi kuonyesha matumizi mawili ya kistari kifupi (-). (alama 2)

f) Andika katika usemi wa taarifa. (alama 4)

‘Mbona unamfanyia karaha mwenzako? Je, utaenda kumwomba radhi?’ Phanice aliuliza.

g) Andika katika hali ya mazoea. (alama 2)

Mtambo ambao unakarabatiwa leo utatufaa.

h) Andika kwa ukubwa wingi. (alama 2)

Mke wa mzee huyu hupenda mtoto huyu sana.

i) Changanua kwa kutumia mtindo wa jedwali. (alama 4)

Wazazi wengi sana waliofika shuleni mapema walileta vyakula vingi sana.

j) Yakinisha sentensi hii katika umoja. (alama 2)

Msipohama hapa hamtapewa makazi mapya

k) Onyesha kiima, chagizo na yambwa tendewa katika sentensi hii. (alama 3)

Mkulima alimfungia mwajiri ng'ombe kondeni.

l) Tunga sentensi ukitumia kitenzi 'pwa' katika kauli ya kutendea. (alama 2)

m) Eleza matumizi ya 'ji' katika sentnsi hii. (alama 2)

Mwimbaji amejikata jidole lake kwa jiwe.

n) Tunga sentensi moja ukitumia kinyume cha neno 'lewa'. (alama 2)

o) Tunga sentensi yenye kiigizi na kihusishi cha mahali. (alama 2)

p) Tunga sentensi moja kuonyesha tofauti ya maana kati ya 'guna' na 'kuna' (alama 2)

q) Ainisha vitenzi katika tungo lifuatalo. (alama 2)

Huyu alikuwa angali bwenini.

r) Unganisha sentensi hizi ukitumia kiunganishi cha kinyume. (alama 2)

Wananchi walikabiliwa na hatari

Wananchi waliendelea kuwaokoa majeruhi.

**4. ISIMUJAMII. (ALAMA 10)**

Eleza mambo matano yaliyochangia kuenea kwa Kiswahili nchini kabla na baada ya uhuru.

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: …………………………………………….NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ………………DARASA: …............**

# MTIHANI WA PAMOJA WA CRESCENDO

**102/2**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA PILI**

**Maagizo**

***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

***b)*** *Jibu maswali yote.*

***c)*** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*

***d)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. UFAHAMU | 15 | |
| 2. UFUPISHO | 15 | |
| 3. SARUFI | 40 | |
| 4. ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

**CONTACT US ON:**

WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003

EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**1: UFAHAMU: (Alama 15)**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

"Asante baba, asante mama," akasema Bahati jioni moja baada ya chajio, "Sijui ilitokeaje kukawa na watu wanaothamini binadamu wenye mahitaji maalumu katika jamii hii. Sitawauliza mlichofanya kunikinga na hukumu ya ukoo ya kuniangamiza; hayo mtakuja kunihadithia siku moja. Ila nataka mjue kwamba kuishi na ulemavu wa aina yoyote ile kuna dhiki kuu. Niliyokabiliana nayo baada ya uamuzi wenu wa kunipeleka shuleni hayawezi kutoshea hata chapisho la kurasa elfu.Si kudhihakiwa na miale ya jua; ngozi yangu inashindwa kuuhimili ukali wake, si kutengwa na marika, si kulazimika kusoma hati za kawaida hadi pale serikali ilipoanzisha sera ya kuhakikisha kwamba matini zote za kiusomi zimeandikwa pia kwa hati ambazo zinaweza kusomwa na wenye changamoto kama yangu, si kubaguliwa kazini...."Bahati alitua, akawatazama wazazi wake kama anayetaka kuona taathira ya maneno yake kisha akaendalea.

"Msinione kama aliyekosa hisani, ila' nataka niwaambie kwamba hata uamuzi wenu wa kunitafutia mlinzi kuandamana nami hadi shuleni ulinitia kwenye ngome zaidi.Nilijihisi kama niliyedhulumiwa zaidi katika kule kulindwa! Najua mlikuwa mnachelea kwamba ningekuwa windo rahisi kwa walanguzi wa binadamu ambao wanaamini kwamba viungo vyetu sisi ni dawa ya kutibia ndwele mbalimbali.Hata hivyo, katika kipindi chote hicho nilitamani kwamba mngenifunza mbinu za kujilinda mimi binafsi. Amini usiamini hata nilitamani kwamba ningetekwa nyara, nijadiliane na watesi wangu kuliko kupokwa nafasi ya kubuni mikakati ya kujihakikishia usalama".

"Mwanangu Bahati," alisema mume wangu, "binadamu hawi jagina kwa kuzifuata tamaduni za jamii yake bila kuzichunguza. :haidhuru kwamba ilichukua muda kuyangamua haya'. La muhimu ni kwamba umeweza kuishi kama ndugu zako".

Nilimtazama mume wangu kwa macho yaliyokuwa yamepofushwa na dimbwi la machozi. Moyo uliituma akili yangu kurudi nyuma kule -e-e-e- kwenye miereka ya baada ya kuzaliwa kwa Bahati. Asubuhi hiyo ya kipupwe nilishika ujia ulioelekea kwenye msitu uliokuwa karibu na boma la Mzee Kedi, baba mkwe wangu; mgongoni nimeifungia mbeleko ambayo ilikisitiri kitoto changu. Nilitazama nyuma, nikaiona nyumba ambayo mimi na mume wangu tulikuwa tumechanga bia kuijenga.

"Haya yote nayaacha," nilijiambia, "nayaacha na mengine mengi. Nawaacha mabinti wangu wawili, namwacha mume wangu, naiacha kazi yangu, nayaacha maisha yangu wala sijuti kwa

kuyaacha haya yote. Sina cha kujutia kwani imebidi kuondoka. Jamii yangu imenitema; mimi na mwanangu.Haina nafasi ya mwanangu, kwa hivyo nami nimeamua kwamba haina nafasi yangu kwa vile imesema huu ni mzigo wangu. Ikiwa ukoo umeamua kuwa hatima ya mwanangu huyu ni kuwa kitoweo cha fisi, basi na tuwe sote karamu ya fisi" nilitamatisha kauli yangu kisha nikayarudisha nyuma tena mawazo yangu.

Nilikumbuka sauti ya muuguzi hospitalini siku ambayo nilijikopoa, "Pongezi Tamasha, Mungu amekutunukia kipusa". Nilikifunua kitoto changu kilichokuwa kimefunikwa gubigubi, nikakitazama viguu, vikono, uso...kisha, 'Mungu wangu!' ikanitoka. "Dadangu, unastahili kumshukuru Mungu," akasema muuguzi, "wapo wanawake, mimi mwenyewe nikiwemo, ambao hawajawahi kuambulia ujauzito, sikwambii hata kupoteza mimba.Huyu wako ni kiumbe kamili, kasoro yake i kwenye ngozi tu, na hii ni hali ambayo unaweza kukabiliana nayo. Hapa unionapo nimelazimika kumpa mume wangu talaka, mwenyewe alienda kortini akaiomba. Anadai kwamba hatusikilizani. Ila najua kiini cha haya yote ni kutoshika kizazi".

Nilimtazama huyo muuguzi kana kwamba hajasema lolote. Nilimwona kama anayeuona mzigo wangu kuwa kanda la usufi. Huenda huyu muuguzi hakujua kwamba katika jamii yangu watoto wa aina hii ni kama pacha, huaminiwa kuwa nuksi kwa ukoo mzima, kwa hivyo hutupwa. Muuguzi huyu hakujua pia kwamba tayari nilikuwa na watoto wawili wa kike na huo tayari ulikuwa mzigo mkubwa kwangu kwani ilibidi kumhakikishia mavyaa kila mara kwamba hawa pia walikuwa watoto.

Moyo ulinipa kukumbuka jitimai iliyojiandika usoni mwa mume wangu asubuhi hiyo alipokuja hospitalini. Alikitazama kitoto chetu kana kwamba anaona mzuka. Alinyamaza kwa muda, akashusha pumzi, kisha akanishika kwenye bega na kuondoka kwenye wodi. Machozi yalivunja kingo zake huko yanakohifadhiwa, nikalia kama mfiwa, Mume wangu alirudi tena baada ya siku mbili; anakuja kunipeleka nyumbani.

"Mke wangu, naomba msamaha kwa kutokuja kuwatazama kwa siku mbili. Ilibidi nishauriane na ukoo kuhusu tanzia hii. Inavyoonekana ni kwamba msimamo wa baba na wazee wengine ni ule ule. Wanasema ukoo wa Baulanga haujawahi kupata mtoto wa aina hii, kwamba kumhifadhi mwana huyu kutakuwa kuupaka masizi ukoo. Wahenga hawatakubali tendo hili. Sijui nitakutetea vipi.Nimo kwenye njia panda," mume wangu alikamilisha uzungumzi wake na kuelekea kwenye afisi ya mhasibu kukamilisha viviga vya kutuondoa hospitalini.

“Huna haja ya kuniitetea. Sijafanya kosa lolote. Nililofanya ni kujaliwa kiumbe ambaye anaonekana kuwa punguani kwa misingi ya jamii yako. Nitakilinda kitoto hiki hata kifoni,” nilimwambia mume wangu mawazoni.

(a) “Kufanikiwa kwa watu wenye mahitaji maalumu kunategemea jamii.” Thibitisha kwa kutoa hoja sita kutoka aya tatu za kwanza. (alama 6)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(b) Kwa kurejelea aya ya nne hadi ya saba, onyesha jinsi unyanyasaji wa kijinsia unavyoendelezwa katika jamii hii. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(c) “Msimulizi anahimiza. uwajibikaji.” Thibitisha kwa kutoa hoja nne kutoka aya tatu za ‘ mwisho. (alama 4)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(d) (i) Andika kisawe cha, ‘hisani’ kwa mujibu wa taarifa. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(ii) Eleza maana ya, ‘kuupaka masizi’ kulingana na taarifa. (alama 1)

**2 UFUPISHO (Alama 15)**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Wakenya walipoipata katiba mpya waliidhinisha mfumo wa ugatuzi. Katika mfumo huu, mamlaka ya serikali kuu katika uongozi, usimamizi na utumiaji wa rasilimali za nchi hupunguzwa. Kiasi Fulani cha mamlaka hutwaliwa na maeneo ya ugatuzi. Suala hili halikuzingatiwa katika katiba ya awali ambapo mamlaka yote yalikuwa mikononi mwa serikali kuu. Kutokana na upana na wingi wa maeneo, iliiwia vigumu serikali kuu kuhakikisha kwamba kulikuwa na usawa wa kimaendeleo katika sehemu nchini.

Kwa mujibu wa katiba mpya, serikali kuu haina budi kuyasaidia maeneo yote ya ugatuzi ili yaweze kujinyanyua kiuchumi na kuboresha hali za maisha za wakazi wake. Vilevile ni jukumu la kila eneo la ugatuzi kuweka mikakati madhubuti ili kuchunguza na kubainisha rasirimali zote katika maeneo husika. Hili litasaidia kufumba rasilimali ambazo zinaweza kuchangia katika ustawishaji wa maeneo haya. Maeneo haya pia yanatakiwa kutafuta mbinu zitakazofanikisha uzalishaji na utumiaji wa rasilimali hizi kwa njia endelevu. Mojawapo ya mbinu hizi ni uongezaji thamani katika rasilimali yoyote inayozalisha kwenye eneo mahususi.

Maeneo mengi  ya ugatuzi nchini humu yanategemea kilimo cha ufugaji kama mhimili wa uchumi. Licha ya kuwa nguzo, kilimo hiki hakijawahi kupigiwa darubini vizuri kwa lengo la kukiimarisha ili kiwanufaishe wenyeji kikamilifu. Aghalabu wafugaji wengi huandama mbinu za jadi za ufugaji ambazo haziwahakikishii ongezeko la mapato.Isitoshe, wafugaji hawa wanakabiliwa na tatizo katika soko la mifugo ambapo wengi hupunjwa na matapeli. Pamoja na haya, baadhi ya wakazi huuza mifugo nje ya nchi wakiwa wazimawazima bila kuwazia matokeo ya kitendo hiki. Si ajabu kuwaona ng'ombe, ngamia, mbuzi na kondoo wakipakiwa kwenye malori na kusafirishwa nje ya nchi. Ukweli ni kwamba jambo hili ni hatari sana, si kwa uchumi wa maeneo husika tu, bali pia kwa Kenya kwa jumla. Hii ni kwa kuwa walionunua mifugo wazimawazima wanaweza kuhiari kutowachinja na badala yake kuwatumia kama mbegu kwani baada ya muda huenda wanaonunua mifugo wakijitosheleza na kukosa kununua mifugo wengine. Hali ikiwa hivyo, maeneo yaliyotegemea soko hili huenda yakalipoteza taratibu, na bila shaka kupoteza natija inayotokana na soko lenyewe.

Ili kudhibitisha hali hii, itakuwa bora ikiwa viwanda vya kuchinjia mifugo na kupakia nyama vitajengwa katika maeneo haya ya ugatuzi. Hili litawawezesha wakazi kuuza nyama badala ya kuuza mifugo wazimawazima. Fauka ya hayo maeneo haya yatajikinga dhidi ya kupoteza bidhaa

zinazotokana na mifugo. Hizi ni kama vile ngozi, kwato na pembe ambazo bila shaka zina natija kuu. Ngozi kwa mfano, ni bidhaa muhimu sana katikasekta ya utengenezaji wa mavazi na mifuko. Viwanda vinavyotumia ngozi kama malighafi vikijengwa katika maeneo haya, wakazi wake watanufaika si haba. Madhalani, viwanda vya kutengenezea viatu, mishipi, mifuko na nguo vikianzishwa,wawekezaji watalazimika kuanzisha viwanda vingine tegemezi. Kathalika, ni dhahiri kwamba bidhaa zinazotokana na ngozi huhitaji kutiwa nakshi. Kuanzishwa kwa viwanda hivi basi kutazua haja ya kuanzishwa kwa viwanda vingine vya kutengeneza rangi, pamoja na maduka ya kuuza bidhaa zenyewe. Isitoshe, gundi ya kugandisha bidhaa hizi itahitajika, hivyo kusababisha haja ya kuanzishwa kwa kiwanda cha gundi. Matokeo ya shughuli hizi zote ni kuzalishwa kwa nafasi anuwaiza kazi kwa wakazi. Hili litakuwa na matokeo zaidi chanya, hususan kwa vijana. Badala ya kushiriki ulevi na burudani zinazowahatarisha, wataweza kujitafutia riziki katika viwanda hivi.

Juu ya hayo, mfumo wa ugatuzi utayaweza maeneo husika kuongeza thamani, utoaji wa huduma za kijamii na kuitawala kulingana na mahitaji  ya maeneo haya. Ni muhimu hata hivyo kuzingatia kwamba kila eneo la ugatuzi lina upekee wake, navyo vipaumbele hutofautianakulingana na maeneo. Kuna yale ambayo yatasisitiza usalama, mengine ujezi na uimirishaji wa miundomusingi kama vile barabara, vituo vya afya na hata taasisi za elimu. La muhimu ni wakazi wa maeneo husika kubainisha ni lipi litatekelezwa kwanza.

Kinga na kinga ndipo moto uwakapo. Kufanikiwa kwa mfumo wa ugatuzi kutategemea juhudi za kila mkazi wa eneo husika. Ni muhimu kila mkazi kujiona kuwa mmiliki wa eneo zima la ugatuzi na kuwajibika katika kuliendeleza kwa hali na mali.uwajibikaji huu unajumuisha uteuzi wa viongozi wenye muono mzuri na ambao utawawezesha kuyafikia malengo yao ya kimaendeleo. Hakika, mustakabali na uwepo wa eneo la ugatuzi utakuwa zao la maamuzi ya wanaeneo. Vilevile ufanisi wa maeneo ya ugatuzi utakuwa msingi wa ufanisi wa taifa kwa jumla.

a) Fupisha ujumbe wa aya tatu za mwanzo kwa maneno 85-90 (alama 8, 1 mtiririko)

**Matayarisho:**……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi:**

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

b) Kwa kutumia maneno 75-80, bainisha masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya tatu za mwisho. (alama7, 1 mtiririko)

**Matayarisho:**…………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

(a) Andika neno lenye sauti zifuatazo: (alama 1)

Kipasuo hafifu cha midomo, irabu ya mbele wastani, kikwamizo sighuna cha ufizi, irabu ya kati chini. ____________________

(b) Tunga sentensi moja moja yenye aina zifuatazo za vishazi: (alama 2)

(i) Cha nia

(ii) Kitegemezi cha wakati

(c) Andika maana ya maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)

Wali<u>sita</u> kufanya kazi hiyo baada ya saa <u>sita</u> usiku.

(d) Tia shadda: (alama 2)

i. pekee

ii. alinyongwa

(e)Huku ukitoa mfano, onyesha miundo mitatu ya maneno katika ngeli ya U-I

(alama 3)

f) Tunga sentensi yenye vijisehemu vifuatavyo vya sarufi: (alama 2)

Kiambishi kiwakilishi cha kiima

Kiambishi kiwakilishi cha wakati

Yambwa

Mzizi - dhiki

Kauli ya kutendesha

Kiishio

(g) Tumia neno dhahiri kama: (alama 3)

Kitenzi________________________________________

Kivumishi________________________________________

Kielezi________________________________________

(h) Huku ukitoa mifano, eleza miundo mitatu ya silabi za Kiswahili. (alama 3)

(i) Tofautisha mzizi na shina kwa mifano. (alama 2)

(j) Nyambua ziba katika kauli ya kutenduka kisha utungie sentensi. (alama 2)

(k) Bainisha hali zinazorejelewa katika sentensi hizi. (alama 3)

(i) Mwangeka hufika kituoni mapema.____________________________

(ii) Mgonjwa angetibiwa angepona.____________________________

(ii) Umekuwa nanasi, kutagia mibani? ____________________________

(l) Andika katika udogo wingi. (alama 2)

Ugwe ulipitishwa juu ya ukuta uliomea uyoga na kufungiwa kwenye makuti.

(m) Onyesha kiarifu katika sentensi hii. (alama 1)

Kilimia kimechomoka angani.

(n). Changanua kwa kielelezo cha mstari. (alama 3)

Ndege aliruka angani ghafla.

(o) Ainisha Virai vinne katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Kicha cha funguo kilikuwa kimepotea jana nikicheza kandanda.

i________________________________________________________________

ii________________________________________________________________

iii________________________________________________________________

iv________________________________________________________________

(p) Tunga sentensi kuonyesha matumizi mawili ya nukta mkato. (alama 2)

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________

(q) Andika methali yenye maana sawa na jivu usilolilala usilipigie Jibwa. (alama 1)

________________________________________________________________

________________________________________________

(r) Andika upya sentensi ifuatayo ukianza kwa shamirisho kitondo. (alama 2)

Kaizari amewakatia ng'ombe majani kwa muundu.

________________________________________________________________

________________________________________________

(s) Damka ni kwa rauka, wakati ni kwa_______________oa ni kwa taliki uza ni kwa_______

**4. (ISIMUJAMII)** (alama 10)

a) Katika jamii huwa wakati mwingine kuna matumizi ya lugha isiyo ya kistaarabu. Taja mifano <u>mitano</u> ya lugha sampuli hiyo (alama 5)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

b) Taja mambo matano yanayoathiri jinsi tunavyoweza kutumia lugha katika jamii. (alama 5)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse*)**

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: ……………………………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ………………DARASA: …...........**

# MTIHANI WA PAMOJA WA EAGLES

**Maagizo**

**(a)** Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
**(b)** Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu
**(c)** Jibu maswali yote.
**(d)** Majibu yako yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
**(e)** Majibu yote ni lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
**(f)** Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.
**(g)** Karatasi hii ina kurasa 11 zilizopigwa chapa.
**(h)** Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

Kwa matumizi ya mtahini pekee

| Swali | | Upeo | Alama |
|---|---|---|---|
| | **Ufahamu** | **15** | |
| | **Ufupisho** | **15** | |
| | **Matumizi ya lugha** | **40** | |
| | **Isimujamii** | **10** | |
| | **Jumla** | **80** | |

1. **UFAHAMU**: **(alama15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata**

"Yakobo, eti babu yako ndiye mnyama? Siamini na sitaamini maneno hayo."

"Uliuomba ukweli."

"Kwa nini hukuniambia mambo haya zamani, Yakobo? Kwa nini mama yako hakunifunulia? Kwa nini aliisoma barua hii akaificha?"

"Yote hayo yalifanywa ili uwe na maisha bora. Ulipata wazazi wema waliokulea na kukutunza. Ulipelekwa shuleni, Chaanasa, mimi sikukanyaga shuleni. Ikiwa ungeachwa kinyongo, huenda hungekuwa na maendeleo uliyo nayo. Labda ungeingilia maisha mabaya na kuwa mtu bure kabisa. Zipo siri zinazowekwa ili kuwalinda watu."

Lakini, Yakobo, inaniuma sana. Miaka yote hii tumetembea pamoja, tumekuwa tukitembeleana, tumekula meza moja, tumefanya mambo mengi pamoja wala huniambii mimi ni mjomba wako."

Naomba msamaha, kwa moyo wangu wote, kwa kukosa kueleza mambo hayo mapema. Hata hivyo, ni vizuri kuona mambo kwa njia nyingi, si mtazamo mmoja tu. Tuseme, ningekuambia mambo hayo mapema, je, ungekuwa na furaha zaidi? Huenda jitihada zako za kumtafuta baba yako zingekutia chuki. Pengine hata ungetamani kulipiza kisasi kwa dhiki alizokuletea ukafungwa jela au hata kuhukumiwa kifo. Wakati mwingine, ni salama kutojua. Jambo usilolijua halikunyimi usingizi. Hata hivyo, naomba radhi kwa kutokuambia. Ukweli wa mambo ni kwamba hata Mzee Johari muungwana, yaani, babu yangu, au baba yako, hakujua mambo haya yote. Alikufa bila kujua sura au jina la mtoto wake: Chaanasa."

Bwana Chaanasa, bila kujua, alilia na kudondokwa na machozi kupukupu. Nikaona aibu kubaki hapo, lakini sikuondoka. Nilitaka kusikia hatima ya mazungumzo hayo.

"Yakobo, mpwa wangu," Bwana Chaanasa aliita huku akilia. Akanyoosha mikono yake na kumkumbatia Yakobo.

"Nimekusamehe. Nimekusamehe. Lazima nitekeleze ombi la mamangu. Alinisihi nisiwe na chuki na mtu yeyote. Siwezi kukuchukia mpwa wangu. Naahidi sitakuchukia kamwe. Asante kwa kuniambia ukweli wote. Asante pia kwa hekima yako kwani pia ulingoja hadi wakati unaofaa kunifunulia mambo haya. Ungaliyafunua zamani, kama ulivyosema awali, huenda nisingaliitikia jinsi nilivyofanya leo. Huenda mambo yangekuwa mabaya. Labda ningelipuka kwa hasira na kusababisha hasara, pengine hasara isiyolipika. Sasa ninaelewa kwa nini tunalandana sana nawe, na mzee Busara. Sisi ni wa damu moja. Baba yangu angalikuwa hai, ningalienda nikamwone na kujitambulisha kwake. Ningalimwita 'baba' na huenda angaliniita 'mwanangu.' Ningalimsamehe kwa kumwacha mamangu na kunitelekeza."

"Bado unaweza kumsamehe."

"Jinsi gani?" Bwana Chaanasa akauliza.

"Kwa kusahau yaliyopita na kuganga yajayo. Yazike mambo yote hayo katika kaburi la sahau. Acha ya kale yawe ya kale, ya nyuma yawe ya nyuma, ya zamani yawe ya zamani. Kilichotendeka kimekwishatendeka. Yaliyofanyika yamefanyika. Yamemwagika na hayatazoleka kamwe hata kwa kuchimbua ardhi. Lililopita limepita, si uwele tena.

"Naam, Bwana Chaanasa, lipitalo hupishwa."

**Maswali**

**(a)** Eleza sababu za Chaanasa kufichwa taarifa kuhusu babake. **(alama2)**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**(b)** Thibitisha kuwa babu yake Yakobo alikuwa mnyama. **(alama2)**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**(c)** Eleza umuhimu wa maswali balagha katika kifungu hiki. **(alama2)**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**(d)** Je, ni kweli kuwa kama si kuweka siri mambo yangemharibikia Chaanasa? Tetea jibu lako. **(alama3)**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**(e)** Ni jambo lipi lililomfanya Chaanasa kumsamehe mpwa wake? **(alama2)**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**(f)** Kwa mujibu wa kifungu, kusamehe kuna matokeo gani? **(alama2)**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**(g)** Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu. **(alama2)**

**(i)** hayatakusanywa

……………………………………………………………………………………………

**(ii)** pamoja

……………………………………………………………………………………………

**2. UFUPISHO** **(alama15)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Maadili ni desturi, utamaduni au hulkaa mbazo hubainisha na kulipa kundi fulani la watu upekee wake. Maadili ni muhimu katika kuonesha imani na kanuni za maisha ambazo kundi Fulani la watu huchukulia kuwa chanya na zile wanazozichukulia kuwa hasi. Maadili ndio mwongozo unaothibiti matendo na hulka za kila mmoja.

Kila jamii huwa na maadili yake ambayo yanamhitaji kila mwanajamii kutenda na kuishi kama jamii inavyotarajia. Pia, yaliweza kulegeza mielekeo au mitazamo yao. Hata leo, maadili hutusaidia kubainisha sisini akina nani, mtazamo wetu maishani, pamojana matarajio yetu.

Katika Katiba ya Kenya, maadili ya jamii ya Wakenyayameangaziwavyema. Kwanza, ni wazi kuwa Kenya ni taifa la wacha Mungu, kwa hivyo, kila Mkenyaanatarajiwa kuabudu na kumheshimu Mwenyezi Mungu. Hili limeshadidiwa hata katika wimbo wetu wa taifa. Pamola na hayo, katika kuimarisha umoja wa kitaifa, tofauti zetuWakenya kirangi, kikabila, kitabakana hata kidini hazipaswi kutugawanya.Maadili yanatuhimiza kuzichukulia hizo kuwa sifa za kipekee na kuzionea fahari. Ule utaifa wetu kama wakenya unapaswa kuwekwa mbele daima ili kuzima juhudi zozote za kututenganisha kwa misingi hiyo.

Kama taifa, tunahitaji kudumisha uzalendo wetu kwa kujitolea kuhakikisha kuwa mahasidi hawaporomoshi maadili ya jamii zetukwa kuiga hulka zao potovu. Uzalendo unatuhumiza kuripoti vitendo vyote vya kuihujumu nci au watu wake kwa asasi za dola. Asasi hizo zitachunguza na kuzima utekelezaji wa uhalifu kabla haujatikea, na iwapo utakuwa umetokea, asasi hizo zitawapa adhabu wahalifu ili waweze kubadili mienendo mibaya na kuwa kielelezo kwa wengine wenye nia mbaya.

Maadili, vilevile, humwongoza mtu kuhusu namna za kutatua mizozo na kudumisha amani. Hatuwezi tukajivunia uhuru pasi na kuwepo amani. Amani ndio msingi wa umoja, ustawi na maendeleo ya taifa lolote. Ukosefu wa amani hudumaza na hata kurudisha nyuma maendeleo kwa kuwahini watu nafasi za kushiriki uzalishaji mali. Ukosefu wa amani vilevile husababisha kuongezeka kwa visa vya uhalifu kama vile mauaji, kulememazwa kwa watu, unajisi, uharibifu wa mali na kusambaratika kwa familia, hali ambayo huchangia mporomoko wa maadili katika jamii.

Uadilifu unakwenda kinyume na methali, amani haiji ila kwa ncha ya upanga. Ukweli ni kwamba, tunaweza kusuluhisha tofauti zetu bila kutumia silaha. Matumizi ya silaha aghalabu huzidisha uhasama na kuchochea haja ya kulipiza kisasi. Njia pekee ya kutatua migogoro ni kuelewa chanzo cha migogoro yenyewe, wahusika kufanya kikao na kuizungumzia kwa uwazi na kwa utulivu. Pande zote husika zinafaa kukubali makosa au madhara yaliyotokana na matendo yao na kuomba msamaha ili kupata maridhiano. Kuomba msamaha kusidhaniwe kuwa kujishusha hadhi, bali ni unyenyekevu katika kutatua tofauti kwa manufaa ya muamala wa vizazi vijavyo. Anayeombwa msamaha naye anapaswa kuwa tayari kutoa shifaa kwa dhati na kusahau kosa alilofanyiwa. Yote haya yakishindikana, mgogoro wapaswa kupelekwa

mahakamani. Haki za kila mmoja zimelindwa katika katiba yetu na mahakama zipo ili kutetea haki hizi bila kupendelea upande wowote.

Utiifu wa sheria vilevile ni njia mojawapo ya kukuza maadili ya kijamii. Kwa kuwa sheria hulinda haki za kila mtu; wake kwa waume, wakubwa kwa wadogo, kila mmoja ana wajibu wa kuheshimu sheria. Hii ni pamoja na kulinda rasilimali zetu kama jambo la wajibu bila ya kutegemea kuwepe wadumisha sheria. Uongozi wa kisheria huwapa watu hakikisho kuwa maisha yao hayatakuwa kama ya mahayawani nyikani bali yatafuata utaratibu Fulani. Hivyo basi, sheria ni hakikisho la jamii inayolinda haki na kuendesha mambo yake kwa uwazi, haki na ushwari.

Bila shaka, tukizingatia na kuimarisha maadili, taifa letu litakuwa jamii bora na kivutio cha kila mtu. Kiu ya Wakenya ya kutaka kuhamia nchi nyingine, hasa zilizostawi, itapungua. Wote watakuwa na ari ya kuliendeleza taifa lao.

**Maswali**

**(a)** Eleza umuhimu wa maadili kwa jamii na taifa kwa ujumla. (maneno 60-70)

**(alama 7 , 1 ya utiririko)**

**(b)** Fafanua jinsi mizozo inaweza kutatuliwa kwa uadilifu. (Maneno 75-80)

**(alama8, 1 ya utiririko)**

**Matayarisho**

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

**3. MATUMIZI YA LUGHA** **(alama40)**

**(a)** Linganua sifa za konsonati katika maneno yafuatayo: **(alama2)**

**(i)** Shule

……………………………………………………………………………………………………

**(ii)** Cheza

……………………………………………………………………………………………………

**(b)** Onyesha silabi inayotamkwa kwa mkazo katika maneno yafuatayo **(alama2)**

**(i)** Waliotusherehekea

…………………………………………………………………………………………………….

**(ii)** Wafanyakazi(watu wanaofanya kazi)

…………………………………………………………………………………………………….

**(c)** Eleza majukumu ya viambishi awali katika neno: Waliotuhangaisha **(alama2)**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**(d)** Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? **(alama2)**

**(i)** Kuta

…………………………………………………………………………………………………….

**(ii)** Rafiki

…………………………………………………………………………………………………….

**(e)** Tunga sentensi yenye kitenzi kishirikishi kikamilifu **(alama1)**

……………………………………………………………………………………………………

**(f)** Andika upya sentensi zifuatazo kwa kufuata maagizo: **(alama8)**

**(i)** Mahali palipotayarishwa pamejaa waumini waliotoka nchini kote.
(Tumia kirejeshi amba)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**(ii)** Mwanamichezo hodari amevunja rekodi ya dunia.
(Anza kwa: Rekodi **…...**)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**(iii)** Mtafiti huyu alipewa tuzo nyingine.
(Tumia kiashiria kisisitizi)

……………………………………………………………………………………………………

**(iv)** Nilimwomba rafiki yangu **anisamehe** baada ya kumkosea heshima mkutanoni
(Badilisha neno lililopigiwa mstari liwe nomino)

…………………………………………………………………………………………………….

**(g)** Bainisha kikundi nomino na kikundi tenzi katika sentensi ifuatayo **(alama2)**
Vitabu vyote kumi na saba vimepelekwa maktabani.

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

**(h)** Andika sentensi ifuatayo katika udogo wingi **(alama2)**
Mtu huyu atanunua shamba mwaka ujao.

…………………………………………………………………………………………………………………

**(i)** Eleza hali zilizotumika katika sentensi zifuatazo: **(alama2)**
**(i)** Halati humpikia nyanya.

……………………………………………………………………………………………………………….

**(ii)** Juma ameingia kanisani

……………………………………………………………………………………………………………….

**(j)** Andika kwa wingi: **(alama2)**
Ufito huu ni mzito na mrefu mno.

………………………………………………………………………………………………………………..

**(k)** Tunga sentensi mojamoja ukitumia alama za kuakifisha zifuatazo:
**(i)** Alama za dukuduku **(alama2)**

………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………

**(ii)** Mshangao **(alama1)**

………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………..

**(l)** Rafiki yetu alituambia kuwa ataondoka keshoye kuelekea Afrika kusini kwa masomo ya chuo kikuu (Andika kwa usemi halisi) **(alama2)**

…………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………..

**(m)** Changanua kwa mstari **(alama2)**
Rais aliwafadhili raia waliokuwa wamesajiliwa pekee.

…………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………..

**(n)** Ainisha vielezi katika sentensi zifuatazo: **(aslama2)**
**(i)** Tuliondoka nyumbani usiku wa manane

………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………

**(ii)** Alimpiga rungu mara mbili jana jioni.

………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………

**(o)** Ainisha virai katika sentensi ifuatayo: **(alama3)**

Mwanafunzi mwenye kitabu cheusi ameingia ndani ya darasa.

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

**(p)** Bainisha chagizo na shamirisho katika sentensi ifuatayo **(alama2)**
Wachuna chai walifanya kazi hiyo kwa uvivu mwingi ajabu.

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

**(q)** Eleza maana ya methali ifuatayo: **(alama1)**
Chui na mbuzi hawala nyumba moja.

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

**4. ISIMUJAMII** **(alama10)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

"Niaje buda, umecheki yule morio wetu? Nikama amefyatu kiplani. Itabidi tuache drugs bro venye kunaenda si poa……"

**(a)** Tambua Sajili hii **(alama2)**

………………………………………………………………………………………………………

**(b)** Eleza sifa nne ambazo hujitokeza kwenye Sajili hii **(alama4)**

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

**(c)** Toa sababu nne zinzopelekea vijana kutumia lugha hii **(alama4)**

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: …………………………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ………………DARASA: …...........**

# MTIHANI WA PAMOJA WA KALA

**102/2**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA PILI**

**<u>MAAGIZO</u>**

***a)*** *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***b)*** *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***c)*** *Jibu maswali **yote.***
***d)*** *Majibu yako yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
***e)*** *Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
***f)*** *Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*
***g)*** ***Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

**Kwa matumizi ya mtahini pekee.**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | **15** | |
| 2 | **15** | |
| 3 | **40** | |
| 4 | **10** | |
| **Jumla** | **80** | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**1. UFAHAMU: ( Alama 15)**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Meli alipokivuka kizingiti cha lango la shule ya kitaifa ya Tungambele alikuwa na azma ya kusoma kwa bidii ili kuinukia kuwa kijana wa kutegemewa na jamii yake. Alikuwa kalelewa katika familia yenye pato wastani. Akasoma kwa juhudi za wazazi wake hadi darasa la nane alipokwangura alama za kumwezesha kujiunga na shule hii ya kifahari. Meli alijua kwamba alikuwa mwanagenzi, si katika masomo ya shule ya upili tu, bali pia katika maisha ya jijini ambamo shule hii ilipatikana. Kwa kweli hii ndiyo ilikuwa mara yake ya kwanza kutia guu kwenye jiji hili ambalo habari zake akizisoma, ama katika magazeti machache yaliyowahi kufika kijijini, au kupitia somo la Elimujamii. Hata hivyo, Meli hakuwa mtu wa kuogopa au kunywea machoni mwa changamoto. Alijiambia kwamba kwa vyovyote vile atapambana na maisha haya mapya.

Saa mbili kamili asubuhi ilimpata Meli kapiga foleni katika afisi ya kuwasajili wanafunzi wageni. Wasiwasi wa aina fulani ulianza kumnyemelea alipotazama hapa na pale bila kuona dalili ya mja yeyote aliyemfahamu. Alijihisi kama yule kuku mgeni ambaye mwalimu wake alishinda kuwaambia kuwa hakosi kamba mguuni. Hata hivyo aliupiga moyo wake konde na kujiambia kuwa kuja kwake hapa kulitokana na juhudi zake mwenyewe na katu hatauruhusu ugeni wa mazingira kuifisha ari yake ya masomo.

Usajili ulikamilika, naye Meli na wenzake wakajitosa katika ushindani wa kimasomo jinsi waogeleaji wajitumbukizapo kidimbwini wakapiga mbizi, baadhi wakiambulia ushindi na wengine wakifedheheka kwa kushindwa. Meli na wenzake walibainikiwa kwamba wote walikuwa mabingwa kutoka majimbo na wilaya zao. Ilimbidi kila mmoja wao kujikakamua zaidi ili kuelea katika bahari hii ya ushindani. Muhula wa kwanza ulishuhudia kishindo cha Meli kubwagwa chini na majabali wenzake. Alijipata miongoni mwa wanafunzi kumi wa mwisho; au kama alivyozoea **kuwatania** wenzake katika shule ya msingi, “wanafunzi kumi bora kuanzia mwisho”! Hili lilimwatua moyo Meli na kumfanya kutahayari. Alifika kwao amejiinamia kama kondoo aliyeumia malishoni. Akawataka wazazi wake wambadilishie shule lakini wakakataa.

Muhula wa pili na wa tatu mambo yalikuwa yaleyale. Meli akahisi kama askarijeshi aliyeshindwa kabisa kutambua mbinu za kuwavizia maadui. Akaona kwamba njia ya pekee ni kujiunga na wenzake kama yeye katika vitendo vya utundu kama vile kuvuruga masomo kwa kupiga kelele darasani, kupiga soga bwenini na hata kuvuta sigara. Mwanzoni alichukia vitendo hivi lakini alimeza mrututu akisema kwamba ndiyo njia ya pekee ya **kujipurukusha**na aibu. Wazazi wa Meli hawakusita kutambua mabadiliko katika hulka ya mwanao. Wakajaribu kumshika sikio nyumbani lakini akawa hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Wakawahusisha wataalamu wa ushauri nasaha ambao waliwaambia kuwa Meli hakuwa na tatizo lolote la kuyadumu masomo. Kile alichokosa ni kujiamini tu.

Wazazi wa Meli waliona kuwa ni muhimu kuwahusisha walimu katika kutatua tatizo la mwanao. Mwanzo wa muhula wa pili uliwapata wazazi hawa afisini mwa naibu wa mwalimu mkuu. Mazungumzo kati ya wazazi, naibu wa mwalimu mkuu na mwalimu wa darasa la Meli yalidhihirisha kwamba walimu walikuwa wamemuasa Meli kuhusu kujiingiza katika makundi yasiyomfaidi lakini rai zao ziliingia katika masikio yaliyotiwa nta. Aliyopenda Zaidi Meli nishughuli zilizomtoa nje ya shule kama vile tamasha za mziki, ukariri wa mashairi na drama. Mazungumzo yalibainisha kwamba Meli alihitaji ushauri na uelekezaji Zaidi kutoka kwa mtaalamu wa nasaha pale shuleni.

Meli alianza vikao na mtaalamu huyu ambaye pia alimpendekezea Meli ushauri zaidi kutoka kwa washauri marika. Hili lilimchangamsha zaidi Meli kwani aliwaona hawa kama wenzake waliojua changamoto zake. Juhudi za mtaalamu wa nasaha na washauri marika zilifua dafu. Mwisho wa kidato cha pili ulishuhudia mabadiliko makuu katika hulka na utendaji kimasomo wa Meli. Aliukata kabisa uhusiano wake na marafikiwaliompotosha na kuanza kuandamana na wanafunzi waliotia juhudi masomoni. Polepole alama zake ziliimarika. Matokeo ya mtihani wa kidato cha nne yalimweka kwenye safu ya wanafunzi bora zaidi nchini.

a) “Wanafunzi wawapo shuleni hukumbana na changamoto nyingi”. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hoja sita kutoka kwenye taarifa. .(alama 6)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

b) Eleza mchango wa washikadau mbalimbali katika kumsaidia Meli kupata ufanisi masomoni. (alama 4

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

c) Bainisha mbinu **tatu** za lugha ambazo msimulizi anatumia katika kuwasilisha ujumbe wake katika kifungu. (alama 3)

………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

d) i. Andika kisawe cha ‘**kijipurukusha’** kwa mujibu wa taarifa (alama 1)

……………………………………………………………………………………

ii. Andika maana ya ‘**kuwatania’** kulingana na taarifa. (alama 1)

………………………………………………………………………………………

**2. UFUPISHO (Alama 15)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo.***

Bei ghali ya vyakula ni jambo linalowaathiri wakenya wengi kwa hivi sasa. Inasikitisha kupata kwamba bei ya unga wa ugali imepanda hadi sh. 200. Ni wazi kwamba familia nyingi nchini hukosa lishe lao kutokana na kufumka kwa bei ya bidhaa muhimu. Hata hivyo ibainike kwamba nchi isiyowakimu raia wake kwa chakula ni sawa ng”ombe aliyeshindwa kumnyonyesha ndama wake.

Kwa muda mrefu, viongozi wamekuwa wakipambana na tatizo la ukosefu wa chakula. Msimu wa kiangazi unapobisha hodi, watu wengi hasa wale wahitaji hupukutika kutokana na mngato wa njaa. Japo serikali na wafadhili hutuma vyakula vya msaada kwa jamii zilizoathirika, chakula hiki huwa kama nguo ya kuazima, na bila shaka ya kuazima haikidhi haja.

Mojawapo ya vyanzo vikuu vya uhaba wa chakula ni kiwango cha chini cha uzalishaji na uhifadhi wa chakula chenyewe. Zipo seheu nyingi ambazo ni kame nchini.sehemu hizi hukabiliwa na ukosefu wa maji kwani, ama mvua hainyeshi au inaponyesha haitoshelezi mahitaji ya mimea. Mimea mingi hujikaukia ikiwa michanga na kudhihaki juhudi za wapanzi. Zipo sehemu katika nchi hii ambazo huenda kwa misimu hata mitano bila kupata zao lolote kutoka mashambani. Hali ikiwa hivi makali ya uhitaji huzidi na wakazi wa sehemu hizi hulazimika kuwa wategemezi kwa majirani na serikali. Wengine wanapokosa chakula kabisa huazimia kula visivyoliwa.Wanaamwa la mbwa baada ya kukosa la mama.

Hali kadhalika japo zipo sehemu zingine ambazo hazina tatizo la ukame, mbinu hasi za kilimo husababisha utoaji wa mavuno haba, hivyo kutojitosheleza kwa chakula. Bilas haka wanapopanda ovyo wanavuna ovyo. Kuna wakulima ambao hupalilia mmomonyoka wa udongo kwa kulima kando kando ya mito, kupanda zao lile lile katika sehemu ile ile ya ardhi miaka nenda miaka rudi, na kutopanda mimea ambayo hukinga tabaka la juu la udongo dhidi ya kumomonyolewa na maji au upepo. Matokeo ya haya yanaweza kutabiriwa; udongo wenye rutuba huoshwa na mashamba kutwaa utasa ambao huzidisha kuzalisha kwa chakula haba. Wakulima wengine hukaidi wito wa kupanda mimea ambayo hustahimili ukame kama vile mbaazi mihogo, mtama na wimbi. Baadhi ya wakulima hufuga mifugo wengi ambao hushindwa kustahimili kiangazi. Si ajabu kupata kwamba katika baadhi ya maeneo mizoga ya ngombe na hata ngamia imezagaa kote tanuri la kiangazi linapofanya kazi yake.

Sehemu zingine zimebarikiwa na ukwasi wa chakula. Hata hivyo baadhi ya wakazi wa sehemu hizi hawana mwao kuhusu umuhimu wa lishe bora. Wapo wanaodhani kuwa chakula ni chakula bora tumbo lipate haki. Hawa hula vyakula kama vile viazi, mahindi, na wengine nyama bila kujua wanahiyaji vyakula vyenye virutubisho muhimu, yani wanga, protini , vitamini na madini. Wapo wanaodhani kuwa protini pekee ni nyama. Hawa hula nyama mawio na machweo, matokeo yakiwa kuambulia magonjwa kama vile shinikizo la damu.

Katika kukabiliana na tatizo la uhaba wa chakula, serikali kupitia wizara husika imeanzisha miradi ya kuhakikisha kuwa kuna uzalishaji wa chakula kwa kiwango cha kuridhisha. Serikali ya Ruto sasa imepunguza bei ya mbolea hadi sh 3500 ili kuwawezesha wakulima kupanda chakula kwa wingi. Visima na mabwawa ya maji pia vitachimbwa katika maeneo kame ili kunyunyuzia mashamba maji. Baadhi ya wakulima wameanza kupanda mimea ambayo inapevuka na kutoa mazao kwa haraka ipo mimea ya kuatika ambayo hutoa matunda baada ya muda mfupi, hivyo kusaidia kupunguza makali ya njaa. Wafugaji wengine wameanzisha miradi ya kufuga kuku wa kututumuliwa. Hawa hukuwa na kukomaa kwa muda mfupi na huweza kutoa nyama na mayai. Wafugaji wa kuku hawa huweza kuwauza kununua aina nyingine ya chakula.

Wakulima pia wanahimizwa kutumia njia za kisasa za kuzalisha na kuhifadhi chakula.chakula kinapohifadhiwa vyema, hata mvua isiponyesha raia huweza kujitegemea. Ikiwa maghala ya halmashauri za kuhifadhi chakula nchini hayahifadhi chakula mara nyingi hulazimika kuagiza chakula kutoka nje kiangazi kinapojiri. Aidha chakula kisipohifadhiwa vyemahuishia kuharibika na kuhasiri wanaokila ikawa msiba juu ya mwingine.

Ni muhimu kufahamu kuwajukumu la kupambana na ukosefu wa chakula ni la kila raia. Hali ya kungojea kila mara kulishwa na serikali inatufanya kuwa wategemezi Zaidi. Wadogo wadogo ambao huuza vyakula kwa bei ya chini sana mara tu wanapovitoa mashambani wanapaswa kujiasa dhidi ya mazoea haya na kujua kuwa akiba haiozi. Wanaoishi katika sehemu za vinamasi wasaidiwe kuzitunza sehemu hizi na kuzitumia kwa njia endelevu. Vijana wahimizwe wawaunge wazee mkono kushughulikia kilimo katika sehemu za mashambani badala ya kuhamia mijini kutafuta kazi za ajira ambazo ni haba.

a) Fupisha ujumbe wa aya tano za kwanza kwa maneno 100. (alama 9, 1 ya mtiririko)

**Matayarisho**

**Jibu**

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

Kwa kurejelea aya tatu za mwisho, eleza njia sita za kukabiliana na uhaba wa chakula. (maneno 85)

(alama 6, 1 ya mtiririko)

**Jibu**

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

**3.MATUMIZI YA LUGHA** **(ALAMA 40)**

a) Eleza maana ya kipashio kidogo cha lugha. (alama 1)

……………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

b) Andika maneno yenye sifa zifuatazo: (alama 2)

i) kikwaruzo ghuna cha ufizi, vokali ya chini-wastani, kizuiwa ghuna cha midomo, kiyeyusho cha midomo, irabu ya chini-kati

…………………………………………………………………………………………………

ii) Kipua ghuna cha ufizi, kipasuo cha ufizi, irabua ya mbele-juu, nazali ghuna ya midomo, irabu ya nyuma-juu.

…………………………………………………………………………………………………

c) Ainisha uamilifu wa kisarufi wa mofimu kwenye neno hili. (alama 3)

Lilimjisha

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………

d) Tunga sentensi **moja** kuonyesha matumizi **mawili**ya **"tu".** (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

e) Unda kitenzi kutokana na nomino **toba** kisha ukitungie sentensi. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

f) Yakinisha kwa kutumia kiambishi cha masharti ya uwezekano kwa wingi. (alama 2)

Usiposoma kwa bidii hutofaidika.

…………………………………………………………………………………………………

g) Tumia nomino ya ngeli ya mahali dhahiri pamoja na kivumishi kirejeshi cha kati kwa sentensi. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

h) Andika kinyume cha sentensi hii. (alama 2)

Mjomba alimtwika mwanawe mzigo akabana mlango.

…………………………………………………………………………………………………

i) Bainisha kijalizo katika sentensi ifuatayo. (alama 1)

Tajiri huyo shupavu ana magari makubwa mno.

…………………………………………………………………………………………………

j) Tunga sentensi kwa kutumia chagizo cha ulinganisho. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

k) Andika upya sentensi kwa wakati uliopita hali endelevu, kauli ya tendesheka. (alama 2)

Wenyeji wamewapokea wageni kwa taadhima.

…………………………………………………………………………………………………

l) Tunga sentensi **moja** kuonyesha maana mbili za neno **tema**. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

m) Ainisha aina ifuatayo ya sentensi kiutendakazi. (alama 1)

Safari imekuwa ikitusumbua sana.

…………………………………………………………………………………………………………

n) Onyesha kiima na utambue muundo wake katika utungo huu. (alama 2)

Pesa zote zilihifadhiwa na mwekahazina shujaa.

………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

o) Tumia kishazi tegemezi kwenye sentensi kuonyesha vigezo vifuatavyo. (alama 2)

i) Wakati

…………………………………………………………………………………………………………

ii) Jinsi

…………………………………………………………………………………………………………

p) Changanua kwa kielelezo cha mistari. (alama 4)

Aliponijia kwa mkopo, nilikuwa nasali sebuleni.

………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………

q) Andika upya kwa kuanza na yambwa tendwa. (alama 2)

Mvua iliwanyea wanunuzi sokoni hivi majuzi.

………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

r) Tunga sentensi katika udogo ukitumia kihusishi cha uhusiano. (alama 2)

………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

s) Eleza matumizi ya kiambishi **po** katika sentensi. (alama 2)

Achezapo anapofika sisi hushangilia.

………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………

t) Twasema oyee tunapofurahia jambo……………………………….tunapotahadharisha na ………………

Tunapotoa himizo (alama 2)

**4: ISIMU JAMII** **(alama 10)**

***Soma makala haya kisha ujibu maswali;***

Rafiki yako amezongwa na mambo magumu na anafikiria suluhu ni kujiua umepewa jukumu la kumshauri.Fafanua sifa **kumi** za lugha utakayotumia ili kufanikisha ujumbe wako.

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: ……………………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ………………DARASA: …...........**

# MTIHANI WA PAMOJA WA KASSU

**102/2**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA PILI**

**Maagizo**

***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

***b)*** *Jibu maswali yote.*

***c)*** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*

***d)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**<u>KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE</u>**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. UFAHAMU | 15 | |
| 2. UFUPISHO | 15 | |
| 3. SARUFI | 40 | |
| 4. ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuatia**

Mateso ya wanawakiwa ni suala la kijamii linalofaa kutazamwa kwa darubini kali. Hata hivyo wanaoathirika zaidi ni watoto ambao bado wako katika umri unaohitaji kulelewa na kupewa mahitaji ya msingi kama mavazi, malazi, elimu na mengine anuwai. Hali ya kuachwa na wazazi imekuwa ikizikumba jamii tangu enzi za mababu na kila itokeapo, wanajamii huipokea kwa mitazamo tofautitofauti, hivyo kuwafanya wanawakiwa kuathirika sana.

Baadhi ya jamii zina imani za kijadi pamwe na mila zilizochakaa zinazozifanya kuamini kuwa baadhi ya vifo hutokana na laana. Wengine huchukulia kuwa mwendazake ameondolewa na ulozi. Imani kama hizi huifanya jamii kuwatia watoto walioachwa katika mkumbo ule ule, hivyo kuwaangalia kwa macho yasiyo ya kawaida. Hili husababisha dhana gande. Hali hii husababisha kuwachukulia watoto kama wanaotoka katika kizazi kilicholaaniwa. Jamii basi hukosa kuwapa watoto hawa stahiki yao. Hata wanapojitahidi kuiwania nafasi yao, waliowazunguka huwavunja mioyo. Jitihada zao huishia kuwa si chochote kwa kuwa jamii inawatazama kama waliolaaniwa.

Punde baada ya mzazi mmoja au wote wawili waendapo wasikorudi, inatarajiwa kwamba aliyeachiwa mtoto, awe mzazi wake, mwanafamilia au jirani awajibike na kumtunza mwanamkiwa. Kunao kadha wa kadha wanaowajibika – ninawavulia kofia. Hata hivyo wengi hutelekeza jukumu hili walilopewa na Muumba. Si ajabu basi kuona kuwa idadi ya watoto wanaozurura mitaani inazidi kuongezeka kila uchao. Ukichunguza utakuta kuwa wengi wa watoto hawa ni waliopotelewa na wazazi wao. Inakera zaidi kugundua kuwa baadhi ya watoto hawa wana mzazi mmoja. Kwamba mke au mume wa mtu ameaga, au iwe kwamba mzazi mmoja alimzaa mtoto na kumwachia mwenzake mzigo wa ulezi, aliyeachiwa ana jukumu la kumpa mwanawe mahitaji ya msingi. Machoni pa Jalali, kila anayeupuuza wajibu huu ana hukumu yake siku ya kiama!

Ni haki ya kila mtoto kupata elimu. Katika katiba ya Kenya mathalan, elimu ya msingi, yaani kuanzia shule ya chekechea had kidato cha nne ni ya lazima. Tangu hapo hata hivyo, jamii zimekuwa zikiwanyima wanawakiwa wengi elimu. Kwamba kunao wachache wanaowaelimisha baadhi ya wanawakiwa, ni kweli. Hata hivyo, wengi hukosa hata wa kuwapeleka katika shule ya chekechea, hivyo kuishia kutojua hata kuandika majina yao. Mfikirie mtu katika karne ya 21, asiyejua kusoma wala kuandika! Nani ajuaye, huenda huyo mwanamkiwa asiyepelekwa shuleni ndiye angalikuwa profesa, daktari, mwalimu, rubani au msomi mtajika na mtaalamu wa uwanja muhimu katika jamii!

Kila mtoto ana haki ya kulelewa hadi kufikia utu uzima kabla ya kupewa majukumu mazito. Katika katiba ya Kenya, utu uzima, ulio umri wa kuanza kufanya kazi huanzia miaka 18. Wanaohakikisha watoto hawa wametimiza utu uzima kabla ya kufanyishwa gange ngumu wanafaa pongezi. Hata hivyo wanawakiwa wamekuwa wakitumiwa na wengi kama punda wa huduma. Wanaaila wengine huwachukua wanawakiwa kwa machozi mengi wazazi wao waagapo nakuapa kuwahifadhi na kuwatunza wana wale wa ndugu zao, kumbe ni machozi ya simba kumlilia swara!

Hata kabla ya mwili wa mzazi mhusika kuliwa na viwavi, mateso kwa mtoto yule huanza, akawa ndiye afanyaye kazi zote ngumu. Utakuta watoto wao wamekaa kama sultan bin jerehe huku mwanamkiwa yule akiwapikia, kuwafulia nguo, kudeki, karibu hata awaoshe miili! Kazi kama zile za shokoa huwa za sulubu na aghalabu husindikizwa kwa matusi yasiyoandikika.

Baadhi ya waja walionyimwa huruma huwahadaa wanawakiwa na kuwapeleka ng'ambo wakitumia vyambo, kuwa wakifika kule watapata kazi za kifahari. Maskini wale hushia kushikwa shokoa, wakawa watumwa katika nyumba za waajiri wao, bila namna ya kujinasua. Wengine hushia kutumiwa kama watumwa wa 'kimapenzi' katika madanguro, miili yao ikawa ya kuuziwa makahaba waroho wasiojali utu. Kujinasua kule huwa sawa na kujitahidi kuokoa ukuni uliokwishageuka jivu, maadamu wanawakiwa aghalabu hukosa watu wenye mioyo ya huruma ya kuwashughulikia. Wengi huitumia methali 'mwana wa ndugu kirugu mjukuu mwanangwa' kuwapuuzilia mbali wanawakiwa ambao hukimbiliwa tu wabinafsi hawa wanapofaidika wenyewe.

**Maswali**

**a)** Ipe taarifa hii anwani mwafaka. **(alama 1)**

______________________________________________

______________________________________________

**b)** Eleza dhana ya mwanamkiwa kwa mujibu wa kifungu. **(alama 2)**

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

**c)** Eleza imani za kijadi kuhusiana na wanawakiwa. **(alama 2)**

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

**d)** Jadili masaibu yanayowakumba wanawakiwa. **(alama 4)**

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

**e)** Eleza haki mbili za kikatiba zilizokiukwa kuhusiana na wanawakiwa. **(alama 4)**

______________________________________________

______________________________________________

**f)** Eleza maana ya msamiati ufuatao kulingana na kifungu. **(alama 2)**

**i)** Inakera

**ii)** Majukumu

1. **UFUPISHO: (Alama 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali**

Runinga kama kifaa kingine chochote cha mawasiliano kina manufaa yake. Kwanza kabisa, ni nyenzo mwafaka ya kufundishia. Vipindi vinavyopeperushwa katika runinga huwa na mafunzo kemkemu kwa mtu wa kila rika. Halikadhalika, runinga huweza kuleta vipindi ambavyo huwafahamisha watu mambo yanayoendelea katika mazingira yao na duniani. Aidha, runinga ikitumika pamoja na michezo ya video huauni katika ukuzaji na ustawishaji wa stadi ya kujifundisha au kujielimisha. Michezo ya video, hasa ya kielimu, huwafanya watu kujenga umakini pamoja na kuchua misuli ya ubongo na kuwafanya watu kuwa macho wanapofanya kazi.

Fauka ya hayo, televisheni ni chemchemi bora ya kutumbuiza na kuchangamsha. Hakuna mtu asiyependa kuchangamshwa. Televisheni ni mojawapo ya vyombo mwafaka vya kutekeleza hayo kutokana na vipindi vyake. Uburudishaji huu huwa ni liwazo kutokana na shinikizo na migogoro tunayokabiliana nayo kila siku. Uburudishaji huu hupatikana kwa urahisi majumbani mwetu.

Vivyo hivyo, runinga hutumika kama nyenzo ya kuendeleza utamaduni, kaida na amali za jamii. Vingi vya vipindi vya runinga huwa ni kioo ambacho huakisi mikakati na amali za jamii.

Kwa upande mwingine, hakuna kizuri kisichokuwa na dosari. Licha ya manufaa yake, televisheni imedhihirika kuwa na udhaifu wake. Kwanza, baadhi ya vipindi vya runinga na video hujumuisha ujumbe usio na maadili, kama vile matumizi ya nguvu za mabavu, ngono za kiholela, lugha isiyo ya adabu, ubaya wa kimavazi na maonevu ya rangi, dini, jinsia, kabila na utamaduni. Si ajabu kuwa baadhi ya vijana wetu wanaiga baadhi ya mambo haya. Vijana wetu siku hizi wameingilia ulevi wa pombe na afyuni, ngono za mapema kabla ya ndoa na mavazi yanaowaacha takribani uchi wa mnyama. Wengi wamekopa na kuyaiga haya kutoka katika runinga. Ukiwauliza wafanyacho, watakujibu kuwa ni ustaarabu kwani wameupata katika runinga.

Matumizi ya runinga na michezo ya video yasiyodhibitiwa huweza kuwa kikwazo cha mawasiliano bora miongoni mwa familia. Matumizi kama haya huwapa wanafamilia fursa ya kujitenga. Imedhihirika kuwa runinga haichangii kujenga uhusiano bora wa kijamii. Ukilinganisha

na vyombo vingine vya burudani ambavyo hutoa nafasi ya watu kutangamana na kujenga uhusiano bora, televisheni haichangii haya. Badala yake, tajriba ya televisheni huwa ya kibinafsi. Hali hii inapotokea katika kiwango cha familia, televisheni inaweza kutenganisha wazazi na watoto wao.

Halikadhalika, runinga na video aghalabu hueneza maadili yasiyofaa. Mathalani, baadhi ya vipindi vya televisheni huendeleza hulka ya kuhadaa, ngono za kiholela, kuvunjika kwa ndoa, n.k. Hulka hizi zisizoendeleza maadili ya kijamii huchukuliwa kama zinazofaa na zinazofuatwa na waliostaarabika. Huu ni upotovu.

Isitoshe, baadhi ya matangazo huhimiza matumizi ya dawa za kulevya kama tembo na sigara. Vitu hivi vinapotangazwa, hupambwa kwa hila na udanganyifu mwingi ambao huwavutia vijana na watoto wengi. Si ajabu mtu anapouliza wanaotumia vileo hivi walivyoanza, watajibu kutokana na athari za matangazo katika runinga na vyombo vingine.

Utafiti umeonyesha kuwa vipindi vya runinga na video ni chanzo cha matumizi ya nguvu za mabavu miongoni mwa wanafunzi. Wazazi wengi huchukulia vibonzo katika televisheni kuwa vinalenga kuburudisha tu na havina ubaya wowote. Lakini ukweli ni kuwa vipindi vingi vya vibonzo hushirikisha matumizi ya hila na nguvu za mabavu. Haya huibusha hamu ya vijana na watoto huyaiga.

Kwa hivyo, ni muhimu wazazi na jamii kutambua madhara ya televisheni. Utambuzi huu utawafanya wawaelekeze vijana na watoto jinsi ya kutumia televisheni na video ili kuepukana na madhara yake.

a) Fupisha aya tatu za kwanza (maneno 70 – 75) (alama 7, 2 za utiririko)

Matayarisho

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

Jibu

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

b) Eleza udhaifu wa runinga na video. (maneno 50 – 51) (alama 5, 1 ya utiririko)

Matayarisho

2. **MATUMIZI YA LUGHA:** **(alama 40)**

**a)** Taja aina mbili kuu za ala za kutamkia sauti **(alama 2)**

**b)** Taja mfano mmoja mmoja wa sauti zifuatazo **(alama 2)**

Kimadende__________

Kipasuo kwamizo__________

**c)** Huku ukitoa mfano, eleza maana ya sentensi sahili **(alama 2)**

**d)** Ainisha mofimu katika neno lifuatalo; **(alama 3)**

Tulimpikia__________

**e)** Ainisha vitenzi katika sentensi: Kitabu anachotaka kusoma ki mezani **(alama 3)**

**f)** Tunga sentensi moja ukitumia kiunganishi kiteuzi **(alama 2)**

**g)** Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? **(alama 2)**

a) Uzi__________

b) Muda__________

**h)** Tumia 'o' rejeshi ya kati katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Watu ambao walifika jana ni wale ambao walitoka mbali

**i)** Onyesha shamirisho kipozi na ala katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Mwindaji haramu alimuua ndovu kwa bunduki

**j)** Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari au mishale **(alama 3)**

Kilipikwa jana jioni

**k)** Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi **(alama 2)**

Msingesoma kwa bidii, msingepita

**l)** Tunga sentensi moja kudhihirisha dhamira/jukumu hili **(alama 2)**

Rai/ombi

**m)** Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Mtoto ambaye alianguka jana ana maumivu mengi

**n)** Onyesha matumizi yoyote mawili ya kiwakifishi: koma/kituo **(alama 2)**

**o)** Tumia neno 'Nairobi' kama **(alama 2)**

**a)** Nomino

**b)** Kielezi

**p)** Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya kuku na gugu **(alama 2)**

**q)** Onyesha matumizi ya kiambishi -ji- katika sentensi **(alama 2)**

Mwongeleaji stadi anajishaua sana.

**r)** Andika katika usemi wa taarifa **(alama 2)**

"Wageni wangu watafika saa ngapi? Mama aliuliza

**s)** Unda nomino kutokana na kitenzi **(alama 1)**

Safiri

4. **ISIMUJAMII:** **(alama 10)**

Nipe chai, andazi mbili na egg moja…………

a) Taja sajili inayorejelewa na maneno haya **(alama 2)**

b) Fafanua sifa nane zinazohusishwa na sajili hiyo **(alama 8)**

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: ……………………………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ………………DARASA: …...........**

# MTIHANI WA PAMOJA WA LANJET

**102/2**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA PILI**

**<u>MAAGIZO</u>**

***a)*** *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***b)*** *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***c)*** *Jibu maswali* ***yote.***
***d)*** *Majibu yako yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
***e)*** *Majibu yote* **lazima** *yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
***f)*** *Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*
***g)*** ***Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

**Kwa matumizi ya mtahini pekee.**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | **15** | |
| 2 | **15** | |
| 3 | **40** | |
| 4 | **10** | |
| **Jumla** | **80** | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.**

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jamii, uainishaji wake na uathihirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dahari ya miaka. Suala hili huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu msingi mkuu wa uainishaji wa mahusiano hayo ni kukichunguza kipindi cha mahusiano yenyewe. Yapo mahusiano baina ya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache, na mengine ambayo huenda yakachukua miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni yale yanayojulikana kama mahusiano ya kudumu. Inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi kikubwa. Watu wengi huitikadi kuwa uhusiano uliopo baina ya mtu na jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwa hivyo ni uhusiano wa kudumu. Hali hii hutokana na uhalisi kuwa tunahusiana na jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiano huu hautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu; tunaendelea kuwasiliana kwa barua au, katika enzi hii ya utandawazi, kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi, na kudumisha uhusiano wetu wa kijamaa. Hata hivyo, inawezekena baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalan, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu au kipindi kirefu, unaweza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofumbatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili, mahusiano ya koindi cha wastani, kuna mahusiano yanayohusisha marafiki zetu maishani, shuleni au kwenye taasisi zozote zile, majirani zetu, wenzetu katika mwahali mwa kazi, washirika kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea. Inawezekana kudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya, hususan baina ya marafiki na majirani huweza kuwa ya miongo na daima. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfano wa jamii. Kwa mfano, kwa majirani wanaoishi kwenye janibu, fulani mahususi, na kwa miaka tawili bila ya  kuhajiri. Uhusiano wao na majirani huweza kuwa wa kudumu. Hali hii **inasigana** na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini. Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilkikabadilika. Isitoshe, kutokana na mfumo wa maisha ya  kibepari **yameghoshi** ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi uweza kuumomonyoa ukuta wa uhusiano wa kudumu.

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na majirani zao. Uhusiano kati ya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wa majirani. Vimbunga vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo ya kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasa huweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini.

Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujiri katika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa dukani, kwenye sehemu za ibada, kwenye kituo cha mafuta, kwa kinyozi, kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya kuyazungumzia mahusiano ya aina hii kama ya mapito. Kwanza, uwezekano wa mabadiliko ya anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa kinyozi au msusi untambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo, kuna **vighairi** hususa pale ambapo mtoa huduma anayehusika ni yule mmoja.

Mahusiano ya mpito yanatawaliwa na “uhusiano wa chembe chembe”. Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo wa kibepari, unamaanisha kuwa kinachomshughulisha mtu ni chembe ndogo tu ya mwenzake. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma, kwa mfano, gazeti analokuuzia mtu, kiatu anachokushonea, nguo anazokufulia, ususi anaokufanyia n.k. Mahusiano ya aina hii yametovukwa na hisia za utu na ni zao la mifumo ya kisasa na kiuchumi na kijamii. Mtu anayehusiana na mwenzake kwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwezake amekosa chakula, amefutwa kazi, amefiliwa na kadhalika.

Suala kuu tunalopaswa kujiuliza nji: Je, tunahusiana vipi na jamaa zetu, taasisi zetu, marafiki zetu na majirani zetu? Je, uhusiano wetu na raia wenzetu ni w aaina gani? Je, uhusiano wetu na nchi yetu ni wa mpito au ni wa kudumu?

(a) Taja kigezo muhimu cha kuzungumzia mahusiano. (al 1)

……………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(b) Eleza imani ya watu kuhusu uhusiano baina ya jamaa. (al 1)

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(c) Fafanua athari ya technolojia kwenye mahusiano ya watu. (al 2)

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………….

(d) Eleza sababu nne kuu za kuharibika kwa mahusiano katika maisha ya leo. (al 4)

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(e) Taja sifa kuu ya mahusiano ya muda mfupi. (al 2)

…………………………………………………………………………………………………..

(f) Je, kifungu hiki kina ujumbe gani mkuu? (al 2)

………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(g) Eleza maana ya maneno yafutayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. (al 3)

(i) inasigana……………………………………………………………………………………

(ii) yameghoshi…………………………………………………………………………………

(iii)vighairi………………………………………………………………………………...

**UFUPISHO (ALAMA 15)**

Ujambazi wa kimataifa ni tatizo lililowasumbua walimwengu kwa muda mrefu sana. Serikali nyingi zimetumia mapesa mengi kwa miaka mingi sana zikijitahidi kupambana na janga hili. Hata hivyo, fanaka haijapatikana, wala haielekei kamwe kuwa itapatikana leo au karne nyingi baadaye.

Yumkini tatizo kubwa lililopo ni kuhusu jelezi la dhanaya "ujambazi" tena "wa kimataifa". Hili ni tatizo mojawapo na yapo mengi sana. Tatizo la pili ni kiburi. Kuna wale watu binafsi na hasa viongozi w anchi kubwakubwa na serikali zao zilizojiaminisha kuwa ujambaz ni balaa kweli, tena belua, lakini huo ni wa huko, wala hauwezi kuwagusa licha ya kuwashtua wao.

Kulingana na maoni watakaburi hao, ujambazi ni wa watu 'washenzi' wasiostaarabika, wapatikanao katika nchi zisizoendelea bado. Ujambazi peke wanaouona unafaa kukabiliwa ni dhidi ya mbubujiko wa madawa ya kulevya uliosababishwa na vinyagarika kutoka nchi hizo maaluni za "ulimwengu wa tatu". Kulingana na wastaarabu wa nchi zilizoendelea, vinyangarika hivi ndivyo hasa adui mkubwa wa ustaarabu ulimwenguni na ni

sharti vifagiliwe mbali bila huruma. Baada ya kusawasagwa, ulimwengu mstaarabu utazidi kutononoka na ahadi ya mbingu hapa ardhini itakamilika.

Imani ya watu hawa ya kuwa ujambazi wa kimataifa, hata iwapo upo, hauwezi kuwashtua wala kuwatingisha wao ilikuwa kamili na timamu. Ilikuwa kamili na timamu hadi hapo mwezi Septemba tarehe 11 mwaka wa 2001, ndege tatu za abiria zilipoelekezwa katika majumba mawili ya fahari, yenye urefu wa zaidi ya ghorofa mia moja na kuyatwangilia mbali. Mshtuko na kimako! Kimako kwa kuwa, kabla ya siku hiyo, Wamarekani hawangeweza kudhani kwamba ingewezekana taifa lolote au mtu yeyote kuthubutu kushambulia nchi yao, taifa wasifa lililojihami barabara dhidi ya aina yoyote ile ya uchokozi kutoka pembe lo lote la dunia.

Hakuna ulimwenguni mzima, aliyeamini kuwa Marekani ingeweza kushambuliwa. Kwa ajili hiyo, mshtuko uliitingisha ardhi yote na huzuni ilitanda kote, kama kwamba sayari nzima imeshambuliwa, wala sio Marekani pekee.

Mintarafu hiyo, Marekani ilipolipiza kisasi kwa kuwaunguza waliokuwemo na wasiokuwemo kwa mabomu hatari huko Afghanistan, idadi kubwa ya watu duniani ilishangilia na kusherehekea. Kwa bahati mbaya, tafsiri ya shambulizi la minara-pacha na Newyork na lile la Pentagon, uti wa uwezo wa kivita wa Marekani, ulizorota. Kuna wengi waliodhani huo ni mwanzo wa vita vya Waislamu dhidi ya Wakristo na kwa muda, Waislamu wote wakashukiwa kimakosa kuwa ni majambazi wa kimataifa.

(a) Bila kubadilisha maana, fupisha aya tatu za kwanza. (maneno 65 – 75) (al 10, 2 za utiririko)

Nakala safi

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

(b) Ukizingatia aya tatu za mwisho, fafanua fikira za watu na mambo yote yaliyotokea baada ya Septemba tarehe 11, 2001. (maneno 65 – 75) (al 10, 2 za utiririko)

Nakala safi

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

**MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

(a) Silabi ni nini? (al 2)

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(b) Tenga silabi katika maneno yafuatayo kisha uandike aina yake. (al 2)

(i) igwa

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(ii) Oa

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(c) Dhihirisha panapotiwa shadda katika maneno yafuatayo. (al 2)

(i) Galagala …………………………………………………………………………………

(ii) Teketeza ………………………………………………………………………………...

(d) Bainisha nomino katika sentensi zifuatazo kisha utaje aina zake. (al 2)

(i) Uhubiri wa mama huyu una mvuto mkubwa

…………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(ii) Kabati hili limevamiwa na wadudu wengi waharibifu.

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(e) Eleza matumizi ya kihusishi <u>kwa</u> katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Tahadhari huandikwa kwa hati nzito.

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(f) Tenga viambishi na mzizi katika neno lifuatalo. (al 2)

Siji.

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(g) Unda nomino kutokana na kivumishi kifatacho. (al 1)

Tepetevu

…………………………………………………………………………………………………..

(h) Pigia mstari na kuainisha kirai katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Haifai kujenga karubu na nyaya za umeme

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(i) Bainisha shamirisho kitondo katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Mzalendo amemwandikia mhariri barua.

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(j) Eleza kama sentensi ifuatayo ni sahili, ambatano ama changamano. (al 2)

Tulipewa ratiba ya shughuli hiyo lakini hatukuitia maanani

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(k) Bainisha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Simu tamba ambayo ameninunulia imenirahisishia mawasiliano

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(l) Kanusha sentensi ifuatayo. (al 2)

Ninamtarajia mpwa wangu awasili leo

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(m) Andika katika wingi. (al 2)

Huzuni aliyokuwa nayo yatima huyu ilinitia kite na imani.

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(n) Andika kinyume cha neno lililopigwa mstari. (al 1)

Mhalifu huyu <u>alitunga</u> mimba

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(o) Bainisha matumizi ya **KI** katika sentensi ifautayo. (al 1)

Jua limekuwa likiwaka tangu Januari

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(p) Bainisha matumizi ya **ka** katika sentensi ifuatayo: (al 1)

Sungura alifika nyumbani akamsalimu mkewe, akafululiza msalani akaoga

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(q) Akifisha sentensi hii: (al 2)

Mmea wa pareto ni muhimu mno nchini akasema afisa wa kilimo

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(r) Badilisha katika usemi wa taarifa: (al 2)

"Tutakusaidia ikiwa utashirikiana nasi," afisa wa usalama akasem.

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(s) Andika katika ukubwa ukizingatia neno lililopigwa mstari. (al 1)

Aliyerembesha <u>uso</u> kwa poda.

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(t) Bainisha maana mbalimbali za sentensi ifuatayo: (al 3)

Mwalimu amempigia wanafunzi simu

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(u) Silabi mwambatano ni nini? (al 1)

…………………………………………………………………………………………………..

(v) Tunga sentensi moja udhihirishe maana mbili za neno hili: <u>Rudi</u> (al 1)

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………………….

(w) Pigia mstari vivumishi katika sentensi ifuatayo kisha uandike aina yake. (al 2)

Bibi huyu ni mpole uso wake wenye haya huuinamisha kila mara.

………………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………………..

**ISIMU JAMII**

Maenezi ya Kiswahili Afrika mashariki punde baada ya uhuru yalikuwa na chagamoto tele. Fafanua zozote tano. (al 10)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse*)**

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: ……………………………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ………………DARASA: …............**

# MTIHANI WA PAMOJA WA MIRROR

**102/2**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA PILI**

**<u>MAAGIZO</u>**

***a)*** *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***b)*** *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***c)*** *Jibu maswali* ***yote.***
***d)*** *Majibu yako yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
***e)*** *Majibu yote* **lazima** *yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
***f)*** *Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*
***g)*** ***Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

**Kwa matumizi ya mtahini pekee.**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | **15** | |
| 2 | **15** | |
| 3 | **40** | |
| 4 | **10** | |
| **Jumla** | **80** | |


**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

1. **<u>UFAHAMU</u>** (ALAMA 15)

***Soma makala haya kisha ujibu maswali yafuatayo.***

Lugha inaweza kuelezwa kwa jumla kuwa ni mfumo wa mawasiliano. Haiyamkiniki kwa mtu yeyote kueleza chanzo au kiini cha lugha na sote tunakubaliana kuwa matumizi yake yameanza tangu kuumbwa kwa binadamu kwani ni vigumu kukisia kuwepo kwa jamii ya watu bila lugha ya mawasiliano yoyote ile.

Katika taifa lolote, huwapo na lugha moja au hata zaidi ya moja ambayo huwa ndicho chombo cha mawasiliano ya taifa katika nyanja za: elimu, maandishi, siasa na biashara. Kwa mfano, mataifa kama Kanada hutumia lugha mbili kwa usawa kama lugha za taifa na zakikazi. Maana ya lugha ya taifa ni lugha moja ambayo huteuliwa kutumika katika shughuli zote za taifa hasa katika nchi yenye lugha nyingi za kikabila. Lugha ya taifa ni muhimu sana kwa maisha na maendeleo ya taifa lolote lile. Lugha hii huwa ndiyo kiungo cha kuenezea umoja na uelewano miongoni mwa jamii nyingi tofauti na huwa kama kitambulisho kwao kuwa wao ni ndugu wajamii moja kubwa, yaani taifa lao.

Kenya ni mfano mzuri wa taifa lenye lugha nyingi zinazozidi 40 za vikundi vidogo vidogo vya kikabila. Hapo kabla ya miaka mia moja hivi iliyopita kila kimojawapo cha kikundi hiki kilijitambulisha kama kabila huru. Baada ya kuja kwa Serikali ya Kikoloni na hasa baada ya Kenya kujinyakulia uhuru, haja ya kuunganisha raia wote chini ya taifa moja lenye uongozi na shabaha moja ilikuwa ndilo jambo lililozingatiwa sana. Kwa hivyo utamaduni wa taifa la Kenya ni mchanganyiko wa tamaduni za watu wengi wenye mila, desturi, imani na itikadi tofauti. Utamaduni humaanisha jumla ya amali na tabia za watu wa jamii fulani. Amali hizi zinafungamanisha fikira, ustaarabu, mila, taasisi na sanaa za aina zote za jamii inayohusika. Ili kujieneza na kujiimarisha, taifa huhitaji chombo hicho kuwasiliana na kuwaunganisha watu wake wenye asili mbalimbali. Chombo hicho huwa ni lugha ambayo siyo tu kwamba ni sehemu ya utamaduni wa jamii bali pia ni njia muhimu sana ya kutawanyia na kustawishia ule utamaduni.

Katika taifa lenye lugha nyingi kama Kenya kwa mfano, lugha ya taifa inayozungumzwa na kueleweka na baadhi kubwa ya raia ambayo imekiuka mipaka na tofauti za kikabila ni njia muhimu sana ya kuenezea maongozi ya taifa na kuleta ufahamikiano bora kote nchini. Kama zilivyo taasisi kama wimbo wa taifa, bendera ya taifa au bunge la taifa, lugha ya taifa ndicho kielelezo cha taifa lolote lile lililo huru. Lugha kama hiyo huvunja na kukomesha hisia za kibinafsi na kikabila na badala yake kuunda moyo wa uaminifu wa kitaifa.

Zaidi ya kuwa chombo cha mawasiliano, lugha ni kielelezo cha fikra na hisia za binadamu. Lugha ya watu fulani haituelezi tu ujuzi au maarifa yao bali pia mtazamo wao wa kimaisha, falsafa na mawazo yao. Kwa ufupi lugha hutufahamisha namna akili za watu waizungumzayo ile lugha zinavyofikiri na kufanya maazimio.

Lugha ni sehemu ya utamaduni wa taifa tulimozaliwa na lazima lugha hiyo ifunzwe katika muktadha wa maisha ya jamii ihusikayo.

Utamaduni wa jamii hautenganiki na lugha yake.

**Maswali**

a) Dhana lugha ina maana gani kulingana na kifungu? (alama 2)

b) Eleza tofauti baina ya lugha ya taifa na lugha ya kazi. (alama 4)

c) Kwa mujibu wa kifungu lugha ya taifa ina manufaa gani. (alama 4)

d) Kuna uhusiano gani baina ya lugha na utamaduni. (alama 2)

e) Eleza maana ya maneno haya kulingana na taarifa. (alama 3)

i) Muktadha

ii) Kielelezo

iii) Haiyamkiniki

**2. UFUPISHO (ALAMA 15)**

Visa vya dhuluma za kinyumbani vimeongezeka hivi majuzi, huku wanawake wakiangaziwa zaidi kwa kuwapiga waume zao. Kwa muda mrefu, visa ambavyo vimekuwa vikishuhudiwa ni vya wanaume dhidi ya wake zao. Ni wazi kwamba wanaume kwa mara nyingi wanaopitia matatizo huogopa kuyatangaza hadharani.

Hali ya kiuchumi imeathiri pakubwa familia nyingi. Pesa za kugharamia mahitaji muhimu kama chakula, mavazi na makazi zimekuwa adimu. Jambo hili linasababisha mivutano baina ya mume na mke inayoishia vita na wahusika kujeruhiwa. Wengine wameyapoteza maisha yao na wengine kulemaa kwa mili yao daima dawamu.

Wake kwa waume wameyapuuza majukumu yao katika ndoa. Kuna waume ambao wanatumia mapato yao na ya familia kwa kupiga maji. Waume kama hawa hujigamba kuwa wao ni wakwasi na huwanunulia wenzao mvinyo huku familia zao zikiteseka kwa umaskini. Waume na wake walevi huwatukana wenzao na kwa hivyo migogoro katika ndoa kama hizi huwa haikomi.

Wanandoa wengine wanajihusisha na mapenzi nje ya ndoa licha ya kula kiapo cha uaminifu wakioana. Usaliti huu hufanya watu wengine kulipiza kisasi kwa kuwapiga wenzao au kutomakinika katika ndoa. Matatizo ya kisaikolojia yamewafanya watu kushindwa kuzidhibiti hisia zao. Kutoelewana kunapozuka, wao hupandwa na hamaki na huenda wakawatesa wake na waume zao.

Ukosefu wa nasaha kwa wanandoa wengi umeleta shida nyingi. Wengi hawaelewi namna ya kutatua matatizo ya nyumbani. Kuna njia tofauti za kuepuka dhuluma nyumbani. Wanandoa wanafaa kudumisha upendo wa dhati kila wakati. Wake kwa waume sharti watekeleze majukumu yao nyumbani bila kuyaepuka. Mapenzi nche ya ndoa lazima yatupiliwe mbali ili muamana unaofaa uwepo.

Licha ya changamoto tofauti katika ndoa, wanaohusika wanafaa wavumilie na kujaribu kuzika tofauti zao katika kaburi la sahau.  Hawafai kuweka rekodi ya makosa ambayo wametendeana. Wosia unafaa kutolewa kwa wake na waume wote ili waelewe mikakati ya kukabiliana na matatizo mbali mbali yanayokumba ndoa.

Viongozi wa kidini wafundishe watu maadali mema ili watu waepuke tamaa za kimwili zinazowasonga na kujihusisha na mapenzi nje ya ndoa.

Ndoa inafaa iheshimiwe na watu wote kwani ndio msingi wa taasisi zile zingine kama jamii na nchi. Mawasiliano yanafaa yaimarishwe katika ndoa. Kukiwa na mazungumzo, matatizo mengi yatajadiliwa na kusuluhishwa ili kuepukana na dhuluma za aina zozote.

a) Eleza kiini cha dhuluma za kinyumbani. (Maneno 40 – 50) (alama 6)

**Matayarisho**

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**Nakala safi**

b) Fupisha aya nne za mwisho ukizingatia ujumbe muhimu (maneno 60 – 70) (alama 9)

**Jibu**

**3. <u>MATUMIZI YA LUGHA</u>** (ALAMA 40)

a) Taja sifa za irabu hizi /i/ na /e/ (alama 2)

b) Tenganisha viambishi vilivyojenga neno lifuatalo: (alama 2)

Tunakumbuka

c) Vitenzi vya Kiswahili hugawika katika vikundi viwili vikuu. Vitaje. (alama 1)

d) Andika nomino mbili zinazoweza kuundwa kutokana na kitenzi ulichopewa: (alama 2)

Saili

e) Tambulisha matumizi ya ‘kwa’ katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Alisababisha ajali <u>kwa</u> ulevi wake.

f) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia kielelezo cha mshale: (alama 4)

Omari atafika kesho jioni

g) Akifisha sentensi ifuatayo:

hoteli ya shelter afrique iliyoko jijini inapigwa mnada baada ya miezi miwili ya kufanya biashara

(alama 2)

h) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya kuyakinisha:

Mchoraji hachori picha nzuri (alama 1)

i) Onyesha aina za nomino hizi: (alama 2)

Jini ______________________________

Wizi ______________________________

j) Onyesha shadda katika maneno yafuatayo: (alama 1)

Meza ______________________________

Linganisha ______________________________

k) Andika sentensi ifuatayo upya kwa msemo wa taarifa: (alama 5)

“Sikiliza bwana mdogo, siku hizi tunaishi katika jamii ambayo imebadilika. Hayo mawazo yako ya zama kongwe hayatakufikisha popote,” alifyoa Kameme.

l) Bainisha shamirisho kipozi na shamirisho kitondo katika sentensi hii: (alama 2)

Okoth alinunuliwa redio nzuri na mjomba wake aliyekuwa ng’ambo.

m) Kanusha neno hili: (alama 1)

Wakimenyanamenyana

n) Onyesha matumizi ya ‘ni’ katika sentensi hizi:

i) Yule mwanafunzi <u>ni</u> stadi sana (alama 2)

ii) Nitawapeleke<u>ni</u> mahakamani

o) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kugeuza neno lililopigiwa mstari kuwa nomino: (alama 2)

Tulipokwenda hotelini <u>tulikula</u> chapati na nyama.

p) Bainisha mofimu katika neno lifuatalo: (alama 2)

Jimbi

q) Eleza matumizi ya '<u>ku</u>' katika sentensi ifuatayo:

Kulikoharibika ni kwa kuogopwa (alama 2)

r) Sentensi ifuatayo inatekeleza jukumu lipi?

Acheni kucheka ovyo! (alama 2)

s) Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi:

Yule mtoto asipoanguka, sitalaumiwa (alama 2)

t) Eleza maana ya kiimbo (alama 1)

**4. <u>ISIMU JAMII</u>** (ALAMA 10)

a) Eleza maana ya isimu jamii. (alama 1)

b) Eleza maana ya dhana zifuatazo za isimu jamii: (alama 3)

i) Msimbo

ii) Lafudhi

iii) Lugha

c) Eleza sifa sita za lugha ya mahakamani. (alama 6)

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: …………………………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ………………DARASA: …............**

# MTIHANI WA PAMOJA WA MOKASA

**102/2**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA PILI**

**<u>MAAGIZO</u>**

***a)*** *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***b)*** *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***c)*** *Jibu maswali* ***yote.***
***d)*** *Majibu yako yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
***e)*** *Majibu yote* **lazima** *yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
***f)*** *Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*
***g)*** ***Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

**Kwa matumizi ya mtahini pekee.**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | **15** | |
| 2 | **15** | |
| 3 | **40** | |
| 4 | **10** | |
| **Jumla** | **80** | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

1. **UFAHAMU: (Alama 15)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Tumeshuhudia baadhi ya ndugu wa familia moja wakiishi bila maelewano na wakati mwingine kukata kabisa kabisa mawasiliano. Hivi leo kuna familia ambazo haziwezi kuketi pamoja na kumaliza matatizo yao, na badala yake huchukua njia za vita ugomvi na hata pengine mauaji kama suluhisho la migogoro yao.

Kawaida maisha sio mstari mnyoofu. Kuna milima,mabonde,kona na hata mashimo. Ndiposa migogoro ni sehemu ya maisha yetu! Mara nyingi **haiepukiki**, isipokuwa kuipitia na kupata suluhisho. Ipo migogoro baina ya ndugu ambayo huleta kutoelewana,kukosesha amani nahata pengine kupoteza kabisa mahusiano. Ni wazi kuwa mahali popote wanapoishi watu au kufanya kazi pamoja, hapakosekani migogoro kwani hata vikombe vinapokuwa kabatini, havikosi kugongana.

Ukweli ni kwamba sote tunazaliwa na tabia tofauti, uwezo tofauti wa kuvumilia na hata kuamua kutenda. Katika mazingira yoyote ya kutoelewana, kiasi kikubwa cha busara, upendo, amani na imani huhitajika ili kuiondoa migogoro hiyo. Isipotafutiwa suluhisho ama utatuzi wake ukatendeka kwa jazba na chuki, migogoro ya ndugu katika familia hukua na kuzaa madhara makubwa.

Kuanzia utotoni au hadi uzimani, kunaweza kuwa na sababu nyingi ambazo huweza kupelekea kuleta tofauti baina ya ndugu. Kwa ujumla, ndugu ni watu unaowaamini, ambao hawatakupa kisogo. Walakini, hii sio wakati wote. Kwa bahati mbaya ukweli umetuonyesha kuwa kuna uhusiano wa kindugu ambao huisha vibaya. Sababu kubwa zikiwa ni mazingira ambayo ndugu wameishi ambayo wakati mwingine kuna upendeleo wa mzazi kwa mtoto au watoto fulani na kuwafanya wengine wahisi wivu, kutopendwa na kutengwa.

Zipo sababu za kiuchumi ambapo ndugu wengine katika familia wanafanikiwa zaidi kuliko wengine na kuwa na maisha bora zaidi kuliko wengine. Hali hii pia inaweza kuleta mfarakano kwa wale ambao hali zao ni tofauti na wengine, hasa iwapo hakukuwa na mazingira ya utangamano katika familia tangu awali.

Ndugu wa familia moja huzaliwa wakiwa na tabia tofauti. Kila mshiriki wa familia ana **haiba** na mtazamo wake tofauti katika masuala mbalimbali. Wengine hukasirika mara kwa mara, wengine ni wakimya sana, wapo walio wakorofi na wengine wanaopenda amani, hivyo jambo hili ni muhimu mno kulielewa mara inapotokea migogoro ili kutamua namna ya kupata suluhisho.

Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba migogoro hii wakati mwingine hupelekea kuvuruga mwelekeo wa maisha ya watoto hasa wakati wa ukuaji, kwani kulingana na tofauti zao, wapo wale wanaoamua kuondoka nyumbani wakiwa bado na umri mdogo na kuhamia mitaani.

Pamoja na migogoro kuwepo katika familia zetu ni vyema wazazi ama walezi waelewe tofauti za kifamilia zinavyoweza kuchangia mfarakano baina ya ndugu wa familia moja. Kwamba mzazi ama mlezi anapompendelea mtoto mmoja na kutokuwa karibu na mwingine, anatengeneza mazingira ya tofauti baina ya watoto wake. Ni vyema kuweka uwiano sawa baina ya watoto na familia ili kuweza kupunguza tofauti zinazoweza kujitokeza.

**Maswali**

(a).Onyesha athari **tatu** za migogoro miongoni mwa ndugu katika familia. (Alama 3)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

(b). Eleza mambo **matano** yanayochangia kuwepo kwa watoto wanaorandaranda mitaani kwa kurejelea kifungu. (Alama 5)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

(c). Malezi yanachangia migogoro baina ya ndugu. Thibitisha kwa kurejelea kifungu. (alama. 1)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

(d). Taja na ueleze mbinu nne za kimtindo zilizotumika katika kifungu. (alama. 4)

………………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

(e). Andika visawe vya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu. (alama.2)

(i) haiepukiki

…………………………………………………………………………………………………..

(ii). haiba

……………………………………………………………………………………………………

2. **MUHTASARI**

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Migongoni mwa starehe ambazo Waswahili wamezihifadhi mpaka leo ni kutoleana hadithi na kutegeana vitendawili. Starehe hizo ambazo kwa kawaida hufanywa nje huwa njiani au uani, ama ndani chumbani au ukumbini, aghalabu hufanywa wakati wa magharibi au usiku baada ya kila mtu kumaliza kazi ya nyumbani,dukani,shambani,ofisini na kadhalika. Mambo haya yakitazamwa sana itaonekana kuwa hayakufanywa vivi hivi.

Tangu zamani wazee wa Kiswahili waliwakataza wana wao kucheza mchana. Hawakupenda vijana wajizoeshe uvivu kwa kupiga malapa. Walisadiki kuwa mwana ambaye hakukanywa dhidi ya utiriri huu hangeweza kujifaa yeye mwenyewe na wala hata watu wengine. Isitoshe nani
Asiyejua kuwa ajizi ninyumba ya njaa:Vijana walilimizwa kusaidia katika makazi mbali mbali yanayofanywa majumbani, mashambani na mahali popote palipohisiwa kuwa mtu angalifanyiwa jambo la kumpa riziki. Ndiposa ungesikia wazee wakiwaambia watoto wao, ‘ukisimulia hadithi mchana utaota mkia’. Ingawa kwa

watu wazima maneno haya yangekuwa masihara,kwa watoto yaliaminika sana kwa hivyo wazazi wakapata mradi wao. Hi ndiyo maana Waswahili wanasimuliana hadithi na kutegeana vitendawili jioni au usiku.

Wazazi ambao hawataki watoto wao watembeetembee au wacheze michezo ambayo itawafanya wakimbiekimbie na kujihasiri huwatia ndani ili wawe nao kuanzia magharibi. Waswahili wana itikadi nyingi zinazohusiana wakati wa magharibi. Ni ajabu kuwasikia wakisema kuwa magharibi huwaleta pamoja na kutoleana hadithi. Na hata kama si hivyo hii ni fursa nzuri kwa wazazi kuzungumza na watoto wao ambao kutwa nzima huwa hawakupata nafasi kuwa nao.

Starehe hizi pia huongeza elimu, na kama wahenga wasemavyo, elimu ni mwanga uangazao.. Kwa mfano watoto watategewa vitendawili, jambo hili litawafanya wafikiri. Na kufikiri huku kutawafanya wavumbue mambo mengi ambayo mengine hapo awali hawakuyajua na kuyathamini. Vile vile huwafunza werevu wa kufumba na kufumbua mafumbo ambayo elimu inayohitaji kiwango kikubwa cha busara.

Kutoleana hadithi ni miongoni mwa starehe ambazo kwazo hujifunza mambo mengi sana. Katika hadithi watoto wanaweza kujifunza mambo yanayohusu mila na desturi, katika mambo haya watu hujifunza tabia nzuri, heshima na uvumilivu. Pia katika hadithi mtu anaweza kujifunza mambo ya historia na pia ya mazingira aliyoyazoea na hata mambo ambayo hayajui.

Aidha hadithi ni chombo ambacho wazee hukitumia kuwafundisha watoto mbinu za kuzungumzia. Wazee wenye busara aghalabu huwapa nafasi watoto wao wabuni na wasimulie hadithi zao. Wakati mwingine jamaa mbili jirani huweza kukutana kufanya mashindano ya kutambiana hadithi. Mazoezi kama haya huwawezesha vijana kufikia viwango vya juu vya ufasaha na matumizi ya lugha na ujasiri na ukakamavu wa kuweza kusema mbele za hadhira kubwa katika maisha yao. Baadhi ya watambaji wakubwa waliopata kusifiwa haikosi mwanzo wao ulikuwa wa namna hii. Hadithi pia huwafundisha watu kuhusu maisha duniani. Zinaweza kuwafunza jinsi ya kuishi na ndugu, majirani, marafiki, wake au waume. Ulimwenguni humu tunamoishi na mambo mengi yanoyomtatiza binadamu kwa namna mbalimbali. Hadithi zinaweza kupendekeza mambo ya kufanya na kuonyesha njia zenye mapato mema tunapofikiwa na hadhaa kadhaa. Zinaweza pia kukanya kiburi na kuonyesha faida ya kutosema uwongo ama kuishi katika maisha yasiyo muruwa, yaliyojaa kiburi na majivuno. Hapana shaka hadithi zinaweza kuongoza na kuwafanya wawe watiifu na raia wema katika nchi zao.

**Maswali**

(a). Kwa nini mwandishi akaoanisha utambaji wa hadithi na wakati wa jioni? (Maneno 40)
(alama 5, alama 1 ya mtiririko)

**Nakala chafu**

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………..………………

……………………………………………………………………………………..……………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………..………………………………………………………………………………

……………….………………………………………………………………………………………………..…

………………………………………………………………………………………………..…………….

(b). Kwa maneno kati ya 70 na 90 eleza umuhimu wa kutambiana hadithi na kutegeana vitendawili,kulingana na mwandishi. **( Alama 8, 1 ya mtiririko)**

**Nakala chafu**

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………..………………………………………………………………………………

……………………..………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….………………………

…………………………………………………………………………..……………………………………

……………………………………………………………………………………………….………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….………………………

…………………………………………………………………………..……………………………………

**3. MATUMIZI YA LUGHA** **(Alama 40)**

(a). Andika neno lenye kikwamizo sighuna cha ufizi, irabu ya mbele wastani, nazali ya midomo na irabu ya chini kati. (alama 2)

………………………………………………………………………………………….………………………

……………………………………………………………………………..……………

…………………………………………………………………………………………….……

(b). Eleza muundo wa silabi katika neno <u>mbilikimo.</u> (Alama1)

……………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………….

(c). Andika upya kwa kutumia 'o'-rejeshi tamati.

Majarida ambayo yatasomwa yameagizwa (alama. 1)

……………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………….

(d). Tunga sentensi zifuatazo (alama 2)

i) Arifu

………………………………………………………………………………………………………

ii) Rai

………………………………………………………………………………………………………

e) Tunga sentensi moja yenye kiwakilishi cha A-unganifu,kitenzi kishirikishi kipungufu na kijalizo

(alama.2)

………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

f) Andika sentensi zifuatayo katika hali ya udogo (Alama 2)

Mbuzi wake amekaata kamba akaingia shambani na kula mahindi.

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

g). Andika katika usemi wa taarifa (Alama 2)

"Wanasiasa hawa wenu wakipigana hivi wataharibu nchi" Rais alisema.

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

h). Changanua sentensi kwa jedwali. (alama.4)

Jirani aliyenisaidia juzi ataondoka mwakani.

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

i). Onyesha yambwa katika sentensi ifuatayo

Alawi alifumiwa mkeka mzuri na shangaziye kwa miyaa. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

j). Eleza tofauti ya kisarufi ya maneno yaliyopigia mstari (alama.2)

i) Duka <u>la mwalimu</u> limechomeka

……………………………………………………………………………………………….

ii) Duka <u>la</u> mwalimu limechomeka

……………………………………………………………………………………………..

k). Tunga sentensi kuonyesha wakati ujao, hali ya mazoea (Alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………….

l(I). Tumia neno pongezi katika sentensi kama (Alama 2)

i). Nomino

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

(ii). Kihisishi

…………………………………………………………………………………………………

m). Eleza matumizi ya ‘na’ katika sentensi ifuatayo:Ridhaa na Mwangeka walikuwa wameketi karibu na jumba lakifahari walipoitwa na Apondi. (alama.3)

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

n). Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo

(i). Mwana <u>mwadilifu</u> huwaletea wazaziwe fahari. (alama 1).

*( Badilisha neno lililopigiwa mstari kuwa nomino.)*

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

(ii). <u>Nyota nyingi</u> ziliipamba anga usiku huo. (alama 1)

*(Tumia nomino ya jamii badala ya maneno yaliyopigiwa mstari)*

……………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………

(iii). Makokha ni mkakamavua Onyango ni mkakamavu pia. (alama 1)

*(Unganisha iwe sentensi moja yenye kihusishi cha kulinganisha.)*

……………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………

(iv). 'Kibali,nionyehse ulipoandika zoezi hilo.'Mwalimu alisema. (alama.1)

*(Tumia kiwakilishi nafasi badala ya nomino ya pekee.)*

……………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………

o). Kwa kutunga sentensi, onyesha ngeli mbili za neno '**upwa**' (alama.2).

……………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

p). Andika maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii. (alama.2)

Selume alimsimulia Ridhaa kisa chake.

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

q). Tunga sentensi moja kubainisha maana mbili za neno. (alama.2)

Kina

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

r). Rubani ni kwa ndege,…………ni kwa meli na……………..ni kwa matwana. (alama 2)

**ISIMU JAMII** **(Alama 10)**

Wewe ni mtaalamu wa maswala ya usalama. Umepewa fursa kuhutubia warsha inayojumuisha maafisa wa usalama kutoka katika vikosi mbalimbali kuhusu jukumu lao katika kudumisha usalama,amani na maridhiano nchini.

(a). Taja sajili ambayo utatumia kisha ueleze sababu ya jibu lako. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

(b). Andika huku ukifafanua vipengele vinane vya kimtindo utakavyotumia kufanikisha mazungumzo yako. (alama 8)

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: ……………………………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ………………DARASA: …...........**

# MTIHANI WA PAMOJA WA MOMALICHE

**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**

**MAAGIZO**

***a)*** *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***b)*** *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***c)*** *Jibu maswali* ***yote.***
***d)*** *Majibu yako yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
***e)*** *Majibu yote* **lazima** *yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
***f)*** *Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*
***g)*** ***Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

**Kwa matumizi ya mtahini pekee.**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | **15** | |
| 2 | **15** | |
| 3 | **40** | |
| 4 | **10** | |
| **Jumla** | **80** | |


**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

## 1. UFAHAMU (Alama 15)

***Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali***

Huku ulimwengu unapoingia katika teknologia ya tarakilishi na sera ya utandaridhi, ukweli wa mambo ni kuwa akina mama wamezinduka. Suala la usawa wa kijinsia limeanza kushamiri kote duniani na ole wake mwanamume yeyote ambaye hajawa tayari kutembea na majira. Lakini hebu tuchunguze jambo hili kwa makini zaidi.

Usawa wa jinsia ni nini? Usawa wa kijinsia ni usawa wa binadamu wote; wawe wake au waume. Usawa huu unapaswa kudhihirika katika kugawa nafasi za kazi, utoaji wa elimu, nafasi za uongozi na nyanja nyinginezo zozote za maisha.

Ubaguzi wa aina yoyote ile hasa dhidi ya mwanamke ni jambo linalokabiliwa na vita vikali sana ulimwenguni kote.

Dahari na dahari, hasa katika jamii za kiafrika, kumekuwa na imani isiyotingisika kuwa mwanamke ni kiumbe duni akilinganishwa na mwanaume. Kwa hivyo mwanamke amekuwa akifanyiwa kila aina ya dhuluma ikiwepo kupigwa, kutukanwa, kudharauliwa, kunyimwa haki zake, kunyimwa heshima na mambo kama hayo. Lakini je, ni kweli kuwa mwanamke ni kiumbe duni asiyefaa kutendewa haki?

Tukichunguza jamii kwa makini tunaweza kuona mara moja kuwa hivyo ni imani potofu isiyo na mashiko yoyote. Ukiimulika familia yoyote ile iliyopiga hatua kimaendeleo, uwezekano mkubwa ni kuwa mume na mke wa familia inayohusika wana ushirikiano mkubwa. Mume anamthamini mke wake na hadiriki kufanya maamuzi muhimu yanayoweza kuathiri maendeleo ya familia bila kumhusisha mke. Mume kama huyo huketi na mkewe, wakishauriana na kufikia uamuzi bora.

Tukitoka katika muktadha wa kifamilia na kumulika ulimwengu wa kazi iwe ni katika afisi za kiserikali au kwenye makampuni binafsi, ukweli ni kwamba kiongozi yeyote yule aliyefaulu katika usimamizi wake mara nyingi huwa na mke nyumbani ambaye wanashauriana kila uchao kuhusu kazi anayofanya hata kama mke hafanyi kazi mahali pale. Hisia na mawaidha anayotoa mke kwa mume wake ni tunu na huenda asiyapate kwingineko kokote hata katika vitabu vya kupigiwa mifano. Hii ni mojawapo ya sababu ambayo huwafanya viongozi wa nchi mbalimbali kupenda sana kuwatambulisha wake na familia zao waziwazi kwa vile wanajua kuwa jamii inathamini sana msingi wa jamii. Kiongozi ambaye hana mke au familia au yule ambaye mke wake hatambuliki, hutiwa mashaka na jamii hata kama ni kiongozi aliye na azma ya kushikilia kazi ngumu ya kuongoza umma.

Tukirudi nyuma kidogo na kupiga darubini mataifa ya mbali, tunaweza kuwaona wanawake mashuhuri walio uongozini ambao hadi waleo unapigiwa mfano. Wanawake mashuhuri waliotoa uongozini ambao hadi waleo unapigiwa mfano. Wanawake hao walisimamia mojawapo ya mataifa yenye uwezo na ushawishi mkubwa zaidi duniani. Ingawa wengi wao sasa wameng'atuka, uongozi wao bado unakumbukwa hata baada ya miaka mingi ya wao kuamua kupumzika, Mifano ni kama: Bi Margaret Thatcher aliyekuwa waziri mkuu wa

Uingereza, Bi Bandranaike wa Sri Lanka, Golda Meir wa Israel na wengine wengi katika mataifa kama Indonesia, Ufilipino, Bangladesh, Pakistani na kwingineko.

Katika kufikia tamati, tunapozungumza kuhusu jinsia, hatuna budi kugusia kitafsili masuala nyeti. Kwanza, imani ya kushikilia kikiki tamaduni zisizofaa, ni jambo linalofaa kuchunguzwa kw makini. Kwa mfano, kuna badhi ya jamii ambazo humlazimu mke kurithiwa baada ya kifo cha mumewe. Vile vile baadhi ya jamii za kiafrika zinashikilia kuwa mwanamke hana haki ya kurithi. Kutokana na imani hii, wanawake wengi huishi maisha ya taabu baada ya kutengana na waume zao kwa vile hawana haki ya kurithi chochote kutoka kwa wazazi wao hata kama wazazi hao wana mali nyingi kupindikukia. Mali ya wazazi ni haki ya watoto wa kiume wala si watoto wa kike! Hili ni jambo la kusikitisha mno.

Isitoshe, wanawake hukumbwa na kizingiti kingine wanapojaribu kumiliki mali ya waume zao baada ya waume hao kukata kamba. Sababu ni kuwa, baada ya hao wenda zao kuwekwa kaburini, vita vya umiliki wa mali huanza mara moja na mwishowe yule mke maskini hujikuta hana hata mahali pa kulala sembuse mali waliyochuma na mali yake yote kunyakuliwa na aila ya mumewe . Jambo hili linaonyesha namna tulivyoachwa nyuma na uhalisia wa mambo. Ni lazima jamii izinduke na itoke kwenye kiza hiki chenye maki nzito.

**MASWALI**

(a) Ina maana gani kusema kuwa wanaume hawana budi "kutembea na majira?" (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(b) Kabla ya uzinduzi huu kuhusu usawa wa kijinsia, wanawake wamekuwa wakitendewa dhuluma za kila aina. Taja tatu. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(c) Je, ni kwa nini viongozi wengi hupenda kujitambulisha na familia zao? (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(d) Je, unaamini kuwa hisia na mawaidha anayotoa mke kwa mume wake ni tunu na huenda yasipatikane kwingineko? Fafanua (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(e) Je licha ya kunyimwa haki yake ya kujiamulia, ni matatizo yapi mengine yanayoweza kumukumba mke anayelazimishwa kurithiwa? (alama 3)

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………_

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo jinsi yalivyotumiwa katika muktadha. (alama 3)

Kushamiri………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

Hulka……………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

Azma……………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

**MUKHTASARI (Alama 15)**

***Soma taarifa ifuatayo kasha ujibu maswali yatakayofuata.***

Binadamu hupenda kujivika vilemba vingi mno.Tunapenda kuheshimiwa na kutukuzwa na kila mtu. Tunapenda kuombwa ushauri na wote ambao wanahitaji ushauri! Tunapenda kutambuliwa popote tuendapo.

Watu wengi hukataa kufanya jambo la halali kwa kuhofia kuitwa wajinga. Mfano mzuri ni pale ambapo mtu amekosea kidogo katika kutenda jambo; utaona kuwa mtu huyo anaona ugumu wa kuomba radhi au samahani ati kwa sababu ataonekana mjinga.

Je, ni mara ngapi mkurugenzi ameita mkutano na katika barua yake akatisha kuwaadhibu watakaochelewa na mwishowe ni yeye mwenyewe anayechelewa? Tena huwa haombi msamaha. Ataulaumu usingizi uliomchukua, au gari lililomleta.

Aghalabu tunapowakuza watoto wetu, tunawafunza maadili mema. Tunawahimiza wale wadogo kwamba ni vizuri kuomba radhi kwa wakubwa wako unapowakosea. Lakini kumbuka kwamba kukosea ni kwa binadamu wote. Mtu anaweza kukukosea kwa makusudi au kwa bahati mbaya. Kwa hivyo tunapaswa kufahamu kwamba, tunapofanya makosa ni lazima tuombe msamaha, iwe ni kwa wakubwa au kwa wadogo, ili kuondoa kero.

Waja wengi huogopa kusimama mbele za watu na kuwasilisha au kutenda jambo fulani. Kisa na maana, mtu hataki kutenda jambo fulani halafu akosee. Hajiamini na anaogopa kuwa huenda watu wakaona kasoro yake. Lakini kumbuka, kukosa njia ndiko kuijua.

Huenda ikawa watu wanajadili maswala ibuka kama vile ufisadi, kuavya mimba, matumizi ya dawa za kulevya, ukimwi, uzuiaji wa kizazi na kadhalika... labda huyaungi mkono maoni ya watu wengine kwa sababu ya imani na maadili yako. Hata hivyo, hutaki kusimama ukatoa msimamo wako mbele za watu ingawa dhamiri yako imekwazika. Baadaye utasikika ukiwalaumu watu wengine ilhali ulikataa kusimama na kutetea msimamo wako.

Wengi wetu hujichukua kuwa watu muhimu sana. Wanaona kuwa sherehe au mkutano wowote hauwezi kufaulu ikiwa wao hawako. Wanapokuwa kwenye hiyo mikutano wao hutaka watambuliwe. Hupenda majina

yao yatajwe. Haya huwaridhisha , lakini swali ni je, kuwepo kwao ni muhimu kiasi hicho? Kumbuka kwamba mkutano ungeendelea vizuri bila kuwepo kwao. Kwa hivyo, tusiwe watu wa kutaka kutambuliwa kila tunapoenda mahali. Pia, tusilalamike ikiwa hatukuhusishwa katika jambo fulani.

Unaposhuhudia jambo fulani, kama wizi au ajali, usiwe na woga wa kutoa usaidizi kwa kutoa ushuhuda. Wengine hata huogopa kutoa usaidizi huo, hata kwa manusura wa ajali za barabarani, eti kwa sababu wanahofia kuitwa mahakamani kutoa ushuhuda. Kuna shida gani kuenda kusema yale uliyoyashuhudia bila kuongeza au kutoa chochote?

**MASWALI**

a) Bila kupoteza maana, fupisha aya ya kwanza hadi ya nne.(maneno 60) (alama 7)

***Jibu:***

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

b) Fupisha aya nne za mwisho. (maneno 50) (alama 7)

***Jibu:***

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**MATUMIZI YA LUGHA** **(Alama 40)**

a. Taja tofauti iliyopo kati ya sauti /f/ na /v/ (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

b. Andika sentensi ifuatayo ukitumia kinyume cha neno lililoandikwa kwa herufi ya mlazo: (alama 1)

Binadamu hawezi *kumuumba* mwenzake.

……………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

c. Andika sentensi ifuatayo upya ukizingatia kisawe cha neno lililopigwa mstari: (alama 1)

Mtoto mwenye hamaki hawezi kuelewa maagizo.

……………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

d. Andika kwa usemi halisi: (alama 3)

Yule mshukiwa aliyekamatwa na polisi alisema kuwa papo hapo ndipo alipoficha ule mkufu.

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

e. Tunga sentensi inayoshirikisha nomino uliyopewa pamoja na vipashio vifuatavyo vya sarufi: kivumishi kisisitizi, kitenzi kishirikishi, kitenzi, na kielezi cha wakati. (alama2)

Pinde……………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

f. Sahihisha sentensi zifuatazo :

(i)Ndegwa alipeana kalamu yake kwa mwanafunzi. (alama 1)

……………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

(ii)Siku hizi mahitaji imezidi na pesa haitoshi. (alama 1)

……………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

g. Tunga sentensi mbili kubainisha maana mbili tofauti za neno: **rudi.** (alama 2)

(i)

……………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

(ii)

……………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

h. Akifisha: (alama 2)

Mtume asimame nusura aingie kwenye shimo la taka

…………………………………………………………………………………………………………

i. Unda nomino kutokana na kivumishi:**refu** (alama 1)

……………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

j. Onyesha chagizo katika sentensi ifuatayo: (alama 1)

Watu wanne walipeperushwa juu kwa juu na upepo mkali.

……………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

k. Tunga sentensi ukitumia**: isije ikawa** (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

l. Andika upya sentensi ifuatayo ukitumia virejeshi vya tamati: (alama 2)

Mwanafunzi anayefanikiwa maishani ni yule anayesoma kwa bidii na pia anayewatii wazazi wake.

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

m. Ainisha viambishi awali na tamati katika sentensi: **Anikumbukaye** (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

n. Kanusha kwa udogo: Mwizi aliiba kikapu na ng'ombe. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

o. Andika umoja wa sentensi: (alama 1)

Kwato za wanyama hutufaidi.

……………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

p. Andika kwa wingi : (alama 4)

Wimbi hilo la maji lilimhofisha mvuvi akashindwa kutupa wavu wake majini.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

q. Andika katika hali ya kutendewa: (alama 2)

Kuku hawa wamemsumbua Sabina kwa muda mrefu.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

Tumia sentensi moja moja kubainisha tofauti kati ya sentensi **sahili** na sentensi **ambatano** (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

r. Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mistari au mishale:

Mwanasiasa aliyewapuuza wanaeneo bunge lake amekomelewa. (alama 4)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

s. Andika katika usemi wa taarifa. (Alama 2)

"Karibu Bakari, tafadhali kaa", Maimuna alisema. "Asante, je, habari za nyumbani?" Bakari aliuliza.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

t. Taja aina ya yambwa iliyopigiwa mstari katika sentensi uliyopewa: (alama 1)

Mpishi amempikia <u>mgeni</u> wali vizuri.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**ISIMUJAMII (Alama 10)**

Kwa kutolea mifano, eleza sifa zozote nne za kimsingi za sajili inayoweza kutumika darasani. (alama 10)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

*Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)*

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: ………………………………………NAMBARI YA USAJILI: …………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ………………DARASA: …...........**

# MTIHANI WA PAMOJA WA SAMIA

**102/2**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA PILI**

**Maagizo**

- ***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
- ***b)*** *Jibu maswali yote.*
- ***c)*** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*
- ***d)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. UFAHAMU | 15 | |
| 2. UFUPISHO | 15 | |
| 3. SARUFI | 40 | |
| 4. ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |


**CONTACT US ON:**

WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003

EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**1. UFAHAMU:** **(alama15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata**

"Yakobo, eti babu yako ndiye mnyama? Siamini na sitaamini maneno hayo."

"Uliuomba ukweli."

"Kwa nini hukuniambia mambo haya zamani, Yakobo? Kwa nini mama yako hakunifunulia? Kwa nini aliisoma barua hii akaificha?"

"Yote hayo yalifanywa ili uwe na maisha bora. Ulipata wazazi wema waliokulea na kukutunza. Ulipelekwa shuleni, Chaanasa, mimi sikukanyaga shuleni. Ikiwa ungeachwa kinyongo, huenda hungekuwa na maendeleo uliyo nayo. Labda ungeingilia maisha mabaya na kuwa mtu bure kabisa. Zipo siri zinazowekwa ili kuwalinda watu."

Lakini, Yakobo, inaniuma sana. Miaka yote hii tumetembea pamoja, tumekuwa tukitembeleana, tumekula meza moja, tumefanya mambo mengi pamoja wala huniambii mimi ni mjomba wako."

Naomba msamaha, kwa moyo wangu wote, kwa kukosa kueleza mambo hayo mapema. Hata hivyo, ni vizuri kuona mambo kwa njia nyingi, si mtazamo mmoja tu. Tuseme, ningekuambia mambo hayo mapema, je, ungekuwa na furaha zaidi? Huenda jitihada zako za kumtafuta baba yako zingekutia chuki. Pengine hata ungetamani kulipiza kisasi kwa dhiki alizokuletea ukafungwa jela au hata kuhukumiwa kifo. Wakati mwingine, ni salama kutojua. Jambo usilolijua halikunyimi usingizi. Hata hivyo, naomba radhi kwa kutokuambia. Ukweli wa mambo ni kwamba hata Mzee Johari muungwana, yaani, babu yangu, au baba yako, hakujua mambo haya yote. Alikufa bila kujua sura au jina la mtoto wake: Chaanasa."

Bwana Chaanasa, bila kujua, alilia na kudondokwa na machozi kupukupu. Nikaona aibu kubaki hapo, lakini sikuondoka. Nilitaka kusikia hatima ya mazungumzo hayo.

"Yakobo, mpwa wangu," Bwana Chaanasa aliita huku akilia. Akanyoosha mikono yake na kumkumbatia Yakobo.

"Nimekusamehe. Nimekusamehe. Lazima nitekeleze ombi la mamangu. Alinisihi nisiwe na chuki na mtu yeyote. Siwezi kukuchukia mpwa wangu. Naahidi sitakuchukia kamwe. Asante kwa kuniambia ukweli wote. Asante pia kwa hekima yako kwani pia ulingoja hadi wakati unaofaa kunifunulia mambo haya. Ungaliyafunua zamani, kama ulivyosema awali, huenda nisingaliitikia jinsi nilivyofanya leo. Huenda mambo yangekuwa mabaya. Labda ningelipuka kwa hasira na kusababisha hasara, pengine hasara isiyolipika. Sasa ninaelewa kwa nini tunalandana sana nawe, na mzee Busara. Sisi ni wa damu moja. Baba yangu angalikuwa hai, ningalienda nikamwone na kujitambulisha kwake. Ningalimwita 'baba' na huenda angaliniita 'mwanangu.' Ningalimsamehe kwa kumwacha mamangu na kunitelekeza."

"Bado unaweza kumsamehe."

"Jinsi gani?" Bwana Chaanasa akauliza.

"Kwa kusahau yaliyopita na kuganga yajayo. Yazike mambo yote hayo katika kaburi la sahau. Acha ya kale yawe ya kale, ya nyuma yawe ya nyuma, ya zamani yawe ya zamani. Kilichotendeka kimekwishatendeka. Yaliyofanyika yamefanyika. Yamemwagika na hayatazoleka kamwe hata kwa kuchimbua ardhi. Lililopita limepita, si uwele tena.

"Naam, Bwana Chaanasa, lipitalo hupishwa."

**Maswali**

**(a)** Eleza sababu za Chaanasa kufichwa taarifa kuhusu babake. **(alama2)**

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**(b)** Thibitisha kuwa babu yake Yakobo alikuwa mnyama. **(alama2)**

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**(c)** Eleza umuhimu wa maswali balagha katika kifungu hiki. **(alama2)**

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**(d)** Je, ni kweli kuwa kama si kuweka siri mambo yangemharibikia Chaanasa? Tetea jibu lako. **(alama3)**

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

**(e)** Ni jambo lipi lililomfanya Chaanasa kumsamehe mpwa wake? **(alama2)**

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

**(f)** Kwa mujibu wa kifungu, kusamehe kuna matokeo gani? **(alama2)**

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

**(g)** Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu. **(alama2)**

**(i)** hayatakusanywa

……………………………………………………………………………………………………

**(ii)** pamoja

……………………………………………………………………………………………………

**2. UFUPISHO** **(alama15)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Maadili ni desturi, utamaduni au hulkaa mbazo hubainisha na kulipa kundi fulani la watu upekee wake. Maadili ni muhimu katika kuonesha imani na kanuni za maisha ambazo kundi Fulani la watu huchukulia kuwa chanya na zile wanazozichukulia kuwa hasi. Maadili ndio mwongozo unaothibiti matendo na hulka za kila mmoja.

Kila jamii huwa na maadili yake ambayo yanamhitaji kila mwanajamii kutenda na kuishi kama jamii inavyotarajia. Pia, yaliweza kulegeza mielekeo au mitazamo yao. Hata leo, maadili hutusaidia kubainisha sisini akina nani, mtazamo wetu maishani, pamojana matarajio yetu.

Katika Katiba ya Kenya, maadili ya jamii ya Wakenyayameangaziwavyema. Kwanza, ni wazi kuwa Kenya ni taifa la wacha Mungu, kwa hivyo, kila Mkenyaanatarajiwa kuabudu na kumheshimu Mwenyezi Mungu. Hili limeshadidiwa hata katika wimbo wetu wa taifa. Pamola na hayo, katika kuimarisha umoja wa kitaifa, tofauti zetuWakenya kirangi, kikabila, kitabakana hata kidini hazipaswi kutugawanya.Maadili yanatuhimiza kuzichukulia hizo kuwa sifa za kipekee na kuzionea fahari. Ule utaifa wetu kama wakenya unapaswa kuwekwa mbele daima ili kuzima juhudi zozote za kututenganisha kwa misingi hiyo.

Kama taifa, tunahitaji kudumisha uzalendo wetu kwa kujitolea kuhakikisha kuwa mahasidi hawaporomoshi maadili ya jamii zetukwa kuiga hulka zao potovu. Uzalendo unatuhumiza kuripoti vitendo vyote vya kuihujumu nci au watu wake kwa asasi za dola. Asasi hizo zitachunguza na kuzima utekelezaji wa uhalifu kabla haujatikea, na iwapo utakuwa umetokea, asasi hizo zitawapa adhabu wahalifu ili waweze kubadili mienendo mibaya na kuwa kielelezo kwa wengine wenye nia mbaya.

Maadili, vilevile, humwongoza mtu kuhusu namna za kutatua mizozo na kudumisha amani. Hatuwezi tukajivunia uhuru pasi na kuwepo amani. Amani ndio msingi wa umoja, ustawi na maendeleo ya taifa lolote. Ukosefu wa amani hudumaza na hata kurudisha nyuma maendeleo kwa kuwahini watu nafasi za kushiriki uzalishaji mali. Ukosefu wa amani vilevile husababisha kuongezeka kwa visa vya uhalifu kama vile mauaji, kulememazwa kwa watu, unajisi, uharibifu wa mali na kusambaratika kwa familia, hali ambayo huchangia mporomoko wa maadili katika jamii.

Uadilifu unakwenda kinyume na methali, amani haiji ila kwa ncha ya upanga. Ukweli ni kwamba, tunaweza kusuluhisha tofauti zetu bila kutumia silaha. Matumizi ya silaha aghalabu huzidisha uhasama na kuchochea haja ya kulipiza kisasi. Njia pekee ya kutatua migogoro ni kuelewa chanzo cha migogoro yenyewe, wahusika kufanya kikao na kuizungumzia kwa uwazi na kwa utulivu. Pande zote husika zinafaa kukubali makosa au madhara yaliyotokana na matendo yao na kuomba msamaha ili kupata maridhiano. Kuomba msamaha kusidhaniwe kuwa kujishusha hadhi, bali ni unyenyekevu katika kutatua tofauti kwa manufaa ya muamala wa vizazi vijavyo. Anayeombwa msamaha naye anapaswa kuwa tayari kutoa shifaa kwa dhati na kusahau kosa alilofanyiwa. Yote haya yakishindikana, mgogoro wapaswa kupelekwa mahakamani. Haki za kila mmoja zimelindwa katika katiba yetu na mahakama zipo ili kutetea haki hizi bila kupendelea upande wowote.

Utiifu wa sheria vilevile ni njia mojawapo ya kukuza maadili ya kijamii. Kwa kuwa sheria hulinda haki za kila mtu; wake kwa waume, wakubwa kwa wadogo, kila mmoja ana wajibu wa kuheshimu sheria. Hii ni pamoja na kulinda rasilimali zetu kama jambo la wajibu bila ya kutegemea kuwepe wadumisha sheria. Uongozi wa kisheria huwapa watu hakikisho kuwa maisha yao hayatakuwa kama ya mahayawani nyikani bali yatafuata utaratibu Fulani. Hivyo basi, sheria ni hakikisho la jamii inayolinda haki na kuendesha mambo yake kwa uwazi, haki na ushwari.

Bila shaka, tukizingatia na kuimarisha maadili, taifa letu litakuwa jamii bora na kivutio cha kila mtu. Kiu ya Wakenya ya kutaka kuhamia nchi nyingine, hasa zilizostawi, itapungua. Wote watakuwa na ari ya kuliendeleza taifa lao.

**Maswali**

**(a)** Eleza umuhimu wa maadili kwa jamii na taifa kwa ujumla. (maneno 60-70)
**(alama 7 , 1 ya utiririko)**

**(b)** Fafanua jinsi mizozo inaweza kutatuliwa kwa uadilifu. (Maneno 75-80)
**(alama8, 1 ya utiririko)**

**3. MATUMIZI YA LUGHA** **(alama40)**

**(a)** Linganua sifa za konsonati katika maneno yafuatayo: **(alama2)**

**(i)** Shule

……………………………………………………………………………………………………

**(ii)** Cheza

……………………………………………………………………………………………………

**(b)** Onyesha silabi inayotamkwa kwa mkazo katika maneno yafuatayo **(alama2)**

**(i)** Waliotusherehekea

…………………………………………………………………………………………………….

**(ii)** Wafanyakazi(watu wanaofanya kazi)

…………………………………………………………………………………………………….

**(c)** Eleza majukumu ya viambishi awali katika neno: Waliotuhangaisha **(alama2)**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**(d)** Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? **(alama2)**

**(i)** Kuta

…………………………………………………………………………………………………….

**(ii)** Rafiki

…………………………………………………………………………………………………….

**(e)** Tunga sentensi yenye kitenzi kishirikishi kikamilifu **(alama1)**

……………………………………………………………………………………………………

**(f)** Andika upya sentensi zifuatazo kwa kufuata maagizo: **(alama8)**

**(i)** Mahali palipotayarishwa pamejaa waumini waliotoka nchini kote.
(Tumia kirejeshi amba)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**(ii)** Mwanamichezo hodari amevunja rekodi ya dunia.
(Anza kwa: Rekodi **…...**)

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**(iii)** Mtafiti huyu alipewa tuzo nyingine.
(Tumia kiashiria kisisitizi)

…………………………………………………………………………………………………………

**(iv)** Nilimwomba rafiki yangu **anisamehe** baada ya kumkosea heshima mkutanoni
(Badilisha neno lililopigiwa mstari liwe nomino)

…………………………………………………………………………………………………………

**(g)** Bainisha kikundi nomino na kikundi tenzi katika sentensi ifuatayo **(alama2)**
Vitabu vyote kumi na saba vimepelekwa maktabani.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**(h)** Andika sentensi ifuatayo katika udogo wingi **(alama2)**
Mtu huyu atanunua shamba mwaka ujao.

…………………………………………………………………………………………………………

**(i)** Eleza hali zilizotumika katika sentensi zifuatazo: **(alama2)**

**(i)** Halati humpikia nyanya.

…………………………………………………………………………………………………………

**(ii)** Juma ameingia kanisani

…………………………………………………………………………………………………………

**(j)** Andika kwa wingi: **(alama2)**
Ufito huu ni mzito na mrefu mno.

…………………………………………………………………………………………………………

**(k)** Tunga sentensi mojamoja ukitumia alama za kuakifisha zifuatazo:

**(i)** Alama za dukuduku **(alama2)**

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**(ii)** Mshangao **(alama1)**

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**(l)** Rafiki yetu alituambia kuwa ataondoka keshoye kuelekea Afrika kusini kwa masomo ya chuo kikuu
(Andika kwa usemi halisi) **(alama2)**

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**(m)** Changanua kwa mstari **(alama2)**
Rais aliwafadhili raia waliokuwa wamesajiliwa pekee.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**(n)** Ainisha vielezi katika sentensi zifuatazo: **(aslama2)**

**(i)** Tuliondoka nyumbani usiku wa manane

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**(ii)** Alimpiga rungu mara mbili jana jioni.

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**(o)** Ainisha virai katika sentensi ifuatayo: **(alama3)**

Mwanafunzi mwenye kitabu cheusi ameingia ndani ya darasa.

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**(p)** Bainisha chagizo na shamirisho katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Wachuna chai walifanya kazi hiyo kwa uvivu mwingi ajabu.

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**(q)** Eleza maana ya methali ifuatayo: **(alama1)**

Chui na mbuzi hawala nyumba moja.

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**4. ISIMUJAMII** **(alama10)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

"Niaje buda, umecheki yule morio wetu? Nikama amefyatu kiplani. Itabidi tuache drugs bro venye kunaenda si poa……"

**(a)** Tambua Sajili hii **(alama2)**

……………………………………………………………………………………………………

**(b)** Eleza sifa nne ambazo hujitokeza kwenye Sajili hii **(alama4)**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

Toa sababu nne zinzopelekea vijana kutumia lugha hii **(alama4)**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

# GOLDLITE ONLINE SUPPLIES

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari kenya(kcse)***

# MITIHANI YA PAMOJA YA SHULE ZA KITAIFA 2025

**JINA: ……………………………………………NAMBARI YA USAJILI: ………………………….**

**SAHIHI YA MTAHINIWA: ……………………TAREHE: ………………DARASA: …...........**

# MTIHANI WA PAMOJA WA SUKELEMO

**102/2**

**KISWAHILI**

**MAAGIZO**

- ***a)*** *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
- ***b)*** *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
- ***c)*** *Jibu maswali **yote.***
- ***d)*** *Majibu yako yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
- ***e)*** *Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
- ***f)*** *Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*
- ***g)*** ***Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

**Kwa matumizi ya mtahini pekee.**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | **15** | |
| 2 | **15** | |
| 3 | **40** | |
| 4 | **10** | |
| **Jumla** | **80** | |

**CONTACT US ON:**
WhatsApp/Call or Text 0724351706/0726960003
EMAIL: Goldlitepublishers@gmail.com

**SEHEMU YA A: UFAHAMU (Alama 15)**

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali**

"Hamjambo wananchi?Ni fursa kubwa kusimama hapa kwa niaba ya wachukuzi, makuli na wote wanaoonewa.Kilichotuleta hapa ni kufahamishana kwamba tumeamua kugoma kuanzia keshokutwa.Sababu za kugoma sote tunazielewa kwani tumeshaelezeana zamani ; sana ni dharau ,maonevu , kazi tuifanyayo na marupurupu tunayolipwa. Haya yote hayaturidhishi. Mengine mengi mnayaelewa.Mgomo wetu hata kama hautafuzu, utasaidia kuona matokeo kama wasemavyo wahenga gonga gogo usikilize mlio.Hatuna budi kuwajaribu hawa wanaotunyanyasa.Lazima tuwaonyeshe kuwa sisi wanyonge ndio msingi wa pato la nchi hii.Mgomo huu ni mwanzo wa kuwajulisha kwamba wakati wa mtu mweusi kujua haki yake umefika-mwanzo wa kutetea haki zetu.

Bakari aliyabubuja maneno haya yaliomganda ubongoni mwake kutokana na makala moja ya siasa aliyopewa aisome kwa siri na Kumba ,makala ambayo angekamatwa nayo ,leo hii asingekuwa kasimama hapo alipo.Alimeza mate.Haikuwa hotuba maalum ya mwanasiasa ya kushawishi,bali ni maneno yaliokuwa wazi ,yaliotiririka kwa urahisi wa kufahamika.Madhumuni yake yalikuwa dhahiri.Alisikizwa kwa makini.

"Bahati nzuri,"aliendelea,"hapa shamba kumeingia mzozo wa ng'ombe wa kulazimisha wananchi wawapige sindano. Sisi tulio mjini tumesikia kwamba ndugu zetu mnataka kugoma kupeleka ng'ombe wetu wakapigwa sindano kwa sababu wanakufa,"Alisita tena akameza mate.

Mzee Gae alikohoa kwa muda. Alipomaliza, Bakari aliendelea, "Hapana anayetambua faida ya ng'ombe hao kupigwa sindano ,maana ng'ombe wetu wamekuwa wakiugua na kupona wenyewe ;au kama ipo faida yoyote ,hakuna aliyejishughulisha kuwaeleza wafugaji. Na kwa nini wafe?Iwapo ipo sababu ya ng'ombe hao kufa ,hapana aliyekuja kuwaongoza wafugaji basi. Wazungu wanataka kuwapiga ng'ombe sindano tu ; ikiwa watakufa au wataokoka si shauri lao.Pia tumejifunza kutoka kwa nchi jirani ,upigaji sindano umeteketeza ng'ombe na watu na wafugaji hawakukaa kimya.Tunakuungeni mkono."Alimeza mate tena ,kisha aliendelea,"Pia hapana asiyeuelewa uovu waliotendewa wakuliama ,wa kuvunjiwa nyumba zao na kunyang'anywa ardhi bora ya kulimia ili kujenga kiwanja cha ndege bila fidia madhubuti. Hatujui ndege zinazoruka na kutua zina manufaa gani kwa mfugaji?

Kwa haya machache yatosha kuonyesha ya kwamba wakulima nao wanastahili kuunga mkono kwa kutoleta mazao yao mjini.Tunajua mabwana wakubwa hawawezi kuishi bila chakula,"Bakari aliimaliza maneno yake bila kutarajiwa.

"Sisi wakulima tulikutana tukashauriana na kuamua tusipeleke mazao yetu mjini"alidakia Hassan.

Kumba aliwaeleza wazi wakulima na wafugaji umuhimu wa mgomo huo , wajibu wao na hatari yake.Aliwafafanulia luwa mapambano hayo yalikuwa ni baina ya wenye silaha na walio mikono mitupu na ushindi wao uliegemea sana ushirikiano wao.

**Maswali**

**a)** Sababu za migomo zilikuwa zipi? (alama 4)

**b)** Je,mgomo huu uliwahusu kina nani?(alama 2)

**c)** Wagomaji hawakuwa na matumaini ya kupata ushindi.Thibitisha.(alama 2)

**d)** Kulingana na taarifa ,lengo la mgomo lilikuwa lipi? (alama 2)

**e)** Wakulima walitendewa maovu.Elezea.(alama 2)

**f)** Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika kifungu;(alama 3)

- ***i.*** Tunakuungeni mkono.
- ***ii.*** Wakapigwe sindano
- ***iii.*** Fidia

**SEHEMU YA B; MUHTASARI (Alama 15)**

**Soma taarifa kisha ujibu maswali;**

Nidhamu kwa vijana ni tadbiri ambayo tangu zamani imekuwa ikipigiwa upatu sana.Maisha yanazidi kubadilika ,vijana wanasoma na kuona mengi yakibadilisha mazingira yao kila wakati na hata wanakutana na wenzao kutoka pande zote za ulimwengu basi wanafaa kudhibitiwa .Bila ya kufanya hivyo wataharibika sana.

Wengine kwa uhayawani wao huchukulia kuwa wazazi walio nayo ni ovyo .Wanadai kuwa wao hawakuomba kuzaliwa na wazazi kama hao.Wengine huwaibia wazazi wao au hata kuwapangia wezi.Wengine huwashika wazazi kabari na kuwatishia na kifo.Isitoshe, kuna wale wanaopigana na wazazi wao. Ama kweli dunia hii imekwisha aisee! Badala ya mshikamano wa bega kwa bega na wazazi , imekuwa ni kutoelewana na kuzozana.

Kuzaliwa kwa watoto na wazazi wa aina fulani ama wazazi kuzaa watoto wa aina fulani ni majaliwa ya Mwenyezi Mungu .Hakuna mzazi anayeketi na kuomba azae mtoto atakayemsubu mbele ya watu.Ni mzazi gani atakayeomba mtoto asiye na shukrani wa kumshikia panga?Abadani! Humpati mzazi kama huyo.

Wanapokanywa vijana juu ya mienendo yao ya kutembea na marafiki wabaya ,wao hufura kama andazi lililoumuliwa kwa hamira nyingi.Hawatulii na kusikiliza mawaidha ila wao hujikinga tu katika dhania kuwa marafiki wao ndio bora kabisa kuliko wazazi wao.Wao husahau kuwa damu ni nzito kuliko maji.Mambo wanayoyakamia kuyafanya yanapotumbukia nyongo ,hapo ndipo wanaketi chini na kushika tama.Wakati

mwingine ubishi wao huwazushia makuu yanayowakalifu maishani mwao huku marafiki waliowaingiza gizani kuwatoroka.

Mara nyingi mzazi huwa hana kinyongo na mwanawe.Mtoto wake anapokuwa na shida,mzazi hujikokota hadi aliko mwanawe asikilize shida zake na kujaribu juu chini kumsaidia.Mzazi hamsuti wala kumkumbusha kuhusu ubishi wake wa awali ingawa anajua  ukweli kuwa asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

Jambo linalowachoma moyo wazazi wengi ni kuwa watoto wengi wa siku hizi hawawazi watakavyowasidia wazazi wao au watakavyowaridhisha!Badala yake,wanapoteza muda mwingi kusugua bongo zao wakitafuta njia za kuwachafua roho wazazi wao.Badala ya kujiuliza "Nina lipi linalowapendeza wazazi wangu?",wengi wao hujiuliza "Mbona leo sijatenda jambo la kumwuudhi mzazi wangu?"Wahenga walisema 'ujana ni tembo la mnazi' na ni kweli kabisa ujana hulipua akili za wana hawa.Badala ya kutenda yenye jaza, wao hutenda ya kufurahia ya tandabelua.Badala ya kuona kuwa kuna  wakubwa wanaopaswa kuwaheshimu, ni kama wakajizaa wao na  ndio wanaopaswa kusujudiwa na kupigiwa magoti.Hupenda kuzuzuka na huwa wepesi wa kuzuzuliwa na hao vinyago na vigezo wenzao.

Kila wakati msamiati wao ni ,"Nipe!Sijafanya makosa!Hamnipendi! Stasoma!"na kujifanya wajasiri na werevu kuliko wazazi.Badala ya kutumia maneno yenye nyama ya ulimi, wao ni kufuka kama chungu cha pure kilichocholewa moto mwingi. Kwa nini watoto hawa wasibadilishe msamiati  na kutumia maneno kama 'chukua baba na mama,samahani mama au baba, ahsante kwa yote mnayonifanyia, nitasoma kwa bidii na kadhalika?'Unyeyekevu, heshima, shukrani, usaidizi, wema na kuwa na uelewa wa hali za wazazi ,utaweza kuwafanya wazazi kuwatendea wana wao kila jambo waliwezalo kwa mioyo mikunjufu.Maneno matamu humtoa nyoka pangoni.Ukali wowote unaofikiriwa uko kwa wazazi hautakuwepo tena. Suluhu itapatikana katika kila tatizo na wazazi na watoto wao wataishi kwa Amani.

**Maswali**

**a)** Kwa nini mwandishi anasema kuwa vijana wa siku hizi wamekosa adabu na heshima? (maneno 40-45)

(alama 10)

**b)** Fafanua umuhimu wa nidhamu kwa vijana (maneno 20-30) (alama 5)

**SEHEMU YA C; MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

**a)** Kwa nini sauti /y/ na /w/ zinaitwa nusu irabu? (alama 2)

**b)** Toa maifano ya silabi ambayo ni konsonanti pekee.(alama 2)

**c)** Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya mkwaju (/) kama zilivyoangaziwa;(alama 2)

i. kuonyesha 'au'

ii. katika uandishi wa tarehe

**d)** Andika sentensi hii kwa wingi

**e)** Pendekezo la mwanahabari huyo litaandikwa kwenye tangazo.(alama 1)

**f)** Ondoa kivumishi kilichoka katika sentensi hii na utumie kiashiria cha kuthibitisha cha karibu.

Mchezaji mwingine anaingia uwanjani. (alama 2)

**g)** Kanusha sentensi hii (alama 2)

Kula kwake kumehujumiwa na ugonjwa huo.

**h)** Tumia kihusishi hiki katika sentensi

Mkabala na (alama2)

**i)** Tumia vishale kuainisha sentenzi hii (alama 4)

Mwanamume mwanajeshi alifika jana jioni.

**j)** Andika upya sentensi hii ukizingatia kinyume cha neno lililopigiwa mstari(alama 1)

Mwana **aliyekufa** ni wa nyanya.

**k)** Tunga sentensi moja kuonyesha maana ya maneno haya;

Twaza, tweza

**l)** Ainisha viambishi awali, mzizi na viambishi tamati katika neno hili(alama 3)

Walichezana

**m)** Tumia kiwalishi cha pekee –ingine kuandika upya sentensi hii (alama 2)

Watoto watatu warefu wameingia ofisini.

**n)** Unganisha sentensi hizi ukitukia kiunganishi ingawa.(alama 2)

Alienda kwake mapema sana.

Bado hakumkuta.

**o)** Tunga sentensi yenye mpangilio huu wa maneno.(alama 2)

T+T+T+T+T+E

**p)** Eleza sifa moja ya nomino katika ngeli ya LI-YA (alama 1)

**q)** Unda vitenzi kutokana na vivumishi hivi;(alama 2)

i. Nadhifu

ii. msomi

**r)** Huku ukitoa mifano tofautisha kati ya mofimu huru na mofimu tegemezi (alama 4)

**s)** Onyesha chagizo katika sentensi hii.(alama 2)

Rehema alimpikia chakula haraka zaidi.

**t)** Tunga sentensi uktumia labda kuleta maana zifuatazo.(alama 2)

i. Yawezekana

ii. Pengine

**D. ISIMUJAMII (alama 10)**

Taj ana ueleze dhima ya lugha .(alama 10).